ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 26 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha Baraza cha tarehe 16 Mei, 2017, Mhe. Zulfa Mmaka Omar aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kuwasomea majibu hayo kwenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar alitaka kujua ni vijana wangapi waliopatiwa mafunzo ya Ujasiriamali yatakayowawezesha kujiajiri Unguja na Pemba, na ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kuwapatia mikopo nafuu vijana pamoja na vijana wangapi waliopatiwa mikopo Unguja na Pemba na majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

a) Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya wajasiriamali vijana 420, Unguja 300 na Pemba 120; wanaume 150 na wanawake 370 walifaidika na mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalihusisha uanzishaji wa biashara, utengenezaji wa bidhaa mbali mbali na utafutaji wa masoko.

b) Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 jumla ya Tshs.354,760,000/= zilitumika kuwapatia mikopo nafuu vijana 1,278; Unguja 909 na Pemba 369. Kati ya hao wanaume 517 na wanawake 761.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni sana. Naomba kuwasilisha.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamida Abdalla kwa niaba ya Mwenyeki wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Waheshimiwa Wajumbe kwa vile hoja yetu leo ni ya Mhe. Waziri kutokana na nafasi na muda leo kutakuwa hakuna maswali na majibu. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri moja kwa moja aje awasilishe.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya mwaka 2017/2018 - Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba sasa niwasilishe hotuba ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama nilivyowasilisha taarifa hivi asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ajili kwa ya kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu yaani (*PBB*).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma na Utukufu, kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambapo asilimia kubwa wanajihusisha na kazi za kilimo, ufugaji, uvuvi na uhifadhi wa maliasili.

Mhe. Mwenyekiti, kipekee naomba kumpongeza Mhe, Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambae pia ni Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kuiongoza nchi yetu katika misingi ya utulivu, amani na siasa safi. Aidha, tunampongeza kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kufanikisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa lengo la kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukuwa nafasi hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, ambae pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, kwa kutupa miongozo, maelekezo na michango yake pamoja na kuimarisha ushirikiano wa ndani na nje ya nchi yetu katika maendeleo ya sekta ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na mwenyekiti mwenzako wanaokusaidia kuliongoza Baraza lako tukufu. Tunakuombea dua kwa Mwenyezi Mungu wewe pamoja

na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi akuzidishieni baraka, hekima na busara ili mpate wepesi wa kuliendelesha Baraza hili kwa utulivu na mafanikio makubwa Amin.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii ya pekee kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa miongozo na ushauri waliotoa kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi, kwa kufanikisha utekelezaji wa malengo katika bajeti ya wizara kwa mwaka 2016/2017.

Aidha, tunaishukuru kamati kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya wizara ya mwaka 2017/2018. Naihakikishia kamati yako kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupa tumeyazingatia katika bajeti hii tunayoiwasilisha.

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA 2016-2017

Mhe. Mwenyekiti Sekta ya Kilimo inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar na inatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, ambapo asilimia 40 ya wananchi wameajiriwa na sekta hii; na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii kwa njia moja au nyengine katika kujipatia kipato na kuimarisha maisha yao. Kwa mwaka wa fedha 2016 sekta hii imechangia asilimia 25.7 ya pato la Taifa na imekuwa kwa asilimia 5.7 mwaka 2016, ikilinganishwa na 2.5 ya mwaka 2015.

Aidha, sekta bado inalo jukumu kubwa la kuwawezesha kikamilifu wakulima, wafugaji na wavuvi kwa kuwajengea miundombinu, kuwapatia pembejeo, utaalamu na nyenzo za kufanyia kazi ili waongeze uzalishaji wenye tija. Hali hii itawawezesha wananchi kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada kwa ajili ya biashara, kuwa na uhakika wa chakula na hatimae kupunguza umasikini.

HALI YA UZALISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa mavuno kwa baadhi ya mazao ya chakula na biashara mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. Zao la Karafuu limeongezeka kutoka tani 3,322 mwaka 2015 hadi kufikia tani 4,678.69 mwaka 2016, viazi vikuu kutoka tani 2,408.5 mwaka 2015 hadi tani 3,519.92 mwaka 2016, Muhogo kutoka tani 132,641.32 mwaka 2015 hadi tani 133,412.80 mwaka 2016, ndizi kutoka tani 47,494.7 mwaka 2015 hadi tani

55,454.7 mwaka 2016 na mbaazi zimeongezeka kutoka tani 592.99 mwaka 2015 hadi tani 1,414.42 mwaka 2016. Mboga (tungule, nyanya, bilingani, bamia, mchicha, matikiti, tango na pilipili) kutoka tani 15,715 mwaka 2015 hadi kufikia tani 27,256 mwaka 2016. (Angalia kiambatisho nam. 1).

Mhe. Mwenyekiti, Ongezeko la uzalishaji limechangiwa na matokeo ya utafiti, taaluma inayotolewa kwa Mabibi na Mabwana shamba katika utumiaji wa mbinu bora za kilimo cha kisasa na upatikanaji wa mikopo kupitia mfuko wa uwezeshaji uliopo chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Aidha, hivi karibuni kumejitokeza vikundi vya *SACCOS* vinavyotoa mikopo kwa wakulima pamoja na kuimarika kwa maduka ya pembejeo na zana za kilimo vijijini. Sekta binafsi pia zimechangia kiasi kikubwa katika kuongeza uzalishaji hasa kwa mazao ya chakula na mboga wakiwemo *TAHA, ZAIDI, TAPP, Milele Foundation, VSO* na *TOAM*.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zimeonesha pia kuwepo kwa ushukaji wa uzalishaji kwa baadhi ya mazao ya chakula yakiwemo mpunga kutoka tani 29,082.7 mwaka 2015 hadi tani 4,343.80 mwaka 2016, viazi vitamu kutoka tani 55,765.1 mwaka 2015 hadi tani 24,834.30 mwaka 2016 na Mahindi kutoka tani 2,826.70 mwaka 2015 hadi tani 891.73 mwaka 2016. Sababu zilizochangia ushukaji wa mazao ya kilimo ni pamoja na upungufu mkubwa wa mvua za masika msimu wa mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, sababu nyengine ni kupungua kwa eneo lililolimwa mazao ya chakula ikiwemo viazi vitamu kutoka ekari 7,966.46 mwaka 2015 hadi ekari 3,547.76 mwaka 2016, mahindi kutoka ekari 5,652.21 mwaka 2015 hadi ekari 1,783.46 mwaka 2016 na mtama kutoka ekari 1,425.57 mwaka 2015 hadi ekari 458.00 mwaka 2016. Hii ilisababishwa na kuhama kwa wakulima walio wengi kutoka kilimo cha mazao ya asili ya chakula na kulima mazao ya mboga na matunda ambayo ni ya muda mfupi na yenye tija ya haraka. Aidha, mabadiliko ya tabianchi yamechangia kupungua kwa uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua na mazao mengine. (Angalia kiambatanisho namba 2)

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea na usimamizi na uhifadhi wa misitu na maliasili zisizorejesheka, takwimu zinaonesha ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya kuni kutoka mita za ujazo 18,573 mwaka 2015 hadi kufikia mita za ujazo 19,532.25 mwaka 2016, Boriti mita za ujazo 2,325 mwaka 2015 hadi kufikia mita za ujazo 2,457 mwaka 2016. Kwa mazao ya maliasili zisizorejesheka kumekuwepo na ongezeko la uchimbaji na matumizi ya mawe kutoka tani 74,373 mwaka 2015 hadi tani 81,377 mwaka 2016 na mchanga

kutoka tani 490,576 mwaka 2015 hadi kufikia tani 576,476 mwaka 2016. Hii imetokana na ukuaji wa sekta ya ujenzi wa majengo na barabara mjini na vijijini pamoja na wananchi kutotumia njia mbadala za vifaa vya ujenzi. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwawezesha wananchi katika kupunguza matumizi ya nishati ya kuni kwa kutumia majiko sanifu, gesi salama na kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nishati na Mazingira na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tunaendelea na utafiti wa kuhamasisha matumizi mbadala ya vifaa vya ujenzi, badala ya kutegemea mchanga na mawe pekee.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mazao ya mifugo na uvuvi takwimu zinaonesha pia kuwepo kwa ongezeko la mayai kutoka 184,546,967 mwaka 2015 hadi kufikia jumla ya mayai 186,163,932 mwaka 2016, maziwa kutoka lita 34,983 mwaka 2015 hadi kufikia lita 40,895,412 mwaka 2016. Aidha, takwimu zinaonesha kupungua kwa idadi ya ng'ombe waliochinjwa kutoka 23,677 mwaka 2015 hadi 20,710 mwaka 2016, mbuzi kutoka 2,605 mwaka 2015 hadi 1,625 mwaka 2016 na kuku kutoka 1,104,004 mwaka 2015 hadi kufikia kuku 707,792 mwaka 2016 (Angalia kiambatisho nam. 3).

ii imetokana na ongezeko na uingizaji wa nyama ya kuku na maini ambayo yanauzwa kwa wastani wa TZS. 4,500 kwa kilo moja kupitia Kampuni za *ZANCHICK, MALIK FARAJ* na *FARID* ambazo zinaingiza wastani tani 438,251 kwa mwaka. Lengo la Wizara ni kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa kuku wa nyama kibiashara ili kampuni hizi zinunue kuku waliozalishwa ndani ya nchi. Hii itasaidia kutoa ajira kwa makundi ya vijana ambao kwa kiasi kikubwa hivi sasa wamebaki bila ya ajira ya maana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mazao ya baharini nayo yamepungua ikiwemo Samaki kutoka tani 34,104 mwaka 2015 hadi tani 33,892.5 mwaka 2016 na mwani kutoka tani 16,665 mwaka 2015 hadi tani 11,113.3 mwaka 2016. Hali halisi ya sasa inaonesha sehemu ya samaki na mazao ya baharini (majongoo na kamba) yanasafirishwa na kupelekwa Tanzania Bara na nchi za jirani ikiwemo *DRC*. Sababu za kupungua uzalishaji wa samaki ni kuongezekwa kwa uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi vijana na kupelekea uharibifu wa matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki. Aidha uzalishaji wa zao la mwani umepungua kutokana na kupungua kwa bei ya mwani, kuibuka kwa maradhi ya zao hilo pamoja na kuwepo kwa mabadiliko ya tabianchi.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mipango na Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (ATI).

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imepangiwa kukusanya jumla ya TZS. 2.82 Billioni kutokana na vyanzo vyake 11 vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 Wizara imekusanya TZS. 3.10 Billioni sawa na asilimia 110.2 (Angalia kiambatisho nam. 3).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS. 48.98 Billioni kutekeleza Programu tano, kati ya hizo TZS. 15.74 Billioni kwa kazi za kawaida (TZS. 10.96 Billioni Mishahara, TZS. 4.24 Billioni matumizi mengineyo na TZS. 551.50 Millioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani). Aidha, kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 Wizara imepata TZS. 14.36 Billioni kati ya hizo TZS. 9.87 Billioni Mishahara, TZS. 3.99 Billioni matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 492.79 Millioni ikiwa ni Ruzuku sawa na asilimia 91 ya makadirio (Angalia kiambatisho nam 4).

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za Miradi ya maendeleo, Wizara imeidhinishiwa TZS. 33.23 Billioni ambapo (TZS. 32.17 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS. 1.07 Billioni ni kutoka SMZ). Kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 Wizara imepata TZS. 7.54 Billioni kati ya hizo TZS. 6.95 Billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS. 590.44 Millioni kutoka SMZ sawa na asilimia 23 ya makadirio (Angalia kiambatisho nam. 5).

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imepata mafanikio yafuatayo:

a) Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwemo kampuni ya ZAIDI na TAHA zimeendelea na kazi ya uhamisishaji wa wakulima katika matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji maji kwa matone na green houses katika mazao tofauti ambapo wakulima 100 wa mpunga, ndimu na mboga wamepatiwa vifaa na mashine za kumwagilia maji vyenye thamani ya Tsh. 200,000,000 kupitia programu ya *ASDP*-L.Vilevile wakulima 600 wa umwagiliaji maji kwa matone (400 Unguja na 200 Pemba) wametambuliwa na taarifa zao kuhifadhiwa kwa lengo la kutathmini mafanikio yao;

b) Mtambo wa kukamulia alizeti, wenye thamani ya Tsh. 27,000,000 umenunuliwa. Mtambo huo wenye uwezo wa kukamua tani 4.5 kwa siku umefungwa kituo cha Ole- Dodeani Pemba. Aidha, lita 970 za mafuta ya alizeti zimekamuliwa katika Mtambo uliopo Bambi Unguja;

c) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 1,560 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50 haikufanyika kutokana na kutopatikana Mkandarasi aliyekidhi vigezo kupitia zabuni ya mwanzo. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na mshauri mwelekezi (*KRC JV DASAN*) wanaendelea na matayarisho ya kurudia taratibu za zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji baada ya *EXIM* Bank ya Korea kukubali kurudiwa kwa zabuni hiyo;

d) Kushajiisha wafugaji kuongeza nyama ya Kuku kufikia kilo 663,279, mayai kufikia 184,547,096 na maziwa kufikia lita 36,732,196 kwa mwaka 2017. Wizara imefikia malengo iliyojiwekea kwa uzalishaji wa nyama ya kuku kufikia asilimia 124, maziwa asilimia 116 na mayai 100;

e) Wizara imeendelea kuimarisha huduma za kinga na tiba ya mifugo ili kupunguza maradhi. Jumla ya wanyama 220,329, wamechanjwa na kutibiwa wakiwemo ng'ombe, kuku, mbuzi, sungura, paka na mbwa. Aidha, Wizara imetumia Tsh. 52.00 Milioni kwa matengenezo ya maabara ya Kichaa cha Mbwa Maruhubi na Wete, ujenzi wa karantini ya mifugo Donge Muwanda pamoja na ukarabati wa kituo cha mifugo Makangale na ofisi za A.I umefanyika;

f) Wizara imeendelea na juhudi za kuimarisha uvuvi katika kina kirefu cha maji kwa kuanzishwa na kusajiliwa rasmi kwa Kampuni ya Uvuvi

(*ZAFICO*) kwa mtaji wa Tsh. bilioni saba zitakazofadhiliwa na mashirika ya ndani ya Zanzibar. Aidha, Wizara imekaribisha kampuni za Demko (Ugiriki) na *Hongdong Investments Co. Ltd* (China) ambazo tayari zimepata kibali kutoka *ZIPA*;

g) Wizara ya Kilimo imesaini Mkataba na Kampuni ya *RANS* wenye thamani ya Tsh. 235,000,000 kwa ajili ya kukamilisha Ukarabati wa Ghala la Akiba liliopo bandarini Unguja. Mkataba huo umeanzia Mei, 2017 hadi Agosti, 2017;

h) Vijana 69 wamejiunga na mafunzo katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani kwa muhula wa 2017/2018 sawa na asilimia 69 ya lengo. Vijana 112 wamehitimu mafunzo yao 61 ngazi ya cheti na 51 stashahada za kilimo kwa mwaka 2016. Pia vijana wapya 5 wa kada maalum sawa na asilimia 50 ya lengo wamejiunga katika fani ya Udaktari wa wanyama nchini China;

i) Tafiti na majaribio 11 ya mbinu za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara yakiwemo zimefanyika mpunga (4), muhogo (3), viazi vitamu (1), mboga (1) na minazi (2) sawa na asilimia 92 ya lengo.

j) Uhakiki wa vyombo, majengo na mashamba mawili (Kilombero na Kibokwa) umefanyika kwa lengo la kurekebisha taarifa za daftari la mali za Wizara;

k) Wizara imeendelea kushajiisha na kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi katika masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kufungua duka la bidhaa za Kilimo Maruhubi ili kuwaunganisha na masoko. Aidha, vikundi 127 vya vijana kutoka Wilaya zote za Zanzibar vimeunganishwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwa ajili ya utaratibu wa kupatiwa mikopo.

l) Wizara pia imelipia Tsh. 269 Milioni sawa na asilimia 75 ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya ununuzi wa mashine saba (7) za usarifu na kuongeza thamani mazao ya Mpunga, Mwani, Madagaa, Ndimu na Mboga. Jamii tayari zimelipia Tsh. 89 Milioni ikiwa ni asilimia 25 kwa mujibu wa utaratibu wa mradi;

m) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na jitihada za kuwatafutia soko wakulima wa mwani, vilevile Wizara imefanya Kongano la siku ya mwani kwa kuzindua bidhaa 40

zinazotokana na mwani mnamo tarehe 24/8/2016 huko Pwani Mchangani kwa lengo la kuendeleza soko la ndani la bidhaa hiyo. Aidha, utafiti wa matumizi ya mwani kwa viwango tofauti katika chakula cha kuku umekamilika ambapo umeonesha kuongezeka kwa uzito na siha ya kuku wa nyama kutoka kilo 1 hadi kilo 2.5 kwa kipindi cha wiki saba; Wizara pia kupitia programu ya *MIVARF* imelipia asilimia 75 ya gharama na vikundi viwili kutoka Kidoti na Paje vimechangia asilimia 25 ya fedha kama ilivyo katika makubaliano ya mradi;

n) Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi inaendelea kudhibiti wimbi la uvamizi wa maeneo yote ya kilimo, misitu na mifugo kwa kushirikiana na Wilaya na Halmashauri zake. Kamati ya Wataalamu wa Wizara mbili hizi imeundwa kwa ajili ya kuyapitia na kuyapima maeneo yote ya Kilimo ili yaweze kudhibitiwa kisheria. Kazi hii inaendelea;

o) Utoaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo cha Mpunga kupitia jumuia za wakulima umeendelea. Tani 350 za mbegu ya mpunga, tani 700 za mbolea (100 TSP na 600 *UREA* - Unguja 350 na Pemba 350) na lita 15,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa na kusambazwa (9,000 Unguja na 6,000 Pemba). Aidha, Taratibu za manununzi ya Matrekta 20 na zana zake zenye thamani ya Dola za kimarekani 540,827 kutoka kampuni ya *MAHINDRA* ya India zimekamilika;

p) Jumla ya Miche ya Mikarafuu 636,847 imeoteshwa katika vitalu vya Serikali (105,700 Unguja na 237,169 Pemba) na katika vitalu vya watu binafsi miche 293,978 (17,746 Unguja na 276,232 Pemba) sawa na asilimia 64 ya lengo;

Wizara imeshajiisha wakulima kutumia mezani kupima bidhaa zao kwa lengo la kupata vipimo sahihi. Aidha, Wizara imakamilisha awamu ya kwanza ya utafiti wa kutathmini uzito wa mafungu ya mazao kwa ajili ya kupata vipimo sahihi kulingana na bei.

Gari nane (8) na Pikipiki 53 zimenunuliwa na Wizara kupitia fedha za SMZ, Miradi ya SwioFish, ERPP na *MIVARF*. Vyombo hivyo vya usafiri vimegawiwa kwa watendaji wa miradi husika pamoja na wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi katika ngazi za Wilaya. Lengo likiwa ni kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa kazi, utoaji taaluma na ukusanyaji wa takwimu.

Kupitia mradi wa *MIVARF* ujenzi wa masoko ya Qatar – Chake Chake na Konde (Pemba) na Kinyasini (Unguja) unaendelea pamoja na ukarabati wa Chumba cha Baridi katika soko la Mombasa (Unguja) na kituo cha mafunzo ya uhifadhi na usarifu wa mazao Pujini (Pemba). Ujenzi huo utagharimu Tsh 4 Bilioni.

Kupitia programu ya *ASDP-L* ukamilishaji wa vituo 36 (18 Unguja na 18 Pemba) vya ng'ombe na mbuzi umefanyika sambamba na kuwapatia wananchi bila ya malipo ng'ombe wa kisasa 368 na mbuzi 760 kwa utaratibu wa kukopa na kulipa ng'ombe/mbuzi;
Kupitia programu ya *ZANRICE/ERPP* wakulima wa mpunga 1,884 wamepatiwa taaluma ya kilimo biashara na kutayarisha muongozo wa kilimo bora cha Mpunga inayotumia maji kidogo, mbegu kidogo na mazao mengi (Shadidi)

Serikali imeanzisha Wakala wa Matrekta ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa Huduma za Matrekta na zana za kilimo, pamoja na kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ili kuendeleza utafiti.Kuanzisha programu ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar ambayo itazishirikisha sekta za kilimo, ikiwemo sekta ya biashara na uwezeshaji na utekelezaji wake utahusisha fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, Kampuni mbili za uwekezaji wa sekta ya kilimo, Netafin (Israel - Umwagiliaji maji), Echelon SA (Sychelles - Uzalishaji wa sukari itokanayo na Stavia). Zimepata kibali kutoka ZIPA na kuwasilisha mipango yao kuanza mchakato wa uchambuzi yakinifu kwa kushirikiana na Serikali.

Kuanzisha kituo cha utalii Masingini *Zanzibar City Park* kwa kuimarishwa vivutio vikiwemo ujenzi wa mnara wa kuangalia Mji wa Zanzibar. Aidha, idadi ya watalii waliotembelea hifadhi ya Taifa ya Jozani imeongezeka kutoka 13,935 hadi watalii 44,469 kufuatia kupandishwa hadhi msitu wa Jozani na kuwa *Biosphere Reserve* kutoka *UNESCO*

Kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa uchimbaji wa mchanga chini ya usimamizi wa Serikali kumepelekea kuongezeka kwa mapato kutoka 100,000,000 kwa mwezi wa Machi na Aprili jumla ya Tsh. 584 Milioni zimekusanywa

Wizara imeanza ujenzi wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki chenye uwezo wa kuzalisha vifaranga milioni 10, Kaa milioni tano na Majongoo milioni moja kwa mwaka. Aidha, watendaji na wafugaji samaki 35

wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa mazao ya baharini kupitia wataalamu kutoka China

Utekelezaji Wa Programu Za Wizara Ya Kilimo, Maliasili, Mifugo Na Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti.utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Kilimo kupitia Programu zake kuu tano (5) na ndogo kumi na tatu (13) ulikuwa kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Programu ndogo nne; Programu ndogo ya maendeleo ya umwagiliaji maji, programu ya utafiti na mafunzo ya kilimo, programu ya maendeleo ya huduma za kilimo na Mhe. Mwenyekiti Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo inayojumuisha programu ndogo ya uhakika wa chakula na lishe ambazo zinatekelezwa kwa pamoja na Idara za Umwagiliaji Maji, Kilimo, Uhakika wa Chakula na Lishe, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Programu ndogo ya maendeleo umwagiliaji maji

Mhe. Mwenyekiti Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji na inajukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini. Idara inatoa taaluma za uzalishaji na kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

a) Jumla ya visima na pampu saba (7) vimefanyiwa ukarabati (Kibokwa kisima kimoja, Bumbwisudi visima vitatu, Mtwango kimoja na Cheju viwili) sawa na asilimia 116 ya lengo

b) Malipo ya **TZS. 49.00** Millioni kwa uungaji wa laini kubwa ya umeme yamefanywa kituo cha Machigini, uungaji halisi utafanyika baada ya malipo ya fidia ya mazao TZS. 32.00 Millioni. Aidha, matayarisho kwa ajili ya uungwaji umeme wa Kirindunda yanaendelea sawa na asilimia 50 ya lengo

c) Ukarabati wa Ofisi ya Idara Mbweni, ghala la Cheju umwagiliaji maji na jengo la ofisi na ghala la kuhifadhia zana za kilimo Mtwango umefanyika ambapo Tsh.9.4 Milioni zilitumika sawa na asilimia 70 ya lengo

d) Utengenezaji wa ploti za majaribio juu ya uvunaji wa maji ya mvua katika skimu nne (4) ambazo ni Kiongweni, Msaani, Kiboje Mkwajuni na Muyuni haukufanyika. Hata hivyo ununuzi wa vifaa kwa kazi hii umefanyika ambapo Tsh.2.1 Milioni zilitumika na kazi itaanza mara tu baada ya wakulima kuvuna mazao yao.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS. 883.66 Millioni kwa kazi za kawaida TZS. 603.66 Millioni Mishahara na TZS. 280.00 Millioni kwa matumizi mengineyo). programu pia iliombewa TZS. 185.00 Millioni kwa kazi za maendeleo kutoka SMZ. Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepatiwa TZS. 669.69 Millioni Mishahara TZS. 577.39 Millioni na matumizi ya kawaida TZS. 81.80 Millioni sawa na asilimia 75 na TZS. 10.50 Millioni kwa kazi za maendeleo kutoka SMZ.

Programu ndogo ya utafiti na mafunzo ya kilimo

Mhe. Mwenyekiti Programu hii inatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani, lengo ni kuimarisha na kuendeleza Tafiti za Kilimo na Maliasili pamoja na kuimarisha uwezo wa Chuo cha Kilimo Kizimbani na kuongeza wataalamu katika fani ya Kilimo na Mifugo.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti Kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a) Kujenga mfumo wa maji katika bloki 6 na maabara 1 na miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika eneo la eka 1 na kuweka matangi ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita 23,000 katika kituo cha utafiti Matangatuani.

b) Ujenzi wa matangi 2 ya maji katika kituo cha Kizimbani yenye ujazo wa lita 22,000 kila moja umefanyika, kujenga uzio katika eneo la hekta 1.7 kuzunguka maabara ya mpunga Kizimbani, kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika eneo la eka 1 na kuweka miundombinu ya umeme eneo la utafiti wa mboga mboga Kizimbani. Utekelezaji wa shabaha hii ni juu ya asilimia 100 kutokana na kupata bakaa ya fedha za maendeleo kutoka bajeti ya mwaka 2015/2016

c) Matokeo ya utafiti kupitia vishamba darasa 20 juu ya mbinu bora za uzalishaji wa zao la mpunga kwa wakulima 1,000 (500 Unguja na 500 Pemba) yametolewa. Aidha, matokeo juu ya uzalishaji wa viazi lishe kupitia vishamba darasa 34 (16 Pemba na 18 Unguja) yametolewa kupitia skuli za msingi na vijijini. Vipindi 3 vya TV, taarifa 2 za mawio na taarifa 1 katika Gazeti la Nipashe zote juu ya viazi lishe zilitolewa kwa wananchi. Shabaha

hii imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 600 kutokana na mchango wa miradi ya *NAFAKA* unaofadhiliwa na *USAID*;

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Taasisi ya Utafiti iliombewa jumla ya TZS.1.27 Billioni kwa kazi za kawaida TZS.1.14 Billioni mishahara na TZS.127.83 Millioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 taasisi imepata TZS.1.07 Billioni TZS.1.01 Billioni mishahara na TZS.57.11 Millioni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 84 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti kwa upande wa Chuo cha Kilimo Kizimbani programu ina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, malasili na mifugo katika ngazi tofauti.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti. Kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi 172 ngazi ya Diploma 83 na ngazi ya Cheti 89 na wanafunzi wapya 73 Diploma 40 na Cheti 33 wamedahiliwa

b. Mpango wa matumizi mbadala ya shamba la *RAZABA* umetekelezwa kwa kuandaa utaratibu wa kuingia makubaliano na Shirika la Nyumba la Taifa. Hatua hiyo imefikiwa baada ya kupata miongozo kutoka Serikalini ambapo Wizara imetayarisha *MOU* kwa lengo la kufanya kazi na Shirika la Nyumba la Taifa

c. Wakulima 170 (100 Bumbwisudi, 20 Muyuni na 50 Makombeni wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji bora wa mpunga kupitia mradi wa *TANRICE* na kufanyiwa tathmini. Wakulima hao wameweza kupata mavuno ya wastani wa tani sita (6) katika hekta moja. Mradi pia umetoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagliaji maji na kutegemea mvua kwa wakulima 316 na mabwana/bibi shamba 8 katika skimu za Makombeni, Micheweni, Dobi na Tibirinzi – Pemba na Bumbwisudi, Muyuni na Cheju. – Unguja.

Mhe. Mwenyekiti Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 551.50 Millioni Ruzuku kwa kazi za kawaida TZS. 446.90 Millioni Mishahara na TZS. 104.60 Millioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 Chuo kimepata TZS. 492.79 Millioni Ruzuku kwa kazi za kawaida TZS. 396.19 Millioni Mishahara na TZS. 96.60 Millioni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 89 ya makadirio.

Programu ndogo ya maendeleo ya huduma za Kilimo

Mhe. Mwenyekiti Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Kilimo na Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe imepewa majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalam pamoja na kuratibu upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe katika kaya.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, program kupitia Idara ya Kilimo imetekeleza yafuatayo:

a) Matrekta 20 (14 Unguja na 6 Pemba) yalitumika katika mabonde ya mpunga kwa kuchimbua na kulima, ekari 15,010.25 (Unguja 11,915.5 na Pemba 3,094.75) sawa na asilimia 79 ya lengo la ekari 19,000. Hata hivyo, ili kukidhi mahitaji yaliyopo matrekta 80 yanahitajika kwa kufanikisha kilimo hicho.

b) Ekari 28,848.25 zilichimbuliwa na kupandwa mpunga kati ya eka 33,800 ya lengo la kilimo cha mpunga 2016/17

c) Uhamasishaji na usambazaji wa mitego 2,000 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda umefanyika na mitego 8,003 imebadilishiwa dawa na kusambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba

d) Mpango Mkakati wa Idara ya Kilimo unafanyiwa marekebisho baada ya kuundwa kwa vitengo vipya vya Uendelezaji mazao ya Kilimo na Wakala

wa Huduma za Matrekta na Zana Nyengine za Kilimo. Mpango huu utakamilika mwezi wa Juni 2017

e) Wakulima 311 (156 Unguja na 155 Pemba) walipatiwa mafunzo juu ya kilimo bora cha mboga na udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao wakiwemo nzi wa matunda. Aidha, wakulima 762 (445 Unguja na 317 Pemba) walipatiwa mafunzo na kushiriki katika kilimo cha mpango maalum wa mpunga

f) Kitengo cha ukaguzi wa mazao kimekagua tani 2,208 za karafuu, tani 6,664.4 za mazao ya chakula kutoka Tanzania Bara na tani 19,927.6 za mazao ya chakula kutoka nje ya nchi zimekaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS.3.38 Billioni TZS. 1.80 Billioni Mishahara na TZS. 1.58 Billioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS.3.72 Billioni TZS. 1.63 Billioni mishahara na TZS. 2.08 Billioni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 110 ya makadirio. Ongezeko la fedha hizo zimetokana na fedha walizolipwa wazabuni madeni ya mbolea na mbegu baada ya kufanya uhaulishaji.

Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe

Mhe. Mwenyekiti kwa upande wa Uhakika wa Chakula na Lishe programu imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a) Mafunzo juu ya usimamizi na uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula yametolewa kwa watendaji sita wa Kitengo cha Hifadhi ya Chakula. Taratibu za ununuzi wa vifaa vya Hifadhi ya Chakula zimeanza na zinasimamiwa na Shirika la FAO. Utekelezaji huu ni sawa na asilimi 40 ya lengo

b) Kamati 98 zimepatiwa mafunzo ya lishe bora Unguja 42, Pemba 56. Wanajamii 210 (70 Unguja, 140 Pemba) kutoka Wilaya ya Kaskazini A,

Micheweni na Chakechake wamepatiwa kuku 1,440 kwa ajili ya kuimarisha lishe. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 100 ya lengo

c) Wanajamii 1,642 (547 Unguja na 1,095 Pemba) wamepatiwa mafunzo na wamewezeshwa kuanzisha bustani za mboga kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kupitia progaramu ya Mwanzo Bora inayofadhiliwa na USAID. Pia wanajamii 2,419 (820 Unguja na 1,599 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya lishe katika wilaya za Kaskazini A, Micheweni na Chakechake; na

d) Ufuatiliaji wa Hali ya Chakula umefanyika na ripoti nne za Hali ya Chakula nchini zimetolewa na kusambazwa kwa wadau. Kazi hii imekamilika kwa asilimia 100.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS.344.45 Millioni kwa kazi za kawaida TZS.164.45 Millioni Mishahara na TZS. 180.00 Millioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS.171.50 Millioni TZS.139.50 Millioni mishahara na TZS. 32.00 Millioni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 50 ya makadirio.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Mwenyekiti Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza raslimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai na mazingira yao Idara inaratibu kazi zake kupitia programu ndogo ya uhifadhi wa Rasilimali za Misitu na Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu

Mhe. Mwenyekiti kwa upande wa Maendeleo ya uhifadhi wa Rasilimali programu imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti utekelezaji wa programu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo

a) Notisi zimetolewa za tangazo la kupandishwa hadhi Hifadhi ya Jambiani-Muyuni, Kiwengwa Pongwe, Malilini, Ufufuma - Pongwe na Hifadhi ya Masingini kuwa (Hifadhi ya Maumbile). Hii ni sawa na asilimia 100 ya lengo lililowekwa

b) Matokeo ya moto yalioathiri hekta 35.2 za misitu ya hifadhi Unguja na kusababisha hasara inayokadiriwa kufikia Shilingi 21.1 Milioni

c) Kunguru 2,588 na Kima weusi 551 waliangamizwa Unguja kwa lengo la kudhibiti uharibifu unaosababishwa na wanyama hao

d) Miche 960,984 imeoteshwa vitalu vya Serikali ikiwemo misitu 757,715 (Unguja 722,240 na Pemba 35,475) na Miche ya matunda na viungo 203,269 (Unguja 186,921 na Pemba 16,348)

e) Miche 2,758,816 imeoteshwa vitalu vya watu binafsi miche ya misitu 2,405,430 (Unguja 2,129,414 na Pemba 276,016) na miche ya matunda na viungo 353,386 (Unguja 208,287 na Pemba 145,099)

f) Hekta 125 zimepandwa miti mashamba ya Serikali mwaka 2016 (Dunga - Jendele hekta 21 Unguja Ukuu hekta 14, Chaani 42, Hifadhi ya Masingini hekta 16, Bungi hekta 6, Kibele hekta 18 na Maziwa ng'ombe hekta 8)

g) Hekta 226 zimepandwa miti ya aina tofauti katika maeneo ya jamii, kilomita 55 hifadhi za barabara na hekta 48 zilipandwa mikoko (Unguja 16 na Pemba 24) sawa asilimia 90.8 ya lengo la upandaji miti lililowekwa

h) Mikataba mipya 12 ya makubaliano ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya Jamii imekamilika na inasubiri kuwekwa sahihi. Aidha, kukamilika kwa mikataba hiyo itafikia idadi ya 57;

i) Mikutano 11 ya kushajiisha jamii imefanyika na washiriki 129 wa Shehia 11 za Unguja wameshajiika na kuanzisha vikundi 11 vya uzalishaji wa majiko sanifu

j) Mizinga 250 (125 Unguja na 125 Pemba) imegaiwa kwa wafugaji ikiwa na lengo la kuongeza na kukuza kipato cha wananchi

k) Mafunzo ya ufugaji nyuki kwa walimu wa walimu yamefanyika ambapo wafugaji 50 (25 Unguja na 25 Pemba) walishiriki

l) Mita za ujazo 2,081 za miti aina ya Pines zimevunwa katika shamba la Serikali la Masingini, sawa na asilimia 83.24 ya lengo la uvunaji miti katika mashamba ya Serikali

m) Doria 48 (29 Unguja na 19 Pemba) katika hifadhi, mashamba ya misitu ya Serikali na maeneo ya usafirishaji wa maliasili za misitu zilifanyika ambapo watu 80 walikamatwa. Pia, Misumeno 35 ya moto ilikamatwa 22 iliteketezwa kwa moto 7 ilihifadhiwa na 6 ilikabidhiwa vituo vya misitu kwa ajili ya uokozi.

Mhe. Mwenyekiti.kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliombewa kupata TZS. 96.71 Millioni hadi kufikia Aprili, 2017 imepatiwa TZS.37.44 Millioni kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 39 ya makadirio.

Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka

Mhe. Mwenyekiti kwa upande wa uhifadhi na usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka programu imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

a) Maeneo matatu yenye ukubwa wa hekta 14.7 yameruhusiwa kuchimbwa mchanga Donge Chechele (Hii ilikuwa kabla ya Serikali haijachukua maamuzi ya kusimamia yenyewe rasilmali zisizorejesheka ikiwemo mchanga)

b) Utafiti wa hali halisi ya uchimbaji wa mchanga umekamilika na umeonesha wastani wa tani 39,000 za mchanga na tani 4,320 za kifusi huzalishwa kwa mwezi

c) Hekta 36 kati ya 40 zilizopangwa kurejeshewa maeneo yaliochimbwa mchanga, zimepandwa miti ya matunda, Minazi na Misitu; na

d) Doria 36 zilifanyika maeneo ya uchimbaji na usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka ambapo matukio 32 yameripotiwa yakiwemo mchanga gari 16, kifusi gari 4, udongo gari 2, matofali ya jasi gari 2 na mawe gari 8. katika doria hizo mapato ya Tsh. 56.7 Milioni yalipatikana.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 1.57 Billioni (TZS. 1.42 Billioni mishahara na TZS.149.29 Millioni kwa kazi za kawaida). Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS. 1.34 Billioni (TZS. 1.299 Billioni mishahara na TZS. 47.91 Millioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 85 ya makadirio.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Mwenyekiti Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ya Maendeleo ya Mifugo iliidhinishiwa jumla ya TZS. 1.76 Billioni kati ya fedha hizo TZS. 1.57 Billioni (TZS. 1.32 Billioni mishahara na TZS. 253.50 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo), TZS. 256.75 Millioni kwa kazi za maendeleo. Aidha, programu iliidhinishiwa TZS. 186.75 Millioni kwa kuendeleza Mradi wa wafugaji wa ng'ombe maziwa fedha za SMZ.

Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

i. Programu ndogo ya uzalishaji mifugo
ii. Programu ndogo ya utabibu wa mifugo

Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo

Mhe. Mwenyekiti Programu Ndogo ya uzalishaji wa Mifugo imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa Shabaha za programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo kwa mwaka 2016/2017

a) Wafugaji 14,606 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi, kuku na mifugo mengineyo sawa na asilimia 73
b) Uhamasishaji wa uanzishaji na uimarishaji wa vikundi sita (3 Unguja na 3 Pemba) vya wafugaji umefanyika
c) Kufundisha mabwana/mabibi mifugo wa vijijini 47 (21 Pemba na 26 Unguja)

Mhe. Mwenyekiti Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ya Maendeleo ya Mifugo iliidhinishiwa jumla ya TZS. 1.76 Billioni kati ya fedha hizo TZS. 1.57 Billioni (TZS. 1.32 Billioni mishahara na TZS. 253.50 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo), TZS. 256.75 Millioni kwa kazi za maendeleo. Aidha, programu iliidhinishiwa TZS. 186.75 Millioni kwa kuendeleza Mradi wa wafugaji wa ng'ombe maziwa fedha za SMZ.

Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

iii. Programu ndogo ya uzalishaji mifugo
iv. Programu ndogo ya utabibu wa mifugo

Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo

Mhe. Mwenyekiti Programu Ndogo ya uzalishaji wa Mifugo imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa Shabaha za programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo kwa mwaka 2016/2017

d) Wafugaji 14,606 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi, kuku na mifugo mengineyo sawa na asilimia 73
e) Uhamasishaji wa uanzishaji na uimarishaji wa vikundi sita (3 Unguja na 3 Pemba) vya wafugaji umefanyika
f) Kufundisha mabwana/mabibi mifugo wa vijijini 47 (21 Pemba na 26 Unguja)

g) Huduma za upandishaji wa ng`ombe kwa sindano zimetolewa ambapo ng'ombe 1,443 wamepandishwa ikiwa ni asilimia 36 ya lengo. Aidha, uzalishaji wa gesi ya kuhifadhi mbegu umefanyika ambapo jumla ya lita 2,304 za gesi zilizalishwa na kusambazwa katika vituo vya upandishaji Wilayani

h) Mitambo miwili wa Biogesi imejengwa Unguja (Ndijani) na Pemba (Kendwa Kiwani) kwa azma ya kuongeza matumizi mazuri ya samadi kama nishati mbadala; na

i) Kituo cha majani cha Kizimbani kimefanya ununuzi wa mbegu tofauti za majani na mikundekunde, pia uburugaji na utifuaji wa eneo la eka 3 umekamilika. Aidha, miundombinu ya maji kituoni imeimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo iliidhinishiwa TZS. 1.45 Billioni (TZS. 1.32 Billioni mishahara na TZS. 126.28 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo). Aidha, programu iliombewa TZS. 186.75 Millioni kwa kazi za maendeleo fedha za SMZ. Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS.1.05 Billioni (TZS. 1.02 Billioni mishahara na TZS. 24.04 Millioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 72 ya makadirio.

Programu ndogo ya huduma za utabibu wa mifugo

Mhe. Mwenyekiti Programu ndogo ya pili ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inalenga kuimarisha utabibu wa mifugo, kutoa huduma ya kuimarisha uchunguzi juu ya ubora wa maziwa yanayozalishwa na wafugaji; kuimarisha huduma ya ugani kwa jamii; kudhibiti maradhi yanayoambukizwa na kupe; kudhibiti magonjwa ya kuku na jamii ya ndege; kudhibiti maradhi ya minyoo; kuimarisha huduma za maradhi; na kudhibiti kichaa cha mbwa.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ndogo hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

Utekelezaji wa Shabaha za programu ndogo ya huduma za utabibu wa mifugo kwa mwaka 2016/2017

a) Wanyama 115,130 wamepatiwa chanjo dhidi ya magojwa (Kuku 90,886 walikingwa dhidi ya ugonjwa wa mahepe, kuku 5,226 ugonjwa wa Ndui, kuku 16,576 ugonjwa wa Gumboro, Ng'ombe 100 ugonjwa wa ngozi, Ng'ombe 2,342 walikingwa ugonjwa wa kimeta na chambavu)

b) Sampuli 1,124 za maradhi zilichunguzwa kwa lengo la kuimarisha ubora wa afya za wanyama

c) Wanyama 11,489 walikogeshwa kwa kuwakinga magonjwa ya kupe na wadudu wengine. Kati ya hao ng'ombe 6,237, mbuzi na kondoo 2,175, mbwa 953, paka 181 na kuku wa kienyeji ni 1,943

d) Wanyama 105,263 walitibiwa magonjwa tofauti. Kati ya hao ng'ombe ni 20,742, mbuzi na kondoo 7,149, mbwa 3,804, paka 1,514 na kuku ni 71,935 na sungura 119; Mbwa 5,225 na paka 200 walichanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa.

Mhe. Mwenyekiti Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 iliombewa TZS. 127.22 Millioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS.56.42 Millioni sawa na asilimia 44 ya makadirio.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Mwenyekiti Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi iliombewa TZS. 19.42 Billioni. TZS.881.41 Millioni kwa kazi za kawaida (mishahara TZS. 611.41 Millioni na matumizi mengineyo TZS.270.00 Millioni) na TZS.18.54 Billioni kwa kazi za maendeleo na TZS. 218.22 Millioni ni kutoka SMZ na TZS.18.32 Billioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Pragramu hii imegawika katika program ndogo mbili:

i. Programu ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini.
ii. Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na hifadhi za Baharini.

Programu ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini

Mhe. Mwenyekiti Programu ndogo ya Mazao ya Baharini imetekeleza yafuatayo

Utekelezaji wa Shabaha za programu ndogo ya kuimarisha ufugaji wa mazao ya Baharini

a. Mapipa 26 ya fibre tayari yameshawasilishwa katika eneo la mradi kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki, kaa na majongoo

b. Vikundi 72 vya wafugaji samaki na wakulima wa mwani walipatiwa mafunzo juu ya ukulima na ufugaji bora wa mazao ya baharini. Kamati 48 za mwani zilipatiwa vifaa vya kulimia mwani zikiwemo kamba roll 1,222 na tai tai 2,250

c. Jumla ya vikundi 114 vya wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani wamepatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa mazao ya baharini

d. Ujenzi wa kisima kimoja cha maji chumvi umekamilika

e. Wastani wa tani za mwani 5,089.34 zenye thamani ya Tsh. 10,935,850,159 zimekaguliwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi

f. Jumla ya washiriki 75 Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo bora ya usarifu wa madagaa, mafunzo hayo yalihusu usafi wa dagaa mara baada ya kuvuliwa ili kuongeza thamani, ubora, kutunza afya ya mlaji na kukidhi vigezo vya soko.

g. Kuongezeka kwa idadi ya tani za madagaa zilizosafirishwa nje ya nchi hadi kufikia 990.47 zenye thamani ya Tsh. 22,157,130 mwaka 2016

h. Mkandarasi wa ujenzi wa uzio *fence* na ukarabati wa majengo makongwe katika eneo la mradi tayari ameshasaini mkataba wa ujenzi. “Transformer” ya umeme tayari imeshafungwa katika eneo la mradi.

Aidha, programu ilisimamia utekelezaji wa Mradi mmoja wa Kuimarisha ufugaji wa mazao ya Baharini (Angalia Kiambatisho nam. 6)

Mhe. Mwenyekiti Programu ndogo ya kuimarisha ufugaji wa Mazao ya Baharini kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, iliombewa TZS.4.26 Billioni kati ya fedha hizo TZS.694.01 Millioni kwa kazi za kawaida (TZS.611.41 Millioni kwa mishahara na TZS.82.60 Millioni matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo TZS. 69.00 Millioni ziliombwa kutoka SMZ na TZS. 3.49 Billioni kutoka "*KOICA*" kutekeleza mradi mmoja wa Kuimarisha Ufugaji wa Samaki**.** Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata TZS.540.02 Millioni ambapo TZS.499.19 Millioni mishahara na TZS. 40.82 Millioni matumizi mengine.

Programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa bahari inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu.Mhe.

Mwenyekitikwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa bahari imetekeleza yafuatayo Jumla ya doria 174 zilifanyika, kati ya hizo, doria 50 ni za kuangalia leseni za vyombo vya uvuvi na doria 124 za ukaguzi wa tiketi za wageni ziliendelea kufanyika kisiwani Mnemba, Kizimkazi na Fumba.

Taaluma ya uhifadhi ilitolewa kwa kufanya mikutano ya tisa kwa kamati za uvuvi maeneo ya hifadhi nchini

Taaluma ya athari za uvuvi haramu ilitolewa kwa wavuvi ili kupunguza wimbi la matumizi mabaya ya nyavu ambayo hupelekea kuwepo kwa migogoro katika maeneo ya ukanda wa pwani. Kesi mbili za migogoro ya wavuvi kati ya

Chwaka na Uroa na Chwaka na Marumbi wanaogombania maeneo ya uvuvi ziliripotiwa na juhudi za kutafuta suluhu kwa migogoro hiyo zilichukuliwa

Utafiti wa kujua kiwango cha samaki katika maji ya ndani unaendelea kufanywa kwa awamu, ikiwa pamoja na kujua aina za samaki tulionao kupitia mradi wa SWIOFish. Aidha, maeneo mapya ya hifadhi ya Tumbatu (*TUMCA*) na Changu Bawe (*CHABAMCA*) yameanzishwa na mipaka ya hifadhi kongwe za *MIMCA* na *MENAI* imefanyiwa marekebisho

a). Mafunzo ya ufugaji wa kaa na majongoo yalitolewa kwa washiriki 34 (wanawake 13 na wanaume 21), mafunzo hayo yalihusu njia bora za ufugaji, ujenzi wa uzio kwa ajili ya kufugia majongoo na vizimba vya kufugia kaa; na programu ilisimamia utekelezaji wa Mradi mmoja wa SWIOfish (**Angalia kiambatisho nam. 7**).

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu iliombewa jumla ya TZS. 187.40 Millioni kutoka Serikalini, hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2017, Programu imepatiwa jumla ya TZS. 44.97 Millioni sawa na asilimia 24. Kwa kazi za maendeleo programu iliombewa TZS. 14.97 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo *JICA* na Benki ya Dunia. Hadi kufikia Aprili 2017, Programu imepatiwa TZS.1.15 Billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS. 21.18 Millioni kutoka SMZ**.**

PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA KILIMO NA MALIASILI

Mhe. Mwenyekiti programu hii inayojumuisha programu ndogo tatu ambazo zinasimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Ofisi kuu Pemba.

Programu ndogo ya mipango na usimamizi wa kazi za Kilimo na Maliasili

Mhe. Mwenyekiti madhumuni ya Programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti. Idara ya Mipago, Sera na Utafiti pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 Programu imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2016/2017

a) Mapitio ya Rasimu ya Será ya kilimo (2002) ya Zanzibar yamefanyika pamoja na kupata maoni ya wadau kwa Unguja na Pemba

b) Semina/warsha 5 (3 Unguja na 2 Pemba) kwa wadau juu ya maendeleo/changamoto za sekta ya kilimo nchini zilifanyika

c) Mpango Mkakati wa Wizara (2017-2020) umeandaliwa na umewasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba, hivi sasa unasubiri kupata maoni ya Kamati ya Uongozi ya Wizara

d) Mapitio ya Sheria ya Uhifadhi na Utibabu wa Mimea yamefanyika kwa mashirikiano na ofisi ya Mwanasheria Mkuu

e) Kutoa mafunzo ya usarifu wa mazao na ujasiriamali kwa wananchi 140 (Unguja 70 na Pemba 70) kwa lengo la kuongeza thamani na tija katika bidhaa za kilimo

f) Kazi ya kuainisha maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi yaliyoathiriwa kutokana na mabadiliko ya Tabianchi ilifanyika kwa Unguja na Pemba. Aidha, baada ya kuainisha maeneo hayo utayarishaiji wa vipeperushi 1,000 vinavyoonesha athari hizo umefanyika

g) Kuendeleza ukusanyaji wa takwimu za kilimo, ukamilishaji wa takwimu za kilimo pamoja na utekelezaji wa mradi wa takwimu *SAE* kupitia FAO,

h) Utafiti wa kujua uwezo wa uzalishaji wa mazao ya machungwa, embe na nazi umefanyika kwa lengo la kuyaingiza mazao hayo katika mfumo unaotumika katika kuchangia pato la Taifa *GDP*

i)

j) Wizara imetayarisha mfumo wa pamoja wa kitaasisi katika Sekta ya Kilimo *ZASDP* na kuuwasilisha kwa Washirika wa Maendeleo *DP's-AWG*.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka 2016/2017 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa programu tatu na mradi mmoja kama ifuatavyo: Programu ya *MIVARF* **(Angalia kiambatisho nam. 8);** Programu ya *ASDP-L,* **(Angalia kiambatisho nam.9);** Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga –ERPP **(Angalia kiambatisho nam. 10),** Mradi wa *ZANRICE* **(Angalia kiambatisho nam. 11** na Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo **(Angalia kiambatisho nam. 13).**

Mhe. Mwenyekiti mwaka wa fedha 2016/2017 Programu ndogo hii iliombewa TZS. 14.80 Billioni. TZS. 473.52 Millioni kwa kazi za kawaida (TZS. 298.02 Millioni mishahara na TZS. 175.50 Millioni matumizi mengineyo). Kwa fedha za maendeleo programu imepangiwa TZS. 14.32 Billioni (TZS. 478.04 Millioni kutoka SMZ na TZS. 13.85 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata jumla ya TZS. 5.17 Billioni (TZS.240.23 Millioni mishahara na TZS. 149.75 Millioni kwa kazi za kawaida). Aidha, kwa fedha za maendeleo programu imepata TZS. 379.76 Millioni kutoka SMZ na TZS. 4.39 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Programu ndogo ya utawala

Mhe. Mwenyekiti madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, programu inaratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

Shabaha za programu kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti.Kwa mwaka wa 2016/2017 Programu kupitia Idara ya Utumishi na Uendeshaji imetekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa shabaha mwaka 2016/2017

a) Wafanyakazi 40 wameendelea kulipiwa masomo kwa viwango tofauti.
b) Vijana 15 wameendelea kusomeshwa kupitia program ya udaktari wa mifugo.
c) Jumla ya magari 63, Trekta 54 na pikipiki 217 zimehakikiwa na mashamba/nyumba (madiko) 34 yamepatiwa hatimiliki.
d) Wafanyakazi 153 wamepatiwa maslahi yao.
e) Manunuzi ya Wizara yameratibiwa kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2005;
f) Kukusanya mapato yanayotokana na vyanzo vya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti programu ndogo ya utawala na mafunzo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, iliombewa jumla ya TZS. 1.75 Billioni kwa kazi za kawaida (TZS.1.12 Billioni mishahara na TZS. 643.57 Millioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepatiwa TZS. 1.59 Billioni (TZS.1.10 Billioni mishahara na TZS. 491,77 Millioni kwa kazi za kawaida).

Programu ndogo ya uratibu wa kazi za Wizara Pemba

1. Mhe. Mwenyekiti. Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, ilitekelezwa na Ofisi Kuu Pemba. Kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Programu iliombewa kutumia jumla ya **TZS. 2.96 Billioni** (**TZS. 2.48 Billioni** mishahara na **TZS.3.61 Millioni** ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia Aprili, 2017 programu imepata **TZS.2.72 Billioni** (**TZS.2.36 Billioni** mishahara na **TZS. 358.99 Millioni** matumizi mengineyo).

CHANGAMOTO

2. Mhe. Mwenyekiti. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a) Kuchelewa kwa upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbegu ya mpunga, dawa na mbolea ;

b) Baadhi ya wakulima kuendelea kutumia mbegu zao za asili badala ya mbegu bora walizopewa na Serikali;
c) Mabadiliko ya hali ya hewa yamesababisha mvua zisizotabirika na vipindi virefu vya jua;
d) Uvamizi wa Viwavi jeshi na Kunguni mgunda
e) Uelewa mdogo wa kukubaliana na hali halisi ya upatikanaji wa mchanga;
f) Matumizi mabaya ya misumeno ya moto; na
g) Uvuvi haramu unaoendelezwa na wavuvi vijana.

HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

a) Wizara imekagua maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi na imechapisha vipeperushi 1,000 sambasamba na kutoa mafunzo

b) Wizara inaendelea kuwasiliana na Wazabuni kwa lengo la kuharakisha uletaji wa pembejeo kwa wakati. Kwa msimu wa 2017/18, Wizara itazalisha mbegu za mpunga kutoka kwa wakulima wa Zanzibar

c) Wizara imenunua lita 230 za dawa ili kupambana na Viwavi jeshi kwa zao la mpunga

d) Kamati ya kitaifa imeundwa ili kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa mchanga nchini

e) Wizara kwa kushirikiana na vikosi vya SMZ na jeshi la Polisi inaendelea kuhamasisha kuzuia matumizi ya misumeno ya moto Unguja na Pemba.

Muelekeo wa Mapato na Matumizi ya Bajeti Inayozingatia Programu Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Makadirio ya Mapato 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara inakadiria kukusanya mapato ya jumla ya TZS. 4.93 Billioni kutoka vianzio vyake vya Unguja na Pemba. (Angalia kiambatanisho nam. 13).

Mhe. Mwenyekiti Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu tano ambazo ni:

Programu ya Maendeleo ya Kilimo

Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka

i. Programu ya Maendeleo ya Mifugo;
ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi; na
iii. Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti kwa kutekeleza programu hizo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya TZS. 70.61 Billioni. Matumizi ya kawaida TZS. 23.70 Billioni ambapo TZS. 17.63 Billioni Mishahara, TZS. 4.49 Billioni matumizi mengineyo na TZS. 1.58 Billioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta (Angalia kiambatisho nam. 14). Kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara inatarajia kutumia jumla ya TZS. 46.90 Billioni ambapo TZS. 2,75 Billioni ni kutoka SMZ na TZS. 44.15 Billioni ni kutoka kwa washirika wa maendeleo (Angalia kiambatisho nam. 15).

MUELEKEO WA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI MWAKA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuendeleza kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imejiwekea malengo yafuatayo:

a). Kuimarisha kilimo kwa kutumia teknolojia ya kisasa
b). Kuendeleza utoaji wa huduma za matrekta na zana zake na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na vipuri kwa ajili ya huduma za kilimo
c). Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi. ikiwemo vanilla na pilipili hoho

d). Kuendeleza huduma za uoteshaji na upandaji wa miti

e). Kushajiisha kilimo kinachostahamili mabadiliko ya tabianchi kwa mazao yote
f). Kuimarisha huduma za utafiti, kinga, tiba na uzalishaji wa mifugo

Kutayarisha kanuni itakayowezesha kisheria kuingiza na kutoa bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi nje ya nchi;

g). Kuimarisha utoaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano kwa wafugaji 4,000 Unguja na Pemba;
h). Kuwaendeleza wavuvi vijana kuvua katika Bahari Kuu;
i). Kufanya tafiti ili kutambua maeneo ya uvuvi yenye idadi kubwa ya samaki;
j). Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza sekta ya kilimo;
k). Kuanzisha kituo cha kuwaweka na kuwakuza vifaranga vya samaki, kaa na majongoo kabla ya kusambazwa kwa wafugaji kwa upande wa Pemba.

Programu ya maendeleo ya kilimo

Mhe. Mwenyekiti pragramu hii imegawika katika programu ndogo nne ambazo ni:

l). Programu ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji.
m). Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo.
n). Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Karakana ya Matrekta.
o). Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Mhe. Mwenyekiti.kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Programu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya TZS. 35.85 Billioni. Matumizi ya kawaida TZS. 10.11Bilioni (TZS.6.36 Billioni mshahara na TZS.2.678 Billioni kazi za kawaida. na TZS. 1.08 Billioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani na Wakala wa Matrekta. Kwa kazi za maendeleo program inaombewa TZS. 25.74 Billioni ambapo (TZS. 740.00 Millioni kutoka SMZ na TZS. 25.00 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo *KOICA*.

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya maendeleo ya umwagiliaji maji kwa mwaka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

p). Kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 200 (150 Unguja na 50 Pemba) pamoja na hekta 520 kupitia mradi wa *EXIM BANK* Korea

q). Kukarabati miundombinu ya umwagiliaji maji katika skimu 6 (Bumbwisudi, Kibokwa, Cheju na Uzini kwa Unguja na Makombeni na Mangwena – Pemba)

r). Kutoa taaluma kwa njia ya mafunzo ya vitendo na nadharia juu ya kilimo bora cha umwagiliaji maji kwa maafisa na mabwanashamba 50 (30 Unguja na 20 Pemba). Aidha, Idara ya Umwagiliaji maji imepanga kutoa mafunzo juu ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa njia ya matone *micro irrigation* kwa wakulima 500 (350 kwa Unguja, 150 kwa Pemba

s). Kuendelea na Upimaji na ujenzi wa mabonde tisa (Kibondemzungu, Mtwango, Koani, Mchangani na Bandamaji – Unguja na Machigini, Kwa *DOBI*, Ole na Kwalempona – Pemba) Aidha, mabonde maalumu kati ya hayo yametengwa kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu

t). Kujenga ploti za majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua katika Mabonde manne (hekta 20), Kiboje Mkwajuni na Muyuni - Unguja na Msaani na Kiongweni - Pemba.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS. 27.15 Billioni ambapo TZS. 1.41 Billioni (TZS. 1.06 Billioni Mishahara na TZS. 350.00 Millioni kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu inatarajia kupata TZS. 25.74 Billioni ambapo (TZS. 740.00 Millioni kutoka SMZ na TZS. 25.00 Billioni kutoka kwa washirika wa maendeleo *KOICA*.

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa mwaka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu Ndogo hii ina sehemu mbili ambazo ni Utafiti na ile ya Mafunzo ya Kilimo. Programu Ndogo hii inalenga kutekeleza yafuatayo:

Shabaha zitakazotolewa Taasisi ya utafiti kwa mwaka 2017/2018

u). Kuzindua na kufanya vikao 4 vya Baraza la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar;

v). Kufanya tafiti 12 (9 Unguja na 3 Pemba) katika sekta ndogo za mazao, maliasili na uvuvi; kutoa mbegu 4 mpya za mazao muhimu ya chakula (mpunga, muhogo, viazi lishe na mtama) kwa wakulima; kutoa ripoti 9 kwa njia ya machapisho na kuzisambaza kwa wadau;

w). Kujenga jengo la utawala na maabara za utafiti Kituo cha Utafiti Kizimbani, kukarabati majengo mawili (1Kizimbani na 1Matangatuani), kuweka uzio eneo lenye ukubwa wa hekta tano (3Kizimbani na 2 Matangatuani), kujenga mahodhi ya kuhifadhi maji uwezo wa lita 100,000 (80,000 Kizimbani na 20,000 Matangatuani), kukarabati barabara za ndani urefu wa kilomita 4 Kituo cha utafiti Kizimbani;

x). Kuongeza watafiti 4 katika ngazi ya uzamili (MSc) watakaoongoza programu za utafiti na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watafiti 10;

y). Kuzipatia maabara za utafiti wa mazao, udongo na tissue culture seti 4 za vifaa vya maabara;

z). Kufanya mapitio ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na kutengeneza Mpango Mkakati mpya; na

aa). Kutengeneza scheme of service ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti.kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Taasisi ya Utafiti inaombewa jumla ya TZS. 2.16 Billioni kwa kazi za kawaida (TZS. 1.96 Billioni mishahara na TZS. 200,00 Millioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha zitakazotolewa na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa mwaka 2017/2018

a) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 200 ngazi ya Stashahada na kuchukua wanafunzi wapya 214;

b) Kutekeleza mpango wa matumizi ya shamba la RAZABA; na

c) Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji kwa wakulima 150 katika skimu za Cheju 90, Dobi 30, Tibirinzi 30.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu inaombewa TZS. 782.70 Millioni (Ruzuku) kwa kazi za kawaida (TZS. 672.80 Millioni Mishahara na TZS. 109.90 Millioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Matrekta na maendeleo ya huduma za kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo inalenga kutekeleza yafuatayo:

a) Kutayarisha vitini vya aina tano kwa ajili ya kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji mazao ikiwemo matumizi ya mbegu bora, urutubishaji wa ardhi, usarifu wa mazao na masoko;

b) Kununua na kusambaza tani 70 za mbegu ya mpunga (35 Unguja na 35 Pemba), na kuzalisha tani 5 za mahindi, tani 2 za mtama tani 2 za kunde na tani 2 chooko katika Kituo cha Uzalishaji Mbegu Bambi

c) Kununua na kusambaza tani 722 za mbolea (TSP tani 285 na *UREA* tani 437) na lita 1,000 za dawa ya kuulia magugu

d) Kutoa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS. 5.00 Billioni (TZS. 3.10 Billioni Mishahara na TZS. 1.90 Billioni kwa matumizi mengineyo.

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya huduma za Matrekta na zana za kilimo 2017/2018

a) Kusimamia na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya zana za kisasa za kilimo zitakazopelekea kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo;
b) Kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima, sekta binafsi na Taasisi nyengine;
c) Kuendeleza utoaji wa huduma za matengenezo makubwa na ya kawaida kwa matrekta na zana zake na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi na vipuri kwa ajili ya huduma;
d) Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kuchimba na kuburuga ekari 21,000 (13,000 Unguja na 8,000 Pemba);
e) Kutoa mafunzo kwa madereva 20 (14 Unguja na 6 Pemba) na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wasimamizi wa huduma za matrekta mashambani;
f) Uimarishaji wa mazingira bora ya utendaji kwa wafanyakazi wa kawaida, madereva na mafundi wa matrekta na zana za kilimo;
g) Kuimarisha miundombinu na majengo ya Wakala Unguja na Pemba; na
h) Kuimarisha huduma za kiofisi na utendaji, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi na malengo ya Wakala.

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS. 300.00 Millioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa mwaka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuendeleza mafunzo ya lishe kwa wanajamii 19,000 (6500 Unguja na 12,500 Pemba) waliopo katika Shehia 94 za Wilaya ya za Kaskazini A, Micheweni na Chake Chake;

b) Kukamilisha na kuratibu kazi za hifadhi ya chakula;

c) Kufuatilia hali ya chakula na kutoa ripoti nne za Hali ya Chakula na Lishe nchini.

d) Kuandaa ripoti za hali halisi ya upatikanaji wa chakula kwa Wilaya zote za Zanzibar na kuziwasilisha kwa wadau; na

e) Kuanzisha Mfumo wa Ufuatiliaji wa Masoko na Bei za Vyakula (Agricultural Market Information System).

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS. 455.61 Millioni kwa kazi za kawaida (TZS. 236.81 Millioni Mishahara na TZS. 218.80 Millioni kwa matumizi mengineyo).

Programu ya Maendeleo ya Raslimali Za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka

Mhe. Mwenyekiti programu ya Maendeleo ya Rasilimali za misitu na maliasili zisizorejesheka imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:

i. Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu;
ii. Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti programu hizi zinaombewa jumla ya TZS. 2.77 Billioni (TZS. 2.45 Billioni mishahara na TZS. 323.08 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu ndogo ya Maendeleo ya misitu kwa mwaka 2017/2018:

Shabaha zitakazotolewa na programu ndogo ya maendeleo ya uhifadhi wa rasilimali za misitu kwa mwaka 20172018

Mhe. Mwenyekitikwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kukamilisha taratibu za kisheria za upandishaji hadhi *Final order* wa Hifadhi ya Ufufuma – Pongwe yenye ukubwa wa Hekta 1,988, na Malilini yenye ukubwa wa hekta 566

b) Kudhibiti matukio na kupunguza majanga yanayotokana na moto katika hifadhi 4 ambazo ni Hifadhi ya Taifa ya Jozani, Kiwengwa –Pongwe, Jambiani- Muyuni na Ufufuma- Pongwe

c) Kupanda miti hekta 120 katika mashamba ya Serikali(Unguja) sambamba na kuhamasisha upandaji wa miti hekta 300 katika maeneo ya watu binafsi

d) Kuhamasisha na kuendeleza upandaji wa mikoko hekta 40

e) Kuyatambua na kuyasajili Mazizi (5) ya wanyama pori yakijumuisha, Wamiliki, aina na idadi ya wanyama wanaofugwa)

f) Kufanya doria 64 katika misitu ya hifadhi na Jamii kwa lengo kudhibiti matukio ya uhalifu / Uharibifu;
g) Kuendeleza vivutio na huduma za Utalii wa kimazingira katika hifadhi mbili (Masingini na Ngezi)

h) Kujitangaza kwa njia za mitandao, warsha na maonesho ya ndani na nje ya Zanzibar ili kufikia Watalii 45,000

i) Kuotesha miche 2,500,000 (1,000,000 Mikarafuu, 1,000,000 Misitu,100,000 Minazi na 400,000 ya matunda na Viungo) katika vitalu vya Serikali

j) Kuvuna miti mita za Ujazo 2,500 mashamba ya Serikali, sambamba na kudhibiti ukataji holela wa miti kwa kutoa vibali 240 na kusimamia matumizi ya msumeno wa moto

k) Kuhamasisha ufugaji wa nyuki na kuanzisha database ya

l) Kuhamasisha na kuelimisha teknolojia ya matumizi ya majiko sanifu kwa Taasisi 2 na kaya 400 za Unguja na Pemba

m) Kusimamia maeneo mapya 12 kwa kukamilisha taratibu za usimamizi wa rasilimali za Misitu *CofMA.*

Mhe. Mwenyekiti **p**rogramu hii inaombewa jumla ya TZS. 2.58 Billioni. TZS.2.45 Billioni mishahara na TZS. Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii:

a) Kwanza ina majukumu kuyakagua na kuyapima maeneo yenye vigezo na sifa za kuchimbwa maliasili zisizorejesheka;
b) Kufanya tafiti moja inayohusu urejeshaji na matumizi mengine ya maeneo ya uchimbaji mchanga, mawe, kifusi na kokoto;
c) Kufanya semina mbili (1 Unguja na 1 Pemba) na warsha juu ya upungufu wa mchanga;
d) Kurejeshea kwa kupanda miti hekta 40 katika maeneo ya uchimbaji kwa kutumia mbinu za kilimo hai;
e) Kutumia mazao na vipando vilivyopo katika eneo litakalochimbwa mchanga;
f) Kufanya doria 36 katika maeneo ya uchimbaji, Usafirishaji, uingizaji na uuzaji wa maliasili zisizorejesheka; na
g) Kukamilisha Sera na Sheria ya Maliasili Zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inaombewa jumla ya TZS.191.16 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ya Maendeleo ya Mifugo inaombewa jumla ya TZS. 2.61 Billioni kati ya fedha hizo (TZS. 1.86 Billioni mishahara na TZS. 250.00 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS. 500.00 Millioni ikiwa ni ruzuku kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo) ambayo imeanzishwa hivi karibuni.

Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

i. Programu ndogo ya uzalishaji mifugo
ii. Programu ndogo ya utabibu wa mifugo

Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo inalenga kwa kufanya mambo yafuatayo:

a) Kuwapatia ushauri wafugaji 22,000;
b) Kupandisha ng'ombe kwa sindano 4,000 (2,000 Unguja na 2,000 Pemba);
c) Kujenga mitambo 4 ya biogas (2 Unguja na 2 Pemba);
a) Kuchanja kuku 550,000 dhidi ya ugonjwa wa mahepe (300,000 Unguja na 250,000 Pemba);
d) Kuchanja mbwa 11,000 dhidi ya kichaa cha mbwa (8,000 Unguja na 3,000 Pemba);
e) Kuimarisha maabara ya mifugo - Maruhubi;
f) Kuimarisha vituo vitatu vya karantini (Kisakasaka na Donge Muwanda - Unguja na Nzi wengi Gando - Pemba); na
g) Kuimarisha huduma za kinga na tiba.

Programu ndogo hizi zinaombewa jumla ya TZS. 2.11 Billioni kati ya fedha hizo (TZS. 1.86 Billioni mishahara na TZS. 250.00 Millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

Programu ndogo ya Utafiti wa Mifugo

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

(a) Kuimarisha miundombinu ya Taasisi ya Utafiti;
(b) Kuimarisha mahusiano ya Taasisi za ndani, Kikanda, Kitaifa na Kimataifa na wadau wa sekta ya Mifugo;
(c) Kuwapatia mafunzo kwa watafiti 12 (9 Unguja na 3 Pemba);
(d) Kufanya tafiti saba za Mifugo (5 Unguja na 2 Pemba);
(e) Kuchapisha na kuhifadhi taarifa na matokeo saba ya utafiti;
(f) Utayarishaji wa Sheria ya Uanzishwaji Taasisi ya Utafiti wa Mifugo; na
(g) Kusimamia kazi za ukaguzi na manunuzi ya Taasisi.

Programu hii ndogo ya Utafiti Mhe. Mwenyekiti, itatekelezwa Kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha inaombewa jumla ya TZS. 500.00 Millioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi inaombewa TZS. 13.69 Billioni kati ya hizo TZS.1.16 Billioni zinaombwa kwa kazi za kawaida (mishahara TZS. 848.71 Millioni na matumizi mengineyo TZS. 315.60 Millioni). TZS.12.53 Billioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS. 490.00

Millioni ni kutoka SMZ na TZS.12.04 Billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Programu hii imegawika katika program ndogo mbili:

i. Programu ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini;
ii. Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari.

Programu ndogo ya ufugaji wa mazao ya baharini

Programu ndogo ya mazao ya baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini. Programu imetarajiwa kutekeleza yafuatayo:

a) Kutoa taaluma ya mbinu bora za ufugaji na usarifu wa mazao ya baharini pamoja na ukulima wa mwani kwa vikundi 60;
b) Kuanzisha kituo kimoja cha kuzalisha vifaranga vya samaki, na mazao mengine ya baharini Beit-el-Ras Unguja;
c) Kusaidia vifaa vya ufugaji bora wa mazao ya baharini kwa vikundi saba;
d) Kusaidia vifaa vya ukulima wa mwani kwa Kamati 45.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Programu ndogo ya ufugaji wa mazao ya baharini inaombewa TZS. 2.86 Billioni kati ya hizo TZS.157.19 Millioni zinaombwa kwa kazi za kawaida. TZS.2.70 Billioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS. 200.00 Millioni ni kutoka SMZ na TZS.2.50 Billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa baharini

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa baharini inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017, Programu hii ndogo ina malengo kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi (5 Unguja na 5 Pemba) na kuimarisha taaluma zao;
b) Kuimarisha doria za baharini shirikishi na kamati za za uvuvi katika maeneo ya hifadhi ya MENAI na MIMCA kwa Unguja na PECCA kwa Pemba;
c) Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira katika hifadhi zote tatu;
d) Kuwaendeleza wavuvi vijana 10 Unguja na 10 Pemba kuvua katika kina kirefu cha maji;
e) Kusimamia utekelezaji wa mradi wa *SwioFish* ujenzi wa soko kuu la samaki linalojengwa katika diko la Malindi ambao unategemea utaanza mwezi wa Agosti;
f) Kufanya tafiti ili kutambua maeneo ya uvuvi yenye samaki wengi *"Potential fishing grounds"* pamoja na kuweka matumbawe ya kienyeji kwa upande wa Unguja ili kuongeza uzalishaji wa samaki;
g) Kukusanya taarifa za uvuvi wa bahari kuu kwa kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika uvuvi huo; na
h) Kulenga kwenda katika uvuvi wa kiviwanda *''Semi Industrial'* kwa lengo la kuwapatia ajira vijana, tija zaidi na kuinua kipato cha wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini inaombewa TZS. 10.84 Billioni kati ya hizo TZS.1.16 Billioni zinaombwa kwa kazi za kawaida (mishahara TZS. 848.71 Millioni na matumizi mengineyo TZS. 158.40 Millioni). TZS.9.83 Billioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS. 290.00 Millioni ni kutoka SMZ na TZS.9.54 Billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi madhumuni yake mkubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi wa sekta za kilimo. Kwa mwaka wa fedha Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaombewa jumla ya TZS. 15.67 Billioni kati ya fedha hizo TZS. 7.04 Billioni (TZS. 6.11 Billioni mishahara na TZS. 931.22 Millioni kwa matumizi mengineyo) na TZS. 8.63 Billioni kwa kazi za maendeleo (TZS. 1.52 Billioni kutoka SMZ na TZS.7.11 Billioni kutoka washirika wa maendeleo. Programu hii imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:

i. Programu ya Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvi;
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti;
iii. Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Shabaha za programu ndogo ya utawala ya mafunzo ya mwaka 2017/2018

a) Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;
b) Kuendelea kuhakiki mali za Serikali zilizo chini ya Wizara na kuzipatia hatimiliki;
c) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaalum wafanyakazi 67 wanaoendelea na masomo na 30 wapya ifikapo Juni 2017;
d) Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Wizara TZS. 4.93 Billioni;
e) Kuratibu na kusimamia manunuzi wa Wizara kwa mujibu wa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2005;

Programu ndogo ya utawala na uendeshaji itatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Kwa mwaka wa fedha, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS. 2.36 Billioni kwa kazi za kawaida (TZS. 1.70 Billioni mishahara na TZS. 660.00 Millioni kwa matumizi mengineyo).

Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili;
b) Kusimamia na kuendeleza kituo cha usarifu wa mazao kwa ununuzi wa vifaa Kizimbani;
c) Kufanya tafiti tatu za kiuchumi na kijamii kuhusu uzalishaji wa mboga, mayai na alizeti;
d) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera na Programu WETLAND, ASDP-L na MIVARF na ZANRICE za kupunguza umaskini katika kilimo na kuongeza kipato cha wakulima;
e) Kufanya ziara za Ufutiliaji na tathmini za kazi za Wizara;
f) Kuzitangaza Sera za Sekta ya Kilimo na Mpango Mkakati kwa njia ya warsha 4 (2 Unguja na 2 Pemba);
g) Kukamilisha mapitio ya Sera ya (kilimo, Uvuvi na Misitu. Sheria ya mbegu, Sheria ya Pembejeo na Misitu);
h) Kushiriki katika mikutano sita (6) ya mashirikiano na Wizara za Sekta ya Kilimo T.Bara, kikanda, kimataifa na Kitaifa;
i) Kufanya mikutano minane (8) ya Kamati ya Utafiti;
j) Kuendeleza matayarisho ya programu mpya ya maendeleo ya kilimo kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo;
k) Kuwajengea uwezo wafanyakazi na wadau wa mbegu juu ya masuala ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea;
l) Kufanya utafiti mmoja kuhusu mabadiliko ya tabia nchi;
m) Kuendelea kusimamia Programu na Miradi inayotekelezwa na Wizara;
n) Kufanya utafiti wa udongo katika maeneo yatakayojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji; na
o) Kutoa nakala 2000 za jarida la kilimo, mifugo na uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha Programu inaombewa jumla ya TZS. 9.82 Billioni. TZS. 547.20 Millioni kwa kazi za kawaida ambapo (TZS. 338,06 Millioni mishahara na TZS. 209.13 Millioni matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo programu inatarajia kupata TZS.8.63 Billioni

kwa miradi ya maendeleo TZS. 1.52 Billioni kutoka SMZ na TZS. 7.11 Billioni kutoka washirika wa maendeleo.

Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba

Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu na maendeleo sekta ya kilimo, maliaisli, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili, Uvuvi na Mifugo.

Programu ndogo hii ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, itatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba. Kwa mwaka wa fedha inaombewa jumla ya TZS. 4.14 Billioni (TZS. 4.07 Billioni mishahara na TZS.62.09 Millioni ni matumizi mengineyo).

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutekeleza programu za Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya TZS. 70.61 Billioni (Angalia kiambatisho nam 14d). Matumizi ya kawaida TZS. 23.70 Billioni ambapo (TZS. 17.63 Billioni Mishahara, TZS. 4,49 Billioni matumizi mengineyo na TZS. 1.58 Billioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta). Kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara inatarajia kutumia jumla ya TZS. 46.90 Billioni ambapo (TZS. 2.75 Billioni ni kutoka SMZ na TZS. 44.15 Billioni ni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya uwasilishaji naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara

katika juhudi za kuendeleza kilimo, Mifugo na Uvuvi, zikiwemo nchi za Japan, Finland, Norway, Ireland, China, India, Israel, Mauritius, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta ya Kilimo nchini. Vilevile nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IFAD, UNDP, FAO, JICA, UNICEF, WFP, USAID, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, *Rockfeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation, GIZ*, "WAP", "WHO", Shirika la Mionzi la Ulimwengu (IAEA), Indian Ocean Rim, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC) na Umoja wa nchi za Ulaya - "EU" Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Pia tunazishukuru taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, Mifugo na Uvuvi zikiwemo ZSTC, TAHA, UWAMWIMA, ZAIDI, COSTECH, Milele Foundation, Kilimo Trust, CARE, Wizara ya Kilimo, Chakula Ushirika T/Bara, CARI, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ushirikiano ya Afrika Mashariki, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Sayansi ya Baharini, *"State Oceanic Administration"* (SOA) ya China, *Heifer Project Tanzania, Zanchick*, "ZAASO", "ZSPCA" na "WIOMSA"

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wanakamati za hifadhi ya Maliasili zetu wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, Mifugo na mazao ya Baharini, pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Pia Napenda kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake na Wataalamu wote wa Wizara yangu Kilimo na Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Afisa Mdhamini Pemba pamoja na Wakurugenzi na Watengaji wote na Taasisi zote zana Wizara hii; naomba tuendelee kushirikiana katika kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula .

Mhe. Mwenyekiti, Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa

mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu, Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa uzowefu wangu wa mwaka mmoja niliokaa katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ile ahadi niliyoitoa katika Baraza lako Tukufu nimebakia miaka miwili na siku kumi na saba. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wakiweza hata kuipitisha leo Bajeti ili siku mbili zilizobakia nikafanye kazi ya uharibifu mkubwa, wa mpunga Cheju na pahala pengine ili tuendelee na kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo kwa hotuba yako, Waheshimiwa wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuelekeza salamu zangu za pongezi kwa Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi na maarifa yake ya kumshauri ipasavyo Mheshimiwa Rais wetu hadi tukaweza kuyaona mafanikio yaliyofikiwa. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uwezo huo na amjaalie maisha marefu yenye kheri na yeye. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, salamu zangu za pongezi pia zimwendee Mwenyekiti wangu wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wake wote kwa kukubali kuniteua mimi kuwasilisha hotuba hii kwa niaba yao kwenu nyinyi Waheshimiwa Wajumbe. Hii inadhihirisha wazi kwamba Kamati yangu inajali na kudumisha usawa wa kijinsia na kutekeleza kivitendo kauli inayosema ‘Wanawake wanaweza bila kuwezeshwa’. Hivyo nimefarijika sana kuwa mbele yenu kutekeleza Wajibu huo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa nampongeza Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa kuteuliwa kwake na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi kuja kuungana nasi katika kuwatumikia wananchi wetu ndani ya chombo hiki muhimu. Kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kumueleza kwamba sisi Wawakilishi wenzio tunamkukaribisha sana na tunamuahidi kumpatia ushirikiano wa hali ya juu na tupo tayari kupokea mawazo na ushauri wake kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa napenda kuwapa pole wananchi wetu wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kutokana na maafa ya mvua za msimu huu wa Masika zilizoathiri mali, makaazi ya wananchi wetu pamoja na kusababisha baadhi ya watu kupoteza maisha. Kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo nasi hatuna budi kuwaomba wananchi hao wawe na moyo wa subra na uvumilivu hasa katika kipindi hiki kigumu. Aidha, naiomba serikali kuendelea kuchukua juhudi za kuwajali na kuwathamini Wananchi hao kwa kuwapatia misaada ya hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, kwa kutambua mchango na ushauri mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati hii, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe
5. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
6. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe.

Aidha, Kamati yetu pia inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue makatibu hao ni:

1. Ndugu Ramadhan Khamis Masoud - Katibu
2. Ndugu Said Khamis Ramadhan - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara husika na mwaka husika. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati yangu ilipitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tarehe 06/05/2017 baada ya kuelekezwa kufanyiwa marekebisho kutokana na utofauti wa jumla ya Makadirio ya matumizi iliyoainishwa katika Kitabu cha Mswaada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya mwaka 2017/2018 na ile *'Ceiling'* waliyopewa Wizara kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba niwasilishe mbele ya Baraza Lako Tukufu maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Kilimo imeundwa na Programu ndogo nne zinazojumuisha:

- Programu ndogo ya Umwagiliaji Maji,
- Programu ndogo ya utafiti na mafunzo ya Kilimo,
- Programu ndogo ya maendeleo ya huduma za Kilimo na
- Prgramu ndogo ya uhakika wa chakula na lishe.

Programu zote hizi kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Umwagiliaji Maji, Kilimo, Uhakika wa chakula na Lishe, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani. Aidha, jukumu kuu la Programu hizi ni kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini, kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kuimarisha na kuendeleza tafiti za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi pamoja na kuratibu upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kupitia utekelezaji wa Programu hii inapenda kuchukua fursa hii tena kuwapongeza viongozi na watendaji wa Wizara ya

Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuzifanyia matengenezo pampu saba (7) ili kuhakikisha huduma ya umwagiliaji maji katika mashamaba ya Kibokwa, Bumbwisudi, Mtwango na Cheju inapatikana kama kawaida na kuwawezesha wakulima wanaolima katika mashamba hayo wanazalisha mpunga mwingi kwa maslahi yao na taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kupitia Programu Kuu hii inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuwasaidia wakulima wa shamba la Mtwango ama kwa kuwaongezea fedha walizonazo au kuwatafutia njia mbadala itakayowawezesha kununua trekta kwa matumizi ya kulimia maeneo yao ili waweze kuongeza kipato chao. Aidha, Wizara hii ihakikishe inashirikiana na Wizara ya Fedha na Mpango kulifuatilia ipasavyo suala la matrekta ya Mahindra kwa lengo la kupunguza upungufu wa matrekta unaowakabili wakulima wa Zanzibar. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika Kamati inatambua na kuthamini juhudi zinazochukuliwa na Wizara hiiza kununua na kusambaza Tani 350 za mbegu ya Mpunga kwa Wakulima wa Unguja na Pemba, Tani 700 za mbolea (100 TSP na 600 *UREA*) ambapo Unguja wamesambaza Tani 350 na Pemba Tani 350 na Lita 15,000 za dawa ya kuulia magugu ambapo Unguja wamesambaza lita 9,000 na Pemba lita 6,000. Pamoja na mafanikio hayo, Kamati yangu inaitaka Wizara hii izalishe mbegu za kutosha na zenye ubora na kuzisambaza kwa walengwa ili kuepuka malalamiko ya wakulima kwamba mbegu nyingi zinazoagizwa huwa hazina ubora na yasije kujitokeza kama yalivyokuwa katika ununuzi wa dawa ya *Hansunil*.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kamati inaipongeza Wizara hii kwa kukamilisha na kusambaza ripoti za Hali ya chakula na Lishe katika ngazi ya Taifa na Wilaya. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuzisambaza ripoti hizo kwa wadau mbali mbali wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe Bazara la Wawakilishi ili umma uelewe muelekeo mzima wa upatikanaji na ukosekanaji wa chakula katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza tena Wizara hii kwa juhudi za kumtafuta Mshauri Elekezi wa kuandaa michoro na kulipima Shamba la Kilimo la ZARABA liliopo Makurunge - Bagamoyo ambalo kwa kipindi kirefu limetelekezwa bila ya kuendelezwa. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha Mshauri Elekezi huyo anapatikana haraka iwezekanavyo na kazi hiyo inafanyika kwa mafanikio ili hatua za kuliendeleza shamba hilo ziweze kufanyika. Aidha, Kamati pia imeitaka Wizara ya Kilimo ikae na Wizara ya

Fedha na Mipango ili watafute namna bora zaidi ya kuyaendeleza mashamba ya mpira yaliopo Unguja na Pemba.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu hii imeundwa na Programu ndogo mbili zinazojumuisha Programu ndogo ya Uhifadhi wa Misitu na Programu ndogo ya Maendeleo ya Misitu ambapo Programu zote hizo kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Aidha, Programu Kuu hii ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza raslimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai na mazingira yao pamoja na kusimamia na kudhibiti maeneo ya uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara kwa upande wa Unguja za kuanzisha utaratibu mpya na mzuri wa kulipia malipo ya Mchanga kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Kupitia utaratibu huo, Wizara imeweza kukusanya jumla ya Tzs. 380 milioni kwa mwezi mmoja tu wa Machi, 2017 kiasi ambacho hakikuwahi kukusanywa katika miaka iliyopita. Hivyo, Kamati inawataka viongozi na watendaji wa Wizara hii kuanzisha utaratibu huo katika Kisiwa cha Pemba. Halikadhalika, Kamati imeitaka Wizara kuutumia utaratibu huu katika raslimali nyengine za mawe, kifusi na kokoto ili mianya ya uvujaji wa mapato ipungue kama si kuondoka kabisa na Serikali kujiongezea mapato. Aidha, Kamati pia inaiomba Serikali iwe inazifuatilia bei elekezi za Mchanga inazozitoa ili ziwe zinafuatwa kikamilifu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imeitaka Wizara kuongeza juhudi za upandaji miti katika maeneo yaliyochimbwa mchanga ili kujaribu kupunguza athari zaidi za uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu ya Unguja na Pemba. Sambamba na hilo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza Wizara kwa kuendelea kufanya doria 36 katika maeneo ya uchimbaji na usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka na kufanikiwa kukamata gari 30 na misumeno ya moto 35 ambayo ilikuwa ikitumika vibaya kuharibu maliasili zetu. Kutokana na athari ya misumeno ya moto, Wizara inapaswa kuongeza juhudi na kuweka mikakati maalum kuhakikisha wanapambana ipasavyo na uhalifu huo hata ikiwezekana watumie Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.(*Makofi*).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu hii imeundwa na Programu ndogo mbili zinazojumuisha Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo na Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ambapo Programu zote hizo kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Aidha, Programu Kuu hii ina jukumu kubwa la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu kuu hii, Wizara imefanikiwa kuwapatia wakulima jumla ya ngo`ombe wa maziwa 188 na mbuzi wa maziwa 443 Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza idadi ya ng`ombe na uzalishaji wa maziwa. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuendelea na zoezi hilo la ugawaji na usambazaji wa ngo`ombe lakini pia washughulikie ubora wa maziwa yanayozalishwa na Wafugaji wetu kwani inasemekana ubora wa maziwa yetu hayapo katika kiwango kizuri. Kutolishughulikia vizuri suala hili tunaweza kuwakosesha wafugaji wetu soko la maziwa pamoja na kuikosesha Serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kamati inaieleza Wizara kwamba kwa sasa kuna soko la kutosha la maziwa yanayozalishwa Zanzibar lakini inahitajika juhudi za makusudi kuchukuliwa kuhakikisha maziwa ya kutosha na yenye ubora yanazalishwa, hasa kwa kuwaruhusu wawekezaji Wazalendo wanapatia maeneo ya kuwekeza kwa kufuga ng`ombe na mbuzi wa kutosha kuweza kukidhi haja ya mahitaji ya mazao hayo. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali kuhamasisha wawekezaji waje kuwekeza katika eneo hilo.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu hii imeundwa na Programu ndogo mbili zinazojumuisha Programu ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Bahari ambapo Programu zote hizo kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Uvuvi. Aidha, Programu Kuu hii ina jukumu kubwa la kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuhakikisha kunakuwepo kampuni itakayoshughulikia uvunaji wa Samaki Zanzibar (*ZAFICO*). Mbali na pongezi hizo, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha Kampuni hiyo inaandaa '*management team'* nzuri na iliyomakini

itakayotambua thamani za fedha zilizowekezwa kwamba ni fedha za wakwezi na wakulima wa Zanzibar ambazo zinahitaji kutumika kwa maslahi yao. Aidha, kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha inaisimamia ipasavyo Kampuni hiyo ili iweze kufanya marejesho ya fedha ambazo inazitumia.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeendelea kuipongeza Wizara kwa kuweza kuwapatia mafunzo vikundi 72 vya wafugaji wa samaki na wakulima wa mwani kuhusu ukulima na ufugaji bora wa mazao ya baharini. Aidha, Kamati 48 za mwani wamezipatia vifaa vya kulimia mwani. Mbali na mafanikio hayo, Kamati inaitaka Wizara kulishughulikia suala la kuharibika kwa mwani kutokana na kushambuliwa na maradhi yasiyoeleweka, kwani wakulima wa mwani wameanza kukata tamaa na kilimo cha aina hiyo na iwapo hakuna juhudi itakayochukuliwa basi zao hilo linaweza kutoweka na kubakia historia tu kwamba lilikuwa likilimwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mafunzo kwa wajasiriamali wa dagaa, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutoa uelewa kwa wajasiriamali hao ili waweze kufanya kazi zao kwa utaalamu utakaowapatia tija zaidi na kuiingizia mapato Serikali.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu hii imeundwa na Programu ndogo tatu zinazojumuisha Programu ndogo ya Utawala na Uratibu wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Aidha, Programu Kuu hii ina jukumu kubwa la kusimamia na kuratibu masuala ya Sera, Sheria, Mikakati pamoja na Mipango ya Maendeleo na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu Kuu hii Wizara imeweza kuzihakiki jumla ya gari 66, pikipiki 212 pamoja na kuyapatia hatimiliki mashamba 34. Vile vile, wafanyakazi 153 wamepatiwa maslahi yao. Kupitia mafanikio hayo, Kamati inaitaka Wizara ihakikishe tatizo la maslahi ya wafanyakazi hasa waliopo Pemba linatatuliwa ili malalamiko ya wafanyakazi yaweze kumalizika. Sambamba na hilo, Kamati pia inaitaka Wizara hii kuhakikisha inapeleka Mwanasheria Kisiwa cha Pemba kwa lengo la kuondosha ukosefu na uzoroteshaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara - Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imegundua kuna tatizo kubwa la ajira linaloikabili Wizara kwani imefikia Bwana au Bibi shamba mmoja kuzifanyia kazi Shehia tano. Hali hii inapunguza ufanisi wa Mabwana na Mabibi shamba hao na kuwaondoshea hamu ya kufanyakazi zao ipasavyo ya kuwasaidia wakulima kulima kilimo cha utaalamu na cha kisasa kinachowawezesha kutumia nguvu kidogo na kupata mazao mengi. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kwa kushauriana na Wizara inayoshughulikia Utumishi wa Umma kukamilisha mchakato wa ajira ili kuwapunguzia mzigo kama si kuwaondolea kabisa ugumu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mhe. Hamad Rashid Mohamed, Naibu Waziri Mhe. Lulu Msham Abdalla; Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao pamoja na mashirikiano yao ya dhati waliotupatia wakati wote wa kupitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*).

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muiunge mkono bajeti hii ili tuiwezeshe Wizara kwenda kutekeleza na kufanikisha yale waliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 na baadaye nasi tupate fursa ya kuja kumuhoji kwa kile alichoingiziwa na matokeo halisi ya kile kilichotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo naiunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamida Abdalla Issa Mwakilishi Nafasi Maalum Wanawake kwa hotuba yako.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa kwanza kwa siku ya leo ni Mhe. Hidaya Ali Makame, Viti Maalum Vijana kutoka Kaskazini, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman (Shihata) na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya Mhe. Hidaya kuna taarifa ya kuhusu wageni wetu wa leo ni wageni wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvu. Wageni hawa ni wafadhili wa Wizara hiyo, wageni wenyewe ni kama hawa wafuatao:

1.	Mr. Isack Lymo	-	TAHA
2.	Ndg. Kassim Biwi	-	TAHA
3.	Ndg. Khadija Sharif	-	*MILELE FOUNDATION*
4.	Mr. Abdillahi Yahya Caisser	-	ZAIDI
5.	DR. Flower Msuya	-	*Institute of Marine Science University of Dar-es-Salaam*

Wageni wengine ni wa Mhe. Waziri Hamad Rashid (Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi). Hawa ni Viongozi wa Chama cha (*ADC*). Wageni hao ni kama wafuatao:

1.	Ndg. Khamis Mohamed Kombo	-	Naibu Katibu Mkuu (ADC)
2.	Ndg. Mustafa Halfani Issa	-	Mkurugenzi Stard Guard (ADC)
3.	Ndg. Juma Ali Khamis	-	Sera, Utafiti, na Uenezi (ADC)
4.	Ndg. Mtumwa Faiz Sadik	-	Fedha na Uchumi (ADC)
5.	Ndg. Salma Ayoub Amour	-	Kamishna Mjini/Magharib (ADC)
6.	Ndg. Haji Hamdani Mzee	-	Kamishna Kaskazini Unguja (ADC)
7.	Ndg. Tatu Juma Khatib	-	Kamishna Kusini Unguja (ADC) na
8.	Ndg. Fatma Ramdhan Mussa	-	Mwenyekiti Jumuiya ya Wanawake ADC Taifa na
9.	Mhe. Saadun Serenge	-	Mjumbe wa Jumuiya ya Vijana ADC

Wageni wetu karibuni sana.(*Makofi*).

Waheshimiwa tunaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, leo nikiwa mchangiaji wa mwanzo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kufika katika kwenye Baraza letu Tukufu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza nianze kuipongeza Kamati husika ya Wizara hii ya Kilimo kwa kazi yao nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha wanapita kila bonde, lakini wanapita kila kwenye Shehia ambayo inahusika na masuala haya ya kilimo na uvuvi, kuhakikisha wanaifanyia kazi na wanaipa haki Kamati hii nzuri ambayo inatupa nguvu wakulima na wakwezi katika kuzifanya kazi zetu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza moja moja nianze kuhusu suala la wakulima wadogo wadogo. Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia zaidi hotuba ya Kamati ya Wizara ya Kilimo wamesisitiza kuhusu suala la Mabwana shamba na Mabibi shamba, kwa kweli suala hili mpaka muda huu bado lina uchache na lina changamoto kubwa kwa wakulima wetu. Mhe. Mwenyekiti, kama tukizingatia Mhe. Waziri katika hotuba hii ametuambia kwamba wana lengo la kwamba hawa wakulima wa mpunga waweze kulima mpungu huu wao na waweze kuzalisha mbegu nyingi ili Serikali inunue mbegu hizo kupitia kwa wakulima wetu hawa wa wa mpunga.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hili jambo kwa asilimia kubwa linawezekana katika nchi yetu hii, lakini jambo hili litawezekana pale endapo wakulima hawa watakuwa wana mawasiliano ya karibu na wizara yao, lakini pia watakuwa na msukumo mkubwa au wana moyo kupitia hawa Mabibi shamba na Mabwana shamba endapo kuwa watakuwa na mashirikiano ya hali ya juu katika kukiimarisha kilimo hiki cha mpunga, lakini pia wakishirikiana na Wizara katika kuyaimarisha mabonde yetu na kuvienzi vianzio vya maji ikiwemo mito na visima.

Mhe. Mwenyekiti, Mabwana shamba na Mabibi shamba ndio ngao ya wakulima wa mpunga na wakulima wote wadogo wadogo, kwa sababu wakulima wanakumbana na changamoto nyingi zikiwemo za kuingiliwa na maji kwenye mabonde yao lakini pia kuunguliwa na mipunga au na mazao yao mengine kwa kipindi cha jua kali kutokana na kuwa mabonde yale yanakosa kuwa hayana maji lakini na hiki kipindi cha mvua kuwa mabonde haya hayana zile njia za kupitia maji kutoka nje na kuweza kuyaacha yale mazao yakaweza kunawiri na kustahamili mpaka hatua ya kuvuna ikafikia na ikaweza kuvuna

mazao haya. Mhe. Mwenyekiti, tunaona changamoto kubwa, tukiangaliza zaidi katika kipindi hiki hapa cha masika, ukipita kwenye mabonde yote sasa hivi yamejaa maji, mipunga hii haionekani imefunikwa kabisa. Kwa hivyo kwa vile mipunga hii inakabiliwa na changamoto hiyo ya kujaa maji kwenye mabonde, unamkuta mkulima yule hana hata ile faida ya mbegu wala hata ule mpunga wa kupata angalau kupika uji.

Mhe. Mwenyekiti, je, tujiulize hapa hizi mbegu zitapatikana wapi kwa kupitia changamoto kama hizi. Kwa sababu unamkuta mkulima anajitahidi kufanya kila hali kuweza kukabiliana na hali ngumu ya kimaisha ili tu la alimradi ahakikishe yeye ule mpunga anaokwenda kuumwaga kule bondeni mwisho wa siku anapata angalau vipolo vitatu, kimoja anaweza akaweka mbegu na viwili mwenyewe anaweza kupika uji na wanawe akaweze kwenda mbele na maisha. Lakini unamkuta mkulima huyu anarudi nyuma na kila siku anakuwa katika hali ya unyonge na kusononeka kutokana na hizi changamoto za kujaliwa kwa maji na mabonde lakini pia za kuwa mabonde haya ni makavu, kile kipindi cha jua kali hata ile sehemu ya kwenda ukasema leo ninakwenda nikapalilie, nikaburuge nimwage hii mbegu ya mpunga hauwoti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije ukurasa wa 12 wa hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, ukurusa wa 12 kuendelea wa 13 unasema, Wizara inaendelea kushajihisha wakulima na kuwaunganisha pamoja wafugaji na wavuvi katika masoko ya ndani na nje ya nchi, kwa kufungua duka la bidhaa za kilimo Maruhubi ili kuwaunganisha wakulima hao kwenye masoko. Aidha vikundi 127 vya vijana kutoka Wilaya zote za Zanzibar vimeunganishwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili jambo kama kweli ndiyo limefanyika linatupa moyo sana kwa wakulima wetu, lakini kwa vijana wetu pia. Kwa sababu vijana nao wana hali ngumu ya kimaisha lakini pia wakulima wetu na wavuvi na wafugaji nao wako katika hali ngumu ya kimaisha. Kwa hivyo jambo hili kama kweli litaendelea au litafanyika basi wakulima wetu hawa na wafugaji na wakulima wetu hawa watakuwa katika hali nzuri ambayo inaweza kuwapa moyo wakazifanya kazi zao hizi bila ya kuwa na wasi wasi wa kukutana na changamoto nyengine kama hizo nilizozitaja hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ningemuomba hapa Mhe. Waziri anieleze hawa vijana wa Wilaya zote waliunganishwa kwenye vikundi 127 vikundi hivi vikaweza kuimarishwa na hili duka, hivi vikundi kweli (yaani sijui hata niseme nini) vina mvuto wa aina gani na hivi vikundi vimeimarishwa vipi. Hawa vijana je, ni vijana wa aina gani. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa ukija

naomba unambie katika hivi vikundi 127, kuna wanawake wangapi wanaume wangapi lakini kwa Wilaya zote ungenambia, labda ungetufanyia mchanganuo hapa Wilaya "A" kuna vikundi vingapi, Wilaya ya Kaskazini, Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kati ungetutajia hizi idadi ya hivi vikundi ambavyo vimetajwa hapa tukaweza kujua kweli kila Wilaya kuna vikundi vingapi ambavyo vimekusanywa ili vikafikia idadi ya 127.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nikiendelea kwenye mchango wangu katika kitabu hiki kuna katika ukurasa wa 75 kuna kiambatisho namba 1 hapa tofauti ya uzalishaji wa mazao ya chakula mwaka 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, hapa kweli tofauti tunaiona kubwa na tofauti ambayo inaweze kutuvunja moyo hata sisi wananchi, kwa sababu kuna baadhi ya mazao ambayo yametajwa yakiwemo karafuu, muhogo, mpunga, migomba, viazi vikuu, viazi vidogo, mahindi, mbaazi, choroko na mboga mboga.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika *diagram* hii hichi kipando cha mbaazi na choroko kwa kweli kinasikitisha, kwa sababu kwenye sehemu hii tunaona asilimia yake kiufupi haionekani ya mbaazi na choroko, lakini na ya mboga mboga pia inaonesha kama ni ndogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, kweli zao la choroko na mbaazi ni zao ambalo lilikuwa lina nguvu sana katika nchi yetu hii hususan katika Mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja, lakini na hata kwa Pemba kwenye Mikoa yote kilimo hichi kilikuwa kinapewa nguvu zaidi kwa wananchi wote. Lakini tunakiona kwamba kilimo hiki sasa hivi kimetoweka na sababu zinazosabisha kilimo hiki kiondoke ni ukanda ule hasa kuingiliwa hasa na ujenzi mkubwa wa mahoteli, pia kwa hawa wananchi kutofahamu yale maeneo waliyokuwa waliyokuwa wanalima hivi vilimo kugawiwa na kupewa waatu wengine ambao hata hawahusiki, wakiwemo na wao wenyewe kuuza maeneo haya. Kwa kweli kilimo hiki sasa hivi hakipo ukizingatia kwamba ni kilimo ambacho kilikuwa yaani yule mwananchi mwenyewe hivi vyakula hana hamu navyo, yaani ukifika msimu wa mbaazi wewe basi tena huna amani na tumbo lako, huna amani na mwili wako kwa sababu *any time* mpaka lile jasho linanuka mbaazi.

Lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kilimo hiki sasa hivi kimetoweka na hakipo katika nchi yetu. Ningemuomba sana Mhe. Waziri afanye kila hali maeneo bado yapo ukichia huko kwenye maeneo ya Wilaya ya Kaskazini "A", lakini pia maeneo hayo hayo ya Kaskazini ya Wilaya ya Kaskazini "A", bado kuna maeneo yapo na yanaruhusu kulima kilimo hiki. Ningemuomba sana Mhe. Waziri azidi kujumuisha na haya mabwana shamba na mabibi shamba kuwaweka wananchi hawa ili waweze kukirejesha kilimo hiki cha mbaazi na

choroko, uwele na mtama ili kilimo hichi kizidi nguvu na kiweze kuwa imara zaidi kama hapo mwanzo kilivyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama utaangalia kwenye kumbukmbu wazee wetu ilikuwa asubuhi mtu akishapata bakuli ya uji, basi anaweze akafika jioni saa 12:00 ndio akapa tonge ya ubwabwa au ya ugali. Lakini kwa sasa hivi hiyo bakuli ya uji inayouzwa huko mitaani pia haiko kwenye uwalisia wake, kwa kuwa tu kilimo hiki kimetoweka na kimepotea hata ule wa kununua huko madukani unaukuta unatoka sehemu ambazo hata hazistahiki na hali yake haiko vizuri. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie suala hili kwa umakini zaidi ili kiweze kurudi kilimo hichi na kiweze kurudi kwenye asili yake na wananchi wetu waweze kunufaika na afya zetu ziwe nzuri zaidi kuliko zilivyo hivi sasa kutokana na mavyakula ambayo tunatumia na makemikali yaliyokuwemo ndani ya vyakula hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tufikiri kwamba suala la mtama na mbaazi ni vyakula imara na vyakula vyenye siha na afya zaidi ndani ya miili yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije pia kwenye ukurasa wa 80 tunaona utofauti wa mazao ya baharini yanayosafirishwa mwaka 2015/2016, pia hapo hapo tuangalie kwenye jadweli yetu hili au sehemu hii inaonesha mazao ya baharini yakiwemo mwani, majongoo, makome, kamba, dagaa, chaza, samaki, kaa, matumbo na ngozi za chewa na ambali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye kitabu hiki pametajwa matumbo lakini Mhe. Waziri tungekuomba sana uje utufafanulie haya matumbo ya aina gani. Kwa sababu ukisema matumbo tu hapa tunaweza kusema hata haya yetu pengine yatakuja kukatwa yapelekwe huko yasafirishwe. Lakini si mazao ya baharini ila kama mazao ya baharini kuna matumbo mengi tunayoyajua lakini haya yanayosafirishwa ni yepi, ya tenga, ya chaa, ya samaki sijui ya aina gani papa au changu au yupi. Kwa hivyo tungemuomba sana Mhe. Waziri hapa aje atufafanulie haya matumbo ni ya aina gani.

Lakini pia tuangalie hapo hapo kwenye orodha hii ya hivi vitu ambavyo vinapatikana baharini na vikaweza kusafirishwa, si tunafahamu pia kuna haya mapenzi ya papa, nayo ni kitega uchumi kikubwa, nayo ni maliasili kubwa ambayo wavuvi wetu au wajasirimali wanayakusanya mapenzi haya na kuyasafirisha, nayo yanandana na soko. Kwa nini hapa hayakuorodheshwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia hapo hapo kuna hili suala la majongoo. Mhe. Mwenyekiti, majongoo tunayajua na yako ya aina nyingi. Majongoo haya

kwenye hii sehemu tunaona kwamba kitu ambacho kipo kwenye asilimia kubwa ni haya majongoo ambayo kwa asilimia kubwa kuliko vitu vyote vilivyoorodheshwa hapa.

Lakini hapo hapo tukiangalia hawa wananchi wetu ambao wanaofanya biashara hii ya majongoo yaani kutafuta kwenda kuzamia pwani na kuyatafuta haya majongoo, manufaa yao ni madogo. Kwa sababu bei ya majongoo ambayo inapatikana huko mitaani ni ndogo sana lakini tukiangalia ni kitu ambacho kinasafirishwa kwa asilimia kubwa kuliko vyengine vyote. Hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri aliangalie suala letu hili kwa wananchi hawa au wavuvi wetu hawa wanaojisughusha na shughuli hizi ili na wao waone faida ya haya majongoo, wanapokwenda kuzamia kule baharini na kuyapata majongoo haya kwa sababu tunajua kwamba kazi ya kuzamia baharini si kazi ndogo na ni kazi ambayo unauza roho yako.(*Makofi*).

Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri aliangalie suala hili la majongoo na aweke bei yake kwanza tunaona kwenye hizi bei tunavyohamu haya majongoo yako aina mbali mbali na kila jongoo lina bei yake kwa hapo zamani tulivyokuwa tunauza. Lakini sasa hivi natako wewe utoke uende baharini urudi na polo nzima ya majongoo, basi utakuja na Shs 2000/= au Shs.3500/= polo nzima ile. Mhe. Mwenyekiti, wakati hapo zamani unakwenda pwani ukirudi na majongoo yako unajua kwa sababu haya majongoo haya ninayoyaokota hapa ni majongoo ambayo yako kiwango cha juu kibei unapata pesa yoyote na unaweza hata kununua kilo ya mchele au ya mtama, lakini kwa sasa hivi hali imekuwa tofauti na tunaona wananchi wetu wanajitahidi kuifanya kazi hii. Nimuombe sana Mhe. Waziri aje atuhakikishie bei ya majongoo kwa wavuvi wetu ili na wao waweze kunufaika na waweze kuiona kazi hii ni ya muhimu na ina maana kwao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye suala jengine la kilimo cha matunda. Mhe. Mwenyekiti kilimo cha matunda sasa hivi tunaona matunda yamewekwa kipa umbele zaidi kwa afya za binadamu, lakini pia nitazungumzia baadhi ya matunda likiwemo doriani, danzi na balungi.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita doriani kila mtu alikuwa hana habari nalo, wala hata halijui. Lakini kwa hali inavyokwenda hivi sasa mambo ya *digital* na *internet,* kila mtu kaujua umuhimu wa doriani ukiachilia utamu wake na harufu yake na ladha. Mhe. Mwenyekiti, lakini tumeona kwamba doriani liko katika hali ya juu yaani sasa hivi ya kiuasilia kwa sababu kila mtu ukimtajia doriani hapa kila mtu sasa hivi mdomo unamchechemka mate, kwa sababu ya doriani kila mtu analijua. Doriani sasa hivi likizaliwa tu basi kila

mmoja kishaanza kupanga bei yake na sasa hivi doriani duchu linauzwa kwa bei ya shilingi elfu 5,000 na shilingi elfu 3,000 duchu la mwisho, sikwambii ukija ukilikuta hilo kubwa unaambiwa shilingi elfu 12,000 na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ningekuomba sana juu ya kilimo cha miti hii ya midoriani, kwa kweli midoriani sasa hivi inatoweka kwa sababu iliyopo sasa hivi mingi yao imeshakula karne kama mbili na kuendelea. Kwa hivyo midoriani hii tayari imeshakuwa ule uwezo wake wa kuzalisha ni mdogo. Hivyo tuchukue jitihada Mhe. Waziri wa kuviatika vitalu vingi vya midoriani tuvisambaze kwa wananchi wetu kwa kila ile sehemu ambayo inaruhusika kupandwa miti hii ipandwe, ili soko lake nalo liendelee lizidi kuwa kubwa na faida ienee kwa wananchi lakini na kwa serikakli yetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia pia kwenye hili zao la balungi na danzi. Mhe. Mwenyekiti, haya madanzi na mabalungi nayo ni matunda ambayo yana siha na afya kwa miili yetu lakini hata kwa afya zetu, kwa sababu hata kwa upande wa madaktari pia wanatuasa sana kuhusu kutumia madanzi na mabalungi kutokana na maradhi yaliomo sasa hivi ya *pressure* na sukari. Lakini tunaona kwamba haya matunda hayamo kabisa katika muonekano wa kufanyiwa kazi au kutumiwa kwa sababu mtu hata umtajie danzi anakwambia aah! danzi ndio nini, halijui umuhimu wake. Kwa hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri ukishirikiana na mabwana shamba na mabibi shamba watoe elimu juu ya matunda haya lakini kuna mastafeli pia na machungwa.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mazao ambayo…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hidaya Ali Makame naomba umalizie.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namalizia.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri juu ya matunda na mazao haya ambayo sasa hivi yanaonekana kutaka kutoweka katika nchi yetu hii, na ni mazao ambayo yalikuwa hayahitaji kupandishwa na mtu, hakuna haja ya mtu kutafuta mbalungi au mdanzi kwenda kuotesha, ni mjiti ambao unajiotea wenyewe na kujiimarisha wenyewe, hautaki kumwagiliwa maji wala hautaki kupaliliwa. Lakini sasa hivi ni miti ambayo inatoweka katika nchi yetu. Hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri uwe na umakini juu ya miti hii ya asili na matunda haya ambayo yana siha na afya zaidi kwa miili yetu na kwa afya zetu, yaimarishwe na yatafutiwe miundombinu mipya ya kuhifadhiwa ili yasije yakapotea katika nchi yetu hii na yabakie milele.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia na niunge mkono hotuba hii asilimia mia moja na niwapongeze sana Wizara pamoja na Kamati inayohusika, naiunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makamea. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kumpisha mchangiaji anayefuta kuna mgeni mwengine wa Mhe. Waziri ambaye ni Mshauri wa Mambo ya Kilimo anaitwa Mzee Golo, karibuni sana. (*Makofi*).

Waheshimiwa tuendelee sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali akifuatiwa na Mheshimiwa, nilimtaja Mhe. Rashid lakini kwa makosa, naomba akisha Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf afuatie na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi kwa bajeti yake ya 2017/2018.

Pili nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuhakikisha kwamba tunajua kuwa katika nchi yetu kilimo ni uti wa mgongo na ndio roho ya wanyonge ya wakwezi na wakulima.(*Makofi*).

Tatu niipongeze Kamati kwa taarifa yake nzuri kwa yale waliyoyatoa na kuona kwamba pana maelekezo ambayo yafanikishwe ili tuendelee katika ukuzaji wa kilimo chetu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar asili yetu ni wavuvi na wakulima na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alikuwa analipigania kila siku suala la kilimo na uvuvi, na tukizingatia hilo hata katika nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko mbele yetu na kwenye vitabu hivi, kuna alama mbili kubwa. Alama ya kwanza kuna minazi kwa Unguja na Pemba kuna mikarafuu. Kwa hivyo ukiwa katika anga yoyote kati ya visiwa hivi, unahakikisha tu kwamba kwa Unguja ni sehemu ya minazi na kwa Pemba ni sehemu kubwa ya mikarafuu. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba serikali kwa makusudi inakatisha minazi bila ya kujali. Kwa nini nasema hivyo nitatoa maelezo yangu yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar palikuwa panaingizwa mifuko hapa ya plastiki, serikali ikasema ni marufuku kuingiza mifuko ya plastiki katika nchi yetu. Leo ukionekana na mfuko unaweza kwenda kufungwa jela mwaka mmoja au

ukalipa faini ya shilingi kama milioni tatu au milioni nne ili kuliondoa hili tatizo lisiingie katika nchi yetu. Lakini leo utashuhudia Wizara ipo, watu wa Kilimo wapo, watu wa Maliasili wapo, unakuta watu wanaochonga viwanda mbali mbali rundo la minazi imepasuliwa pale bila ya kujali. Mhe. Mwenyekiti, zamani serikali ilikuwa inatoa kauli kwamba minazi iliyotimia umri ni ruhusa kukata, lakini leo minazi ya miaka mitatu au mitano au kumi inakatwa. Jambo hili natoa indhari kwamba ni hatari sana.

Mhe. Mwenyekiti, leo inaonesha dhahiri kwamba serikali haijaweka mkakati wa makusudi kuzuia minazi yetu isikatwe. Nazi leo Mhe. Mwenyekiti, kutoka shilingi 1000/- mpaka 2000/- inafika. Mnyonge katika mwezi wa Ramadhani hii ni kuchemsha kwenda mbele tu, chakula ikiwa muhogo, ikiwa ndizi hata ndizi mbivu zinachemshwa siku hizi. Kwa sababu nazi zinawashinda. Kwa hivyo ningeiomba serikali kwa makusudi, kwa kuwa mikakati ya serikali amri ikitoa ifuatwe, minazi ipigwe marufuku tena isikatwe katika nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linasikitisha tena linatuumiza kwa sababu ni kitu cha msingi kabisa, yaani katika nembo yetu ya Zanzibar inaonesha upande mmoja ni karafuu kwa kisiwa cha Pemba na kisiwa cha Unguja minazi. Leo minazi Unguja haipo, bora huko Pemba iko mingi kuliko hapa, sijui kuna nini. Kwa hivyo ningeomba sana serikali kupitia Wizara ya Kilimo jambo hili waliangalie, minazi inamalizika katika nchi yetu, nazi zimekuwa ghali kuliko kitu chochote sasa hivi. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili katika nchi yetu kuna mambo ambayo tunayategemea sana katika maisha ya binadamu, na katika kitabu hiki ukurasa wa 76 kuna tofauti ya uzalishaji wa madini kwa 2015/2016, tuna tani 200,000 tujiulize kuna nini. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nasikitishwa sana na mambo ya serikali upande wetu, hasa utaratibu sipingi kwa inavyokwenda lakini utaratibu bado hauridhishi. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wa Zanzibar asilimia 80 au 90 ni wanyonge na tuseme tu kwamba wanategemea sana ardhi yao kupata mahitaji yao mbali mbali, moja wapo likiwemo ni mchanga. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala la mchanga sina pingamizi nalo kwamba maeneo yanaharibika, lakini serikali kwa makusudi mimi naona kama pana kitu hakijaonekana. Kuna wananchi wana maeneo yao wenyewe, wengine walinunua ma-*plot* haya kwa ajili ya kuchimba mchanga lakini leo unaambiwa unakwenda kuchimba mchanga, fedha yote unalipa benki, wale wenye mashamba watalipwa nini au wanapata faida gani. Mhe. Mwenyekiti, haya manung'uniko yapo tena ni hatari na tena hayafai. Naiomba serikali kwa

makusudi hali ya mchanga katika nchi yetu utaratibu uliopangwa bado ni mbaya na hauridhishi. Serikali kabla ya kuingilia kati hili suala, mchanga ulikuwa unanunuliwa shilingi 60,000/- kwa gari ya aina *canter*, leo unakwenda mpaka kwenye 240,000/- au 200,000/-, umeupata rahisi kwa kuwa Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata tunakujua, kwa wewe mheshimiwa unafanya lako tupe mpaka 189,000/- ni hatari, mnyonge hajengi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa mfano kwa Hospitali ya Kijitoupele ambayo inaitwa Taveta/Magirisi. Lengo langu na madhumuni yangu kama ingelikuwa bei ya kawaida ningetumia mchanga kama 1,000,000/-, leo karibu milioni 3,000,000 na haijesha, kupiga plasta nje na ndani tu. Mchanga umekuwa ghali na adimu na pia una mashaka kuupata, upo ukienda umekaa lakini nasema tena ujenzi umekuwa mgumu kwa wananchi wetu wanyonge. Naiomba serikali itafute rai nyengine na njia nyengine ya utaratibu, si ya kuwadhulumu wananchi. Maana wananchi kwa asilimia kubwa sana au kubwa waliokuwa nayo wananung'unika na hakuna wa kumwambia au kuwaambia isipokuwa sisi Wawakilishi wao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri yupo wizarani, watendaji wake wanatembea mitaani huku wanajua lakini hawamwambii. Kwa kweli watu wetu wanapata shida sana na wanadhalilika, imefika wakati Mhe. Mwenyekiti, mnyonge hajengi. Bahati nzuri kampuni ya Dangote ni kiwanda kikubwa kwa Afrika Mashariki na Kati cha saruji kiko Mtwara. Huyu amesema mimi nateremsha bei ya saruji. Hivi sasa 13,500/- unapata saruji unayoitaka kutoka elfu 18,000/- na 20,000/-, lakini sasa saruji imekua rahisi, mchanga ghali, tunakwenda wapi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la kusikitisha nasema Wizara ya Kilimo sehemu hii tu naizungumza kwa udhati kabisa maana ndio madini yetu wa Zanzibar ndio Mwenyezi Mungu aliyotupa hayo hayo. Fusi lile la jasi pia lina masharti magumu. Leo mvua kama hizi sisi humo majimboni mwengine watu pa kupita hawana, kifusi kukipata pia kina mashaka kwa taratibu za maliasili. Je, tunaelekea wapi na tunafanya nini. Mimi ningeiomba Wizara kupitia kwa Mhe. Waziri mwenyewe alifuatilie suala la mchanga, alifuatilie suala la jasi na mengineyo ambayo ni kero kwa wananchi wetu, pia kuhusu kifusi tunachokitaka hatukipati au unakipata kwa dhiki na bei kubwa. Kwa hivyo serikali iangalie hili kuleta manusura kwa wananchi wetu na jamii yetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia tunategemea sana uvuvi katika nchi yetu. Mimi narudia tena kuishauri serikali tuna mipango mingi na utafiti mwingi. Lakini narudi

kusema Zanzibar sio wa kupata shida kwa bei ya samaki na Zanzibar si wa kupata umaskini wa kuuza samaki nje. Lakini kwa makusudi ningeiomba serikali iangalie kitu gani kitatusaidia, kama kuna meli au kuna watalaamu mbali mbali kutoka nje waje watusaidie ile *ZAFICO* zamani ilikuwa inatusaidia sana, alisema juzi Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwamba zamani unakwenda pale unapata samaki unaotaka saa yoyote, ikiwa mvua au ikiwa jua, ikiwa Kusi au Kaskazi au ikiwa shwari una hiari yako. Lakini ukenda pale unakwenda kupimiwa kama vibua, visehewa au nini ulikuwa unaridhika roho yako. Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, ni aibu na ajabu. Wenzetu Tanzania Bara, sehemu za Mwanza wana viwanda vya samaki vikubwa, wanaingiza fedha nyingi za kigeni, sisi tunashindwa Zanzibar tumezungukwa na bahari Unguja na Pemba lakini bahari kuitumia tunaiangalia hapa hapa kuifuatilia kuvua samaki hatuwezi.

Mhe. Mwenyekiti, naishauri serikali kwa makusudi hili waliangalie kama Mhe. Waziri aliwahi kutoa kauli akasema ikifikia muda fulani Zanzibar hatuagizi tena mchele, na hapa apige marufuku tena kwa nini tusisafirishe samaki kwenda nje, hapo nitampongeza sana vyenginevyo sifamhamu. Kwa hivyo naiomba sana wizara suala la uvuvi huo uendelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika bahari kuna zao la mwani. Zao hili ni kwamba halijathaminiwa. Wizara kupitia taasisi zinazohusika hawaangalii lina umuhimu gani kwa sababu karafuu ni zao kubwa lina mikakati mpaka nje ya nchi, na kuna vitengo vimewekwa hasa kulitangaza nje. Lakini mwani watu wetu asilimia kubwa wanaoishi katika vijiji vya pwani au katika bandari zetu wanategemea mwani. Lakini mwani huo leo hauna thamani, shilingi mia tano kwa kilo hautaki mtu, hiyo ni hatari. Kwa hivyo niiombe wizara hebu kama tunapigania zao la kilimo kwa jumla kutoka mikarafuu, mwani, minazi hiyo ninayoipigia kelele, tulitangaze hili zao na wananchi wetu wapate fursa ya kuwa na maisha bora katika nchi yao kupitia kilimo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine suala ambalo nitalizungumza hapa ni kilimo cha mpunga. Mhe. Mwenyekiti, tukitaka tusitake ardhi ya Zanzibar haina rutuba tena. Mimi wakati huo ni mdogo, bibi yangu alikuwa analima, anakaa kitako na kijembe kongoroka kile kidogo cha kupalilia, kutoka masafa ya hapa mpaka ulipo Mhe. Mwenyekiti, basi analima gunia kumi. Leo ekari kumi basi hupati gunia kumi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, haya ni masikitiko na bado wataalamu tunao wengi katika wizara, lakini bado sifa za kilimo kwa Zanzibar kilimo cha mpunga kimekwisha.

Zamani nakumbuka wakati mimi nasoma na wewe Mhe. Mwenyekiti, na wengi hapa tulikuwa, tunachukuliwa kwenda kupalilia mashamba ya mpunga ya JKU Mahonda, unakwenda Upenja na kwengineko, Kibokwa watu walikuwa wanavuna mpunga mpaka unasamehewa hauwezekani kuvunwa. Leo Mhe. Mwenyekiti, hamna tutafute kitu gani kilichosababisha hicho.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hapo hapo kwenye kilimo cha mpunga, tatizo jengine ninaloligundua mimi ni suala la kuwa na pembejeo zinazofaa. Kwanza matrekta hatuna ya kutosha, mbolea kwa wakati hatupati, mbegu safi na bora hatuna. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri hebu tutilie mkazo haya mambo matatu, matrekta, mbolea na mbegu safi. Ninaamini tutabadilika katika kilimo chetu tukipata mbegu nzuri za kisasa tunaweza kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitalozungumza hapa kwa ufupi kabisa ndugu yangu Mhe. Hidaya Ali Makame alizungumza suala la uvuvi wa majongoo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuulize Mhe. Waziri, yule mvuvi anapokwenda baharini kavaa ile miwani yake pamoja na viatu vyake vya kuogelea anaharibu mazingira gani. Mhe. Mwenyekiti, aje atwambia hapa Mhe. Waziri ili tusikie kwa sababu wananchi wetu ukivaa ile *glass* baharini na umevaa viatu unaambiwa unaharibu mazingira wengi wanakamatwa. Hili nataka aje atupe maelezo ili wananchi wasikie unaharibu mazingira ya aina fulani na jongoo linapokwenda kuvuliwa pwani Mheshimiwa halipigwi mshale wala umangu, yaani watu wa pwani tunajua umangu wengine hawajui. Lakini la kusikitisha wanaambiwa pia wanaharibu mazingira, wanaharibu mazingira vipi? Hebu itoke taaluma naiomba wizara kwa kuwa wanao wataalamu waeleze uvuvi wa majongoo unaharibu moja, mbili, tatu msiyavue au kama kuna sheria iliyowekwa nyengine pia waelezwe wananchi wetu wasiharibu mazingira yenyewe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kutokana na muda ningezungumzia suala dogo hili la mazao mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tuna kilimo cha mboga mboga nyingi ambazo zinakuwa vizuri sasa hivi. Ukienda kwenye tungule, mabilingani, bamia, pilipili boga na pilipili za kuwasha. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa ana malengo ya kumwagilia maji katika maeneo mbali mbali ya kilimo cha mpunga, basi na hawa tuwaangalie wapatiwe nyenzo za kuweka mifereji yao au visima vidogo ili tuhakikishe kwamba Zanzibar tusikose mambo haya ya mboga mboga. Leo wakati wa tungule nyingi Zanzibar, yaani Unguja na Pemba, kilo shilingi mia tatu tungule mtu hazitaki. Lakini unafika wakati ni shilingi elfu tatu mpaka elfu tatu mia tano kwa kilo. Sasa kwa kuwa uwezekano upo wa kuchimba visima vidogo vidogo, ningemuomba waziri sana katika maeneo yale wana ushirika wetu wamo wengi

katika maeneo, tumetembelea Pemba sisi Kamati yetu ya Wanawake na Watoto tumeona na hapa Unguja zipo sehemu tumetembelea tumeona. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri maeneo haya wasaidiwe wenzetu hawa ili kuongeza pato la kila siku, kwa sababu tuna pato la wakati wa jua na wakati wa mvua.

Mhe. Mwenyekiti, umeshaniwashia taa lakini baada ya hayo niseme tu kwamba namuomba Mhe. Waziri suala letu la mchanga atupe maelezo mazuri, suala la minazi inayokatwa ovyo Zanzibar hasa Unguja atueleze vizuri ili tuondokane na ukame huu tuliokuwa nao wa kukosa nazi na wananchi wetu kukosa mchanga wa kujengea.

Baada ya hayo naunga mkono hoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Machano Othman Said ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bismillahi Rahmani Rahiim.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo na nianze kuwapa Ramadhan Kareem Waislamu wote kwa ujumla pamoja na kuwapa pole wale wakulima wote waliofikwa na maafa ya mvua Unguja na Pemba. Lakini mimi nitaanza na swali hapo hapo kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Tunafahamu kwamba mvua zilizotokea za maafa haya zimeathiri sana wakulima Unguja na Pemba, na athari hizo wamezipata zaidi kwenye maeneo yao baada ya kujaa maji mengi sana na mazao yao yote kuharibika.

Je, wizara yake hadi hivi leo imeshafikia maeneo mangapi ya wale wakulima walioathirika Unguja na Pemba na wamejipanga kuwasaidia nini hasa kutokana na Ramadhani kuwa inakuja na wamejitahidi na wamekula hasara kwenye masuala ya kilimo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini Waziri pamoja na watendaji wake wanafanya kazi vizuri sana lakini hakuna binadamu aliyekamilika, wala wizara iliyokamilika. Nitamsifu kiupande wake kutokana na jitihada anazozichukua pamoja na wenzake, lakini vile vile nitakuwa na mawazo yangu machache kabisa pamoja na masuala yangu ambayo nitaomba nije nijibiwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba kutaka kujua suala la mchanga. Kwa ufupi Zanzibar suala hili limeathiri wananchi wote wa Unguja waliokuwa wanyonge, wa kati kati na hata hao matajiri na Waheshimiwa, sote tumeathirika ndani ya Unguja na Pemba kupanda kwa mchanga. Lakini tufahamu kwamba eneo lile la mchanga basi kuna maeneo ambayo ya watu ambao waliokuwa wakimiliki na katika maeneo ya serikali ambayo wamekwenda kuchukua ni maeneo ya watu, wameotesha miti karibu 62,000 ambayo imeoteshwa pale walinunua wakawekeza wenyewe kwa miaka mingi tu, lakini leo sehemu ile serikali imechukua. Mhe. Mwenyekiti, isitoshe kipindi cha nyuma Mhe. Waziri alipokuja kutujibu kwenye hoja yake, nakumbuka alisema kwamba moja ya sababu ya kuzuiliwa mchanga kuuzwa au kama ilivyo mwanzo imetokana na mahitaji makubwa ya nchi na hasa *project* mbili ambazo amezitaja ya Fumba na *project* ya *airport* ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hii imesababisha sana kwamba mchanga ule kuweza kuzuiliwa na kufuata hayo mambo mengine. Lakini mimi nitataka kueleza jambo ambalo mwenyewe nalifahamu, tusipendelee au tusifikirie wakati mwengine kuzuia kitu kwa watu wawili au mtu mmoja kwa wananchi wote kuwaumiza, leo tumeona athari yake. Tumezuwia mchanga kwa sababu labda ya *project* ya Bakhresa, *project* ya *airport* ambayo ya serikali, lakini athari yake sasa imekuja kuleta kwa nchi nzima, wananchi wote wamepata athari kwa watu wawili hawa. Maana yake tukizungumza serikali ni *airport*, tukizungumza Fumba ni ya mtu binafsi. Tunafahamu ni mzalendo mwenzetu, ni mfanyabiashara mzuri, ni *investor* mzuri ambaye anaongoza na anapenda kufanya mambo mazuri katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili suala lililoamulika kusema la ukweli halileti taswira nzuri na limeumiza wananchi kiuchumi. Leo gari ya mchanga ya shilingi laki moja na nusu inauzwa shilingi laki nne ya mchanga, gari ya shilingi laki mbili na nusu inauzwa shilingi laki saba na nusu hivi sasa. Kwa ufupi tofali zimepanda bei, tofali la shilingi mia saba imekuwa shilingi 1,200, gari zimepanda bei na pia na mahitaji mengine yamepanda bei, isitoshe huo mchanga juu ya hiyo shilingi laki saba pia kuupata tabu. Kwa kweli imekuwa hali ngumu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependelea zaidi kwa kushauriana na Mhe. Waziri kuna mambo mengine tunapofanya maamuzi tuangalie wananchi zaidi, hata kama nchi yetu tunataka kuijenga basi tutafute mbinu mbadala. Kwa sababu leo mimi naamini kama mungezungumza na mwekezaji kukubaliana naye Bakhresa ambaye ulimtaja na *airport project* ambayo mchanga mwingi

unatakiwa, kwa nini wasitumie meli zake za *sea link* mukenda mkachukua mchanga Tanzania Bara kwa watu wawili hawa.

Mimi naamini magari yapo mnayo, ilikuwa mukubaliane tu mumuondoshee kodi yeye pamoja na nyinyi wenyewe kwa watu wawili hawa asilipe kitu alete mchanga kutoka Tanzania Bara na kupakia kwenye meli zake za *sea link.*,Lakini leo tunampa mchanga mwingi kwa sababu tumezuwia wananchi huku wasichukue kwa sababu watu wanatumia sana mchanga. Hili limeathiri sana uchumi na ningependa sana Mhe. Waziri uje utujibu vizuri kama walivyoanza wenzangu. Suala hili la kwenda kuchukua wao Tanzania Bara litaleta athari gani au hasara gani ipo mukiondoshea kodi. Kwa sababu mchanga Tanzania Bara upo mwingi na hakutoleta athari na meli yapo ya kubeba mchanga kwa wingi. Sasa ningeomba hizi *airport* na hii *project* yake basi kama inawezekana ukachukuliwa mchanga Tanzania Bara na hawa Wazanzibari waliokuwa wanyonge na wa kati kati wapate mchanga kama kawaida ya kipindi cha nyuma.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha nyuma tani kumi ni shilingi laki mbili na nusu, sasa hivi shilingi laki saba na nusu na hii hali kwa kweli wananchi wameumia na hasa katika ujenzi na tunategemea kwamba tunazungumza hata Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inazungumza kwamba, maeneo yanataka kuwapa wananchi, wanataka kuwanyang'anya kipindi cha nyuma waliokuwa hawajajenga. Sasa hivi ilikuwa hapo mwanzo mambo yako chini hawakuweza kujenga sasa hivi vitu viko bei juu watajenga lini. Hii kwa kweli itakuja kuangusha uchumi na italeta athari kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri kwa busara zake naamini unaweza ukafanya njia nyengine mbadala ya kuhakikisha hili suala linarudi kama hali ya kawaida ilivyokuwa mwanzo. Kwa sababu hivi karibuni wameweka mpaka misumari, majiti, hakupitiki gari zimepata *puncture* haziendeki watu wamegoma huko. Na hii huwezi kushindana na wananchi, wananchi wana nguvu, wananchi ndio walioweka serikali madarakani na wao ndio ambao wametuweka hapa tukafika humu, leo tukisema tuwawekee vikwazo vyengine ambavyo vya kuwapandishia vitu au masuala magumu na wao hufanya mambo yawe magumu vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli serikali kushindana na wananchi haiwezi tukitaka tusitake, utakuja kuwaweza kwa njia nyengine lakini na wao watakuja kukuangusha kwa njia nyengine. Mimi ninachoomba kwanza nimpongeze hata Naibu Katibu Mkuu wetu wa Chama cha Mapinduzi kaweza kufika maeneo yale ya mchanga kuangalia hali halisi na nimpongeze tu kwa sababu ni Naibu

Katibu Mkuu jembe ambaye anapiga kazi vizuri sana, na anatizama haki za watu ziko vipi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala la mchanga naliacha Mhe. Waziri atakuja kutujibu vizuri lakini nitakwenda kwenye suala la soko langu la Kinyasini.

Mhe. Mwenyekiti, soko langu lile haliridhishi. Ningependa kujua soko lile lita-*cost* bei gani mpaka kumaliza na muda gani ambao wameekea kumaliza na *contractor* ambaye wamempa kujenga soko lile, ana uzoefu gani na kishawahi kujenga sehemu yepi mambo kama yale. Kwa sababu tunakuta kwenye masuala ya *MIVARF* kuna *four billions shillings* za miradi. Sasa mimi ningependa kujua lile soko langu lita-*cost* vipi, litamaliza lini, *contractor* aliyepewa pale ana uzoefu gani na kishawahi kujenga nini. Kwa sababu ilikuwa lile soko liwe la ghorofa, nasikia sasa hivi sio ghorofa tena. Soko lile lilikuwa liwe na *lift* nasikia imeondolewa kwamba itakuwa haipo. Mimi nitaomba nije nipate maelezo ya kutosha kwenye sehemu hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu jengine liko kwenye *deep sea* mambo ya uvuvi. Naamini tuna meli nyingi sana ambazo sio za Zanzibar au Tanzania ni watu ambao wako *off shore* wanavua lakini ni watu ambao wa nje. Ningependa kujua meli ngapi ambazo ziko *off shore* zinavua kwenye bahari yetu na zinalipa vipi. Kwa sababu tufahamu kwamba kuna *charges* za leseni ya ile meli kufika pale lakini pia kuna kuvua wale samaki kwa ma-*tones*, ningejua munawa-*charge* vipi kwa tone au labda kwa kila samaki. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tuangalie Mhe. John Joseph Magufuli kasema mtu hata akinunua pipi apewe risiti. Sasa kwa nini samaki mmoja Tuna anayefika shilingi laki tatu au mbili tusim-*charge* yule ni kwa mujibu wa samaki mmoja mmoja. Ningependa kujua, meli zilizokuweko kule ni za wazalendo wangapi na za *off shore* za wageni i zipo ngapi na zinaingiza pato lile kwa njia gani, muna-*charge* kwa *tone* ya samaki, muna-*charge* kwa *piece* moja moja ya samaki na halikadhalika. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nitaendelea kwenye suala la soko la Malindi. Mimi niliona kwenye mchangio kwamba soko la Malindi litagharimu karibu zaidi ya shilingi bilioni kadhaa. Soko hili ni lipi, kwa sababu ningependa kujua liko soko ambalo limeshajengwa pale. Sasa hili soko ambalo linatarajiwa tena kuja kujengwa ni soko lipi eneo la Malindi hasa la samaki kutokana na fedha ambazo zipo.

Jengine vile vile Mhe. Waziri mimi sijaona kwenye kitabu chako hasa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwamba

kwenye masoko haya ya kilimo, masuala ya matunda na vyakula. Wenzetu nchi nyingi sana duniani kwamba wizara mbili hizi zinaweza kusaidia kufungua viwanda vidogo vidogo na kusafirisha mazao yao kwenda nchi za nje kuuzwa, lakini mimi mpaka leo sijaona bado kwamba labda hapa Zanzibar mna *plan* gani ambayo mmeitaja humu ndani ya kitabu au mshaanza kwamba, labda wafungue kiwanda cha kusafirisha mihogo kwenye ma-*packets* kama wanavyosafirisha wenzetu, kiwanda cha kusafirisha labda *fruits* kama wanavyofanya wenzetu, viwanda vingi tofauti kutokana na mazao haya pamoja na mahindi ambayo yanawekwa kwenye ma-*plastic* kama nchi za wenzetu. Sijaona mimi wazo hili bado kwenye kitabu hiki kwa kushirikiana hasa na Wizara ya Biashara na Viwanda ili kuhakikisha hawa wakulima munawainuwa. Kwa sababu mimi cha kushangaa kitu kimoja, wakulima duniani wote wanakuwa matajiri sana na ni *multi millionaires*, *multi billionaires* kwenye masuala ya *family*, lakini kwa nini Zanzibar wakulima wanakuwa maskini. Mimi ningeomba sana wakulima wainuliwe kwa njia tofauti za viwanda kusaidiwa, fikra na msaada mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia hata kwenye jadweli hili la hizi fedha shilingi 25 bilioni mkopo za maendeleo, inaonesha dhahiri kwamba Wizara bila ya fedha za mkopo haiwezi kwenda kwenye masuala ya maendeleo, ni asilimia karibu 90 inategemea mkopo. Shilingi 25 bilioni mkopo halafu ukiangalia huku kwengine serikali inatoa shilingi 740, kwa ufupi asilimia 90 mpaka 95 wanategemea mkopo tu kwenye masuala ya maendeleo, inabidi wale wanaosaidia wakisema wasitoe misaada au kusipatikane kwenye benki au popote masuala ya maendeleo yatakwama kwa wizara hii. Sasa ningependa zaidi serikali kwamba wasitegemee sana masuala ya mikopo na hawa watu ambao wanasaidia na ninaamini wana imani ya kusaidia lakini wanaweza wakakwambia watakusaidia shilingi bilioni moja ukaja ukapata shilingi milioni mia tano, lengo lako limeondoka.

Mimi ningependa wizara yako Mhe. Waziri ungependelea zaidi uwe unaingiziwa kwenye bajeti kiwango ambacho unachokitaka kuliko kutegemea sana mikopo hasa kwenye masuala ya maendeleo. Kwa sababu suala la maendeleo ni suala muhimu lakini nimeona asilimia zaidi ya 90 kwamba umetegemea mkopo kwenye wizara yako.

Vile vile kuna mradi wa *MIVARF*. Mradi huu wa *MIVARF* mkopo ni shilingi 2,681,000,000, ukiangalia ruzuku hapa hakuna huu ni mkopo na serikali imetoa shilingi 739,000,000. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri hii miradi kwa sababu ni miradi ambayo inatumia mikopo au serikali inalipa iwe inaangaliwa sana, kwa

sababu *value for money* hakuna kwenye miradi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia soko unaambiwa shilingi bilioni fulani lakini thamani yake unakuta haifikii kile kiwango. Sasa hata zile nchi ambazo zinasaidia kwa misaada ile mikopo ambayo inachukuliwa kwa mujibu wa serikali na inalipa madeni, inakuwa inamtia serikali kwenye madeni, halafu isitoshe unakuta vile vile wale wanaotoa mikopo watakuwa hawaridhiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano soko la Kinyasini, ulikuwa hupo Mhe. Waziri lakini mimi nilijaribu kushiriki. Mhe. Mwenyekiti, ilikuja Kamati ya Bunge lakini hawakuridhika kabisa na maelezo ya lile soko la Kinyasini pamoja na thamani halisi (*value for money)* haipo, walikataa kweli kweli wakasema sana. Sasa naomba sana tuje tupate maelezo hizi *value for money* zinapangwa vip,kwa sababu takriban kwenye kila wizara *value for money* ya majengo hakuna sio wizara yake tu, wizara zote. Kwenye kutumia kitu kimoja tu ndio kina *value for money*, vitu vya serikalini sijui vinajengwa na nani au *tender* zinakuwa zinapitishwa vipi, watu wanafanya nini havifahamiki. Sasa hii ni kuitia serikali katika *short* ya madeni na wale wanaotoa msaada mara nyingi wanapenda kuona msaada wao wanapotoa kitu kinakuwa *valued* kinaridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimekuta eneo moja mulikwenda katika ya ufunguzi wa kuhusu masuala ya uvuvi Pwanimchangani, kuna *paragraph* fulani hapa uvuvi, samahani kidogo naomba niiangalie, hii hapa Pwanimchangani mulikwenda mukafanya uzinduzi wa masuala ya uvuvi na mulikwenda kwenye jimbo langu Mhe. Waziri. Mimi ningeomba ziara zozote za kiserikali munapofanya kwenye majimbo basi wawaambieni Wawakilishi na wenyewe wawepo. Kwa sababu hili tumegundua sana zinafanyika ziara tofauti za wizara, wanakwenda mawaziri unasikia tu kenda waziri fulani, lakini taarifa kwa Mhe. Mwakilishi mwenyewe inakuwa haipo hajui na alipaswa kuwepo pale angalau na yeye akashuhudia kinachoendelea ili ajue hata akitaka kuja kuwateteeni nyinyi pamoja na akiuliza swali ajue anajibiwa nini. Leo tunaona Mhe. Rais anakwenda kwenye majimbo sisi tunapata taarifa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio wizara yake tu, mawaziri wengi wanaingia kwenye majimbo, kama jimbo langu mimi ijapokuwa na wao wana haki lakini walikuwa watupe taarifa tukaone yale maendeleo yanayofanyika. Kuna miradi ya maji hatujawahi kualikwa, kuna mambo ya afya watu wamekwenda kwa njia nyengine hatuambiwi. Sisi kwa upande mwengine ni Marais wa majimbo, Rais wa nchi tunamfahamu nani lakini sisi Wawakilishi ni Maraisi wa majimbo. Mhe. Rais anapofanya mikutano yake yote anapokwenda jimbo fulani huambiwa sisi, Mhe. Rais anakuja *in advance* siku tatu, lakini kwa nini Mawaziri munapokwenda kwenye majimbo hamutuelezi. Sisi hatutaki kitu

tunachotaka kwamba tuweko pale tufahamu nini kinaendelea na sisi tutakuja kuwateteeni mlikuja lakini tunaona kwenye vitabu, Mhe. Waziri sikulaumu peke yako lawama hizi kwa Mawaziri wote wanaokwenda kwenye majimbo bila ya kuwaambia Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ninakupongezeni sana la kuangamiza hawa kunguru pamoja na kutibu mbwa vichaa na wale kima wengine, lakini mimi niliwahi kulizungumza. Sasa hili suala ni zuri la kuangamiza kunguru na kweli wamepungua, walikuwa wanakera sana, maudhi mengi pamoja na wale kima wanaoharibu mambo ya kilimo. Lakini ukiangalia kwenye suala la mbwa vichaa wamezagaa mjini, mbwa wako wengi sio wa vichaa lakini wale mbwa koko wako wengi ambao hawafugwi na watu. Ningeomba sana wizara yake ikatafuta gari maalum na watendaji maalum kuja kuchukua wale mbwa kwenda kuwaficha sehemu mukawaondosha katika mji. Mimi nashangaa nchi nyengine wanauza mbwa wanakula kwa nini musiwauzie. Kwa sababu nchi nyingi tunafahamu kwamba wanakula mbwa, sasa sisi tuna mbwa hawana kazi kwa nini musiwauze mukapata mapato.*(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri nimshauri kwamba wale mbwa wote na paka ambao hawana malezi, hawana watu ambao wanaowafuga, basi wawachukue wakawapeleke sehemu ambazo wanajua wao nzuri. Hili suala la kula mbwa Mhe. Waziri mwenyewe anajua mbwa wanaliwa wapi kama China au wapi, Korea wanakula tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kusema kweli nina mambo mengi lakini kutokana na muda na isitoshe *department* hii sio yangu, kusema la ukweli kila mmoja na fani yake. Naamini Mhe. Waziri anafanya juhudi nyingi tu kwenye masuala ya uvuvi, kilimo na mengineyo. Lakini pia ningependa kujua Mhe. Waziri wamejiandaa vipi kuhakikisha hawa wavuvi wanyonge wanawatafutia boti za kwenda *deep sea* kuvua, hawana viboti vyao wanafika hapa kati kati tu na sehemu za karibu. Lakini leo mukiwapatia mukiwawezesha kwa mikopo kuwapatia boti au ikiwezekana hata ya kuwagawia kwamba kila Wilaya au kila kikundi kikubwa sana wakapewa, wakaenda kuvua kule halafu wakalipa kodi si tatizo. Hii itasaidia kuwainua wavuvi kwenye masuala ya uvuvi kwenye kuwapa uwezo na kuweza kulipa kodi vile vile.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nitakuomba sana uwaone sana na hasa jimbo langu pia katika jimbo lililopata maafa masuala ya kilimo. Mimi mwenyewe nimekwenda karibu sehemu zote zimefukiwa na maji na majimbo ya wenzangu. Namuomba sana basi wizara yake iwapatie vifaa au masuala ya

mbegu ili waweze kujiendeleza na hasa na katika mwezi huu Ramadhani inayokuja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisipoteze muda sana namshukuru Mhe. Waziri na asilimia 85 nai-*support* hotuba hii, 15 nasubiri yale masuala niliyouliza nije nijibiwe halafu ndio niikubali.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi akifuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na kama muda utakuwepo basi Mhe. Shehe Hamad Mattar ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kuniruhusu kuweza kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Lakini vile vile kabla ya kuchangia kwanza nichukue fursa hii kuwatakia Waisilamu wote ulimwenguni hususan Tanzania na Zanzibar na hususan katika jimbo langu la Magomeni kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunaoutarajia hivi karibuni. Mwenyezi Mungu atupe afya na atupe wepesi katika kuifunga Swaumu hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri lakini na watendaji wote wa wizara hii inayohusika kwa kuweza kutuandalia hotuba hii ambayo kwa kweli imesheheni mambo mengi sana. Mimi kilichonifurahisha zaidi katika hotuba hii kuweza kutaja changamoto na jinsi gani watakavyozishughulikia changamoto hizo. Niipongeze sana wizara hii kwa sababu katika hotuba zote ambazo zimewashilishwa hapa sikuwahi kuona hotuba ambayo imetaja changamoto na jinsi gani watakavyozishughulikia. Niwapongeze sana.(*Makofi*).

Lakini vile vile niipongeze sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa hotuba yao nzuri ambayo kama itafanyiwa kazi kwa wizara inayohusika basi itasaidia sana katika suala zima la utekelezaji na kuweza kufikia maendeleo katika Sekta hii ya Kilimo, Mifugo na Misitu na hususan muwasilishaji wetu wa hotuba hiyo Mhe. Hamida Abdalla Issa kwa ufasaha wake na umahiri wake katika uwasilishaji.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ni muhimu sana, kilimo ndio uti wa mgongo, kilimo ndio uhai, kilimo ndo uchumi. Kwa kweli tunapaswa kuweza kuichangia

hotuba hii na kuweza kuwapa moyo wenzetu kutokana na juhudi zao wanazozifanya za kuweza kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo katika sekta hii ya kilimo, kwa sababu bila ya kilimo uchumi wetu kwa kweli hauwezi kupiga hatua. Kilimo ni uhai, bila ya kilimo maisha yetu hayawezi kuendelea kama vile ambapo tumepaswa. Kwa hivyo tuna kila sababu ya kuweza kuichangia hotuba hii na hatimae tuweze kuipitisha, kwa sababu mimi nina matumaini makubwa sana na Mhe. Waziri wa Kilimo kwa ile ahadi aliyoitoa kwamba ataviwezesha visiwa hivi kuweza kujitegemea kwa chakula katika kipindi cha miaka mitatu. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri na nina matumaini makubwa na yeye.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika michango yangu na nianze katika hii programu ambayo inahusiana na mifugo. Lakini kwanza niipongeze wizara kwa kuweza kushajihisha wafugaji na kuongeza nyama ya kuku, kuweza kuongeza idadi ya mayai, kuweza kuongeza idadi ya maziwa kama walivyoeleza katika hotuba yao. Mhe. Mwenyekiti, tunapaswa kuwapongeza kwa hatua hii ya kuendeleza lakini bado tukubali kwamba tuna changamoto ya uhaba wa nyama ya kuku, tuna changamoto ya uhaba wa mayai na tuna changamoto bado ya uhaba wa maziwa. Mhe. Mwenyekiti, lazima tukiri na wizara inapaswa kuongeza juhudi zake katika kushajihisha wananchi. Lakini vile vile niwapongeze sana wakulima wadogo wadogo kwa juhudi zao wanazozichukua. Lakini pamoja na hilo Mhe. Mwenyekiti, wakulima wetu, wafugaji wetu wana changamoto kubwa ya mitaji yao.

Mimi nina imani kwamba kama serikali itatafakari na kuweza kuiga wenzetu katika nchi ambazo zinaendelea ya kuweza kuwapatia ruzuku, tufanye utafiti kwanza wale wafugaji ambao wako makini, wamepata elimu na wanaonesha dalili za maendeleo. Mimi nina imani kwamba kama tutapata wafugaji makini mia mbili katika Zanzibar na tukaweza kuwapatia ruzuku na mafunzo vizuri, mimi nina imani tutapiga hatua kubwa sana katika uzalishaji kwenye kuku, maziwa, nyama ya ngombe na kadhalika na kadhalika.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ni suala zima la changamoto ya wizi, wenzetu hawa kwa kweli katika kipindi hichi wanakabiliwa sana na wizi wa mifugo, wizi wa mazao mbali mbali. Mimi nafikiri umefika wakati sasa Wizara ya Kilimo ikae kuweza kufikiria suala zima la bima, wenzetu hawa nafikiri wanahitaji kupewa bima, wapate bima ili wanapotokezewa na majanga haya ya kuibiwa mifugo au mazao basi waweze kupata fidia. Katika nchi zilizoendelea masuala haya hakuna. Nafikiri umefika wakati kwa sababu inawezekana mkulima tumempatia msaada wa kumpa ng'ombe wa maziwa au mbuzi wa maziwa au kikundi fulani. lakini utasikia mbuzi ishirini wameibiwa usiku

mmoja au kuku mia moja wameibiwa usiku mmoja. Kwa kweli hii inarejesha nyuma sana wakulima wetu na wafugaji, umefika wakati tuwapatie bima ili kuweza kuona kwamba wanapata fidia pale ambapo wanapatwa na majanga haya. Vyenginevyo ile kasi ya ufugaji na ukulima wa mazao mbali mbali basi inaweza ikapungua.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika programu ya uvuvi. Kwanza niipongeze sana wizara kwa elimu wanayoitoa kwa wavuvi wadogo wadogo. Kwa kuendelea kusimamia hifadhi za ghuba mbali mbali ambazo zimo katika bahari yetu, vile vile kuweza kudhibiti kwa kiasi kikubwa uvuvi haramu pamoja na kwamba bado unaendelea. Lakini kwa ile azma yao na malengo yao ya kuweza kuanzisha kampuni ya uvuvi ambayo inasomeka kwa jina la *ZAFICO*.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo napenda niishauri wizara kwamba tunataka kuanzisha Shirika hili la Uvuvi na nilivyoisoma hotuba hii kwamba tayari tunawakaribisha wahisani au makampuni ya kigeni ambayo yanaweza kushirikiana na serikali katika kuendesha kampuni hii. Nafikiri ni wazo zuri sana, nafikiri tutaweza kuondosha lile tatizo la hivi sasa la Wazanzibari kuweza kutumia samaki wa mapeduu kutoka nje. Kwa sababu zoezi hili kama walivyotangulia kusema Wajumbe waliotangulia, Zanzibar katika kipindi fulani tulikuwa na Shirika la namna hii na ukweli tulikuwa na samaki ambao kwa kweli walikuwa wanatosheleza.(*Makofi*).

Sasa kwanza tusome tuliteleza wapi baada ya shirika lile kufa kabla ya kuanzisha hii. Lakini tunapoingia kwenye mikataba na makampuni haya ya nje, ningependa sana Mhe. Mhe. Mwenyekiti, Waziri anifahamu kwamba lazima tuwe makini kwa sababu wenzetu ni wazoefu ambao tutaingilia nao mikataba, sisi ndio kwanza tunataka tuanze uvuvi wa bahari kuu. Kwa hivyo mikataba hii inahitaji umakini. Wenzetu wengi ni wajanja kwa hiyo tuweze kuona hila zao mbali mbali na kuweza kusoma *back ground* yao wanakotoka juu ya suala hilo. Lakini wenzetu wana uzoefu vile vile. Kwa hivyo inabidi sana tuweze kufanya utafiti wa kina na makampuni ambayo tutaingiliana nayo mikataba katika uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile wakati mwengine sisi wenyewe watendaji tunakuwa na ulafi tunapoingiliana mikataba. Ulafi huu ndio unaweza kupelekea mikataba mibovu. Niiombe sana serikali itakapoingia mikataba katika uvuvi wa bahari kuu, basi sisi watendaji wenyewe tuache ule ulafi kwa sababu nao unachangia. Mhe. Mwenyekiti, katika hili vile vile tuwe tayari kuwatayarisha wazalendo kwa sababu kama tutawekeza katika uvuvi wa bahari kuu, basi vijana wetu wengi wanaweza kupata ajira. Lakini sasa iwe wana ujuzi kama

hatujaanza sasa kuweza kuwaanda vijana ambao wanaweza kuvua bahari kuu, basi tutakuja kuona kwamba ajira hizi katika kuwekeza bahari kuu zinachukuliwa na wageni na hilo sio lengo letu. Lengo letu tuweze kukuza uchumi lakini vile vile kuweza kukuza ajira kwa vijana wetu. Mimi nina imani kwamba inawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili hili la uvuvi wenzetu tuwapongeze kwa kuweza kutoa misaada mbali mbali kwa wavuvi wetu wadogo wadogo, lakini niwaombe sana wenzetu katika utoaji wa misaada hii ya vifaa vya uvuvi wawe makini sana katika ufuatiliaji. Nafikiri tuna tatizo la ufuatiliaji. Mimi nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, kwamba tulikuwa na mradi wa *MACEMP* hapa ambao serikali tuiopongeze sana ilitoa vifaa mbali mbali zikiwemo boti, injini, nyavu na kadhalika.

Lakini nimuombe Mhe. Waziri afanye utafiti vikundi vilivyopata vifaa hivyo hivi sasa vingapi ambavyo vinaendelea na hali hiyo. Kwa sababu tusikazie tu kuweza kuwapa vifaa lakini tukazie vile vile kufuatia maendeleo yao, vyenginevyo hatuwezi kufika mbali. Lakini niwapongeze vile vile kwa kuweza kuangalia suala hili la kufuga au kwa kuweza kuweka hii sehemu ya ufugaji wa vifaranga vya samaki, ingawa mimi sipendi kulitumia neno hili kwa sababu vifaranga mara nyingi huwa vya kuku, napenda nitumie labda vitoto vya samaki au vichanga vya samaki. Huu ni mradi mzuri ambao utasaidia wafugaji wetu wa samaki katika visiwa vya Unguja na Pemba na ambao hivi sasa wananchi wengi wameshajihika na hilo. (*Makofi*).

Kwa hivyo niwaombe sana waandaliwe sasa wafugaji wetu wa samaki kwamba huu mradi upo lakini ikiwezekana kuweza kuwatafuta wale ambao wana muelekeo wa ufugaji wa samaki ili kuweza kuanza kuwapa ruzuku ya kuweza kuwapa hivi vifaranga kama ulivyotamka Mhe. Waziri, ili sasa tuweze kuona ufugaji huu wa samaki nao unapiga hatua. Na nimefurahi sana kuona hata kwamba mna vifaranga vya pweza, vifaranga vya majongoo na nakadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Mhe. Mwenyekiti, niishukuru sana serikali kwa kufikiria kuwa na Taasisi hii ya Kilimo kwa sababu hapo nyuma vijana wetu au wananchi wetu walikuwa wanapata elimu za kilimo katika sehemu ya Tanzania Bara zaidi na nchi nyengine, kuwa na chuo cha namna hii katika nchi yetu ni faghari kubwa sana na ukweli kimeweza kusaidia kutoa wahitimu wengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi najiuliza kwa sababu tunao wahitimu wengi mitaani lakini kumuona mhitimu amemaliza Stashahada ya Kilimo lakini hata tuta la

mchicha hana, hii inanisikitisha sana. Kwa sababu hawa ambao vijana wamemaliza ndio ambao sisi tunataka wawe ni kioo, wawe ni mfano kwa wananchi wetu au wakulima wetu wadogo wadogo mitaani. Vijana wengi sana ambao wanamaliza *mindset* zao ziko katika kuajiriwa kuliko kujiajiri.

Mimi nafikiri umefika wakati Mhe. Waziri hili alitizame uzuri kuweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali, kilimo tunawafundisha lakini ujasiriamali na aweze kuamini kwamba taaluma anayoipata inaweza ikamfanya yeye kujiajiri na baada ya kumaliza basi wachukue juhudi ya kuweza kuwashajihisha kukaa katika vikundi na hatimae waweze ku-*apply* ile *knowledge* na *skill* ambayo wameipata ili waweze kuitumia katika uzalishaji, kama ni katika kilimo au katika mifungo. Vyenginevyo vijana wengi itakuwa tumewapa elimu hii wa kilimo lakini wanategemea serikali iweze kuwaajiri, nafikiri hatutofika mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikiombe sana chuo hichi kuweza kuwa na utaratibu maalum wa kuweza kuwafuatilia wahitimu wako wapi na wanafanya nini. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina mfano mdogo sana katika Chuo changu pale cha Ushoni. Vijana wote waliomaliza pale basi nina- *contact* namba zao na nina wauliza mko wapo na mnafanya nini na tunawapa misaada ya kuweza kuona kwamba wanajiajiri. Sasa sisi tumezalisha wengi lakini *mindset* zao, kwanza hichi kilimo wanaona wao sio kazi ambazo inaweza ikawatilia kipato, wao wanaona wamepata elimu ya kilimo kwa lengo la kuajiriwa. Sasa hii ni hatari lazima tuweze kubadilika na kuweza kubadilisha mitazamo ya wanafunzi wetu. Lakini vile kuweza kuona mazingira haya ya chuo hivi sasa yanaweza yakafanya kwamba kilimo kiwe cha kisasa. Chuo hichi utakwenda trekta halipo. Hivi sasa tunazungumzia mambo ya *green house,* sijui kama ipo pale chuoni alau wana chuo wanaweza kujifunza nini *green house*. Hivi sasa wakulima wanatakiwa kubadilika na kuwabadilisha ni vijana ambao wamepata taaluma katika kile chuo wanapokwenda katika Wilaya zao au katika Mikoa yao. Sasa ikiwa chuoni hakuna vile vifaa na dhana bora, sidhani kama kutakuwa na maedeleo na yale mapinduzi ya kilimo ambayo tunayaatarajia.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la tafiti na majaribio. Tafiti na majaribio niipongeze sana serikali na wizara kwamba imefanya tafiti na majaribio 11 ya mbinu za uzalishaji wa mazao, ni jambo zuri sana. Lakini tunatarajia sana tafiti hizi ambazo zinafanywa Zanzibar ndizo ambazo ziwasaidie wakulima wetu. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na *tendency* kubwa sana ya kuchukua matokeo ya tafiti zilizofanywa nje na ambayo yametupa hasara kubwa sana. Kipindi fulani hapa si miaka mingi tulileteawa mbegu ya *NERICA*, hivi sasa sijui iko wapi na hii wamefanya tafiti wenzetu sio sisi,

tulikuwa na minazi chotara ilifanyiwa tafiti kutoka nje na tukazichukua sisi, tukapanda minazi chotara hivi sasa hakuna minazi inayozaliwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana hivi sasa serikali yetu ina wataalamu wengi sana hususan Wizara ya Kilimo ina watu wana *PhD,* wafanye tafiti hapa hapa Zanzibar ili utafiti wa hapa matokeo yake ndio ambayo yatasaidia wakulima wetu, kuliko kuweza kuchukua matokeo ya tafiti zilizofanywa nje au nchi jirani. Mimi nafikiri hatuwezi kufika mbali katika hili. Niiombe sana wizara iwatumie wataalamu wafanye tafiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nizungimzie suala zima la udhibiti wa wimbi la uvamizi wa maeneo. Mhe. Mwenyekiti, wanazungumzia wenzetu kwamba wanaendelea na udhibiti na wimbi la uvamizi wa maeneo ya kilimo, misitu na mifugo. Mimi nafikiri serikali lazima ifanye juhudi kubwa. Hivi sasa Mhe. Waziri mimi nataka ufanye ziara na nina hakika unafanya ziara, uko karibu sana na wakulima lakini uwe karibu sana na wananchi wetu, maeneo mengi ya eka tatu tatu, hivi sasa yameuzwa na nyaraka zake sasa zimebadilishwa kwamba ni mashamba sio eka. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ningependa sana kama ulivyoeleza hapa ushirikiane na dada yangu Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili muweze kufuatilia maheka haya na mengine tayari yameshajengwa makuta, eka hizi hizi zimeshajengwa makuta. Sasa tunatarajia kilimo hicho kitakuwa wapi, misitu hiyo itakuwa wapi, ufugaji huo utakuwa wapi, ikiwa eka tatu hizo hivi sasa zinakatwa viwanja, hatuwezi kufika. Wilaya ya Kati tembelea. Leo katika kipindi cha redio cha mawio nimesikia Mkuu wa Mkoa wa Kusini anazungumzia suala hilo. Ningependa sana uzunguke uwasiliane na Wakuu wa Wilaya na Mikoa ili kuona ukubwa wa tatizo. Vyenginevyo hatutokuwa na ardhi. Hichi kilimo sijui tutakifanya wapi au mbinguni au wapi. Lakini kwa muda mdogo sana hatutokuwa na ardhi Mhe. Mwenyekiti, lazima tujitahidi katika hilo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana Wizara hii kwa juhudi zake inafanyakazi kubwa lakini bado tuna kazi ya kufanya kwa sababu miaka ya 1978/80 tulikuwa na maendeleo katika *irrigation*, tulikuwa na maendeleo katika mifugo, lakini leo tuna wataalamu wengi lakini vitu hivi vimedidimia sijui kwa nini. Lazima tukae kitako na kuweza kujifunza tumeteleza wapi ili sekta hii ya kilimo, mifugo iweze kuendelea.(*Makofi*).

Baada ya hayo niwashukuru sana kwa kunisikiliza na nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe

tuipitie hotuba hii vizuri, tuishauri wizara vizuri na serikali ili maendeleo yaweze kupatikana.

Naunga mkono asilimia kwa mia hotuba hii. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said ambaye atakuwa mchangiaji wa mwisho.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi Ijumaa ya leo kuja hapa Barazani kuzungumzia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Aidha naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii na *inshaallah* nitatumia dakika zangu vizuri.

Pia naomba nitoe shukurani kwa Mhe. Waziri kwa wizara na watendaji wake kwa juhudi zao kuimarisha kilimo, uvuvi na ufugaji. Mhe. Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo na Wizara hii inabeba matumini ya wananchi. Mhe. Waziri mwaka jana aliwaahidi wananchi wa Zanzibar kwamba apewe muda ili kumaliza tatizo la uagiziaji vyakula na bado wananchi wanampa muda na marajio yao kwamba ahadi ya Mhe. Waziri itatekelezeka.

Lakini kama walivyozungumza baadhi ya Waheshimiwa inaweza kuwa ngumu sana ahadi hii kama tutaendelea na kuruhusu ujenzi holela katika maeneo ambayo yalikuwa ya kilimo. Baadhi ya maeneo ukipita unaona hasa kwamba juhudi zetu zinakwama kwa sababu hatuko makini katika kusimamia maeneo ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza hapa kwamba mvua kubwa za masika zina baraka zake, lakini zina athari zake na miongoni mwa athari zake ni kuharibika kwa mazao, na ukiachilia mbali pengine wakulima wa mpunga lakini wakulima kama wa mihogo ambao tayari ilikuwa kwa kuliwa wakati huu wa Ramadhani, sehemu nyingi mihogo yao imeingia maji na imeharibika vibaya sana. Kwa hivyo nafikiri wizara watachukua juhudi za makusudi kuwasaidia wakulima hawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo ilikuja na mpango wa kuimarisha miundombinu katika maeneo ya kilimo, na miongoni mwa miundombinu hiyo ni ujenzi wa barabara kwa kupitia mradi wa *MIVARF*.

Kwa bahati nzuri mimi katika Jimbo langu la Mfenesini nilibahatika kupata barabara ya *MIVARF*, barabara kutoka Mwachealale, kutoka Mwakaje kupitia Mwachealale hadi Bumbwisudi ni mradi wa *MIVARF*.(*Makofi*).

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia hali halisi ya *value for money* na zaidi alizungumzia kwa soko la Kinyasini. Mimi nazungumzia *value for money* kwa barabara za *MIVARF*, ama hawakushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ya wakati ule au haukuzingatiwa ubora wa ujenzi wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, barabara zile zilimalizika mwaka jana lakini ukipita leo utashangaa hali ilivyo. Barabara yetu sisi ya Mwakaje, Mwachealale mpaka Bubwisudi, eneo kati ya Mwakaje na Mwachealale karibu litakuwa halipitiki kutokana na ubovu wa barabara. Lakini pia upande wa pili kutoka Mwachealale kuelekea Bubwisudi, yapo maeneo ambayo imekatwa barabara baada ya mvua hizi za masika, gari zinakwama. Mhe. Waziri nilisikia zile barabara bado hazijakabidhiwa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kama zimekabidhiwa basi mimi naomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tushirikiane tuitembelee ile barabara na kama bado basi Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ujenzi tushirikiane tukazione baada ya mvua za masika zile barabara lazima zitengenezwe, vyenginevyo wananchi wa Mwachealale watakatwa na watageuka kisiwa ambao watakuwa hawana mawasiliano na wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nirukie katika shughuli za uvuvi. Mhe. Waziri nakuomba sana baada ya kumaliza kikao cha bajeti, wewe na wataalamu wako wa uvuvi mutembelee Jimbo la Mfenesini. Yapo maeneo ya Kama na Chuwini yana wavuvi wengi na yana bahari. Kuanzia eneo la *Sea Cliff* mpaka Hakuna Matata ni eneo la bahari ambalo liko katika Jimbo la Mfenesini, lakini wananchi bado wana malalamiko yao ni vizuri twende kwa pamoja ukayasiklize kwa kupitia wataalamu wako tupate ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, pia hapa nataka kuzungumzia hali ya masoko. Naliacha kwanza hili la Japan, nayazungumzia haya tuliyonayo. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Tulipata fursa ya kutembelea baadhi ya masoko kwa kupitia kamati yetu, likiwemo soko la Tumbe na soko la Msuka. Mhe. Mwenyekiti, haya masoko yamejengwa yamepoteza fedha za serikali hayatumiki kabisa. Nilipokuwa Tumbe pale nilitamani lile soko nilinyanyuwe niondoke nalo nijenalo mpaka Jimbo la Mfenesini niliweke sehemu kwa ajili ya maendeleo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa sijui serikali haioni kwamba fedha kama zile zinapotea, inakuwa shida. Yaani watu wanajengewa masoko ya kisasa na ya kileo anakwenda kufungua Mhe. Rais, lakini hawayatumii na wanayawacha wanaona kama hawakufanyiwa kitu. Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo liangaliwe.

Lakini la pili kuhusu soko hili la Japan. Wajumbe wengi wakisikia hizi fedha tunaona nyingi bilioni 12. Lakini mimi naomba Mhe. Waziri tusije tukajengewa banda la kununulia samaki na kuuzia samaki. Tujengewe soko la samaki, soko liwe na eneo ambalo mtu anaweza kuchagua samaki, akanunua samaki na halafu akachomewa samaki, akala samaki na vyakula vyengine kwenye soko. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunazungumzia utalii. Wenzetu nchi ndogo na maskini kama sisi wana masoko masafi, wana masoko sehemu ya kuuza samaki wa kila aina na wana sehemu ya watu kwenda kupumzika *weekend* na kula samaki hapo hapo, wanatumia kuuza masaa matatu. Haiwezekani nchi ya visiwa unakwenda sokoni kununua samaki unafumba pua kwamba hapa nanunua samaki naondoka mbio, yale ni mabanda ya samaki hatuna masoko ya samaki. Kwa hivyo Mhe. Waziri katika ujenzi wa soko la samaki jipya tusije tukafanya makosa, ni lazima kuwe na sehemu hata watalii wataweza kukaa na wananchi wa Zanzibar waweze kukaa, wale samaki na vyakula vyengine katika eneo ambalo litakuwa halina matatizo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nijue hoja na msingi wa serikali kuamua kuunda Kampuni ya *ZAFICO* badala ya Shirika au mambo mengine, pengine zipo hoja za maana kwamba kwa nini tukaamua kuunda Kampuni. Mimi nina wasi wasi kidogo na kampuni ufanisi wake utakavyokuwa badala ya Shirika au mambo mengine. Kwa sababu nchi yetu sisi ya visiwa, kwa hivyo haya mambo ya uvuvi lazima yawe na uzito mkubwa sio kama tunavyochukulia kwamba ni jambo dogo. Uvuvi ungekuwa tunaushughulikia hasa pengine ungelichukua asilimia 50 ya ajira ya Wazanzibari wote. Kwa hivyo ni lazima tujiandae kufanya shughuli za uvuvi katika kiwango kikubwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nije kwenye Idara ya Misitu na Maliasili Zisizohamishika. Waheshimiwa wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wametoa mapendekezo yao na zaidi kuhusu suala la mchanga. Mhe. Waziri suala hili linatuumiza sana. Mimi sijawahi kusimama nikaipinga bajeti ya wizara ya serikali, kwa sababu na mimi nimekaa serikalini miaka 10 mfululizo. Lakini kwa suala hili la mchanga mimi nitaipinga wizara hii ya kilimo leo. Labda tukubaliane mambo ya msingi. Kwanza hivi kwa nini wananchi ambao

waliokuwa wanamiliki mashamba ya mchanga wamenyang'anywa mashamba yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, najua kulikuwa kuna utaratibu hawakuwa wakijichotea mchanga tu. Utaratibu wa mwanzo ulikuwa ukitaka kuchimbiwa mchanga unakwenda kuomba Wilayani, unaanza Halmashauri, baada ya Halmashauri unakwenda kwa Mkuu wa Wilaya anaangalia na akiridhika linaletwa ombi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kupitia Idara ya Maliasili. Idara ya Malisasilia wanakwenda kukagua na kujiridhisha kwamba hapa panastahiki kuchimbwa mchanga na ilikuwa kuna orodha. Kwa mfano pengine kuna mashamba 10 au 15 yanataka kuchimbwa mchanga. Tunakubali kweli mchanga umepungua lakini suluhisho sio kuwanyang'anya watu wenye mchanga, serikali ingebakia na uratibu wa mchanga kwa kuweka vikwazo ili mchanga usichukuliwe ovyo lakini bado mashamba yabakie kwa wananchi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza hapa kwamba kuna wengine wameyaendeleza mashamba kwa miaka 15, waliyakuta mashamba hayana kitu, wametumia ma-*bulldozers* kusafisha, wamepanda miti karibu hekari 16, wana miti wanavuna, serikali imekwenda kukata miti yao inachukua mchanga, serikali inatumia bunduki kuwafukuza wenye mashamba. Hivi kweli ndio tunawafanyia haki na kwa bahati mbaya asilimia 90 ya wenye mchanga wako katika Jimbo la Donge, Mahonda na Bumbwini. Hawa wananchi wafanyekazi gani, hawa wananchi wamepata hasara Mhe. Mwenyekiti wanalia, serikali imeshindwa kukaa nao kufanya nao mazungumzo na kuwajua kiasi gani walipwe. *(Makofi)*

Leo Mhe. Waziri anatuambia mapato ya serikali yametoka milioni 100 na yamekuwa milioni 584. Ni kweli kwa sababu zile fedha zilichukuliwa kwa wananchi, hakuna njia nyengine kweli ya kuzungumza. Mimi naamini bado serikali ina nafasi na kaka serikali inashindwa basi Mhe. Mwenyekiti, itumiwe Baraza la Wawakilishi, tuunde Kamati Teule ya Kuchunguzia Mchanga. Tuunde kamati tuzungumzie suala hili ni kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe hapa walizungumza kwanza wenye mashamba wanalalamika, kwa nini iwe sisi tu, kwa nini wa mawe hawamo, kwa nini wa kifusi hawamo, kwa nini wa mikarafuu hawamo, kwa nini wawe wao tu. Ardhi ya serikali lakini wamekabidhiwa wananchi na serikali haifanyi biashara. Leo serikali imegeuka inafanya biashara ya mchanga, serikali hata mchele na nini iliwaachia wananchi wauze. Leo kwa nini iwe mchanga, kwa

nini isiwe kokoto, lakini ukisema pia na kokoto sijui mawe uingize kama hivyo, basi unazidi kutoa maisha magumu kwa wananchi wa Zanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza kwamba gari la mchanga lilikuwa shilingi 100,000/-, sasa ni leo shilingi 200,000/-, gari la shilingi 200,000/- leo shilingi 450,000/- ya shilingi 400,000/- leo shilingi 700,000/-. Hii si tunafanya siasa lakini pia tuna malengo. Sisi wa Chama cha Mapinduzi tunachaguliwa na wananchi, sisi tunawekeza kwa wananchi, inawezekana wataalamu wengine hawana vyama, sisi tunavyo vyama, wananchi wetu wanaumia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawashauri wenzangu suala la mchanga ni lazima tulifikie ufumbuzi pamoja na serikali. Ni kweli kwamba mchanga Zanzibar ni kidogo ni lazima tupange mipango. Lakini hao hao waliokuwa na mashamba wakisimamiwa mchanga utajirejea. Bahati mbaya sasa hivi serikali inachukua mchanga, barabara za kwenda kwenye michanga mbovu, gari zinakatika na hakuna mti mmoja uliopandwa na serikali. Wakati haya mashamba yalipokuwa na kwa hawa watu, wakati mwengine serikali ilikuwa ikipata wageni wazungu wanawapeleka katika mashamba ya watu binafsi kuangalia. Tunafanya nini Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri hili suala ni lazima tulikalie kwa pamoja, Baraza la Wawakilishi lishirikishwe kikamilifu, sisi ndio tumechaguliwa na wananchi, wananchi wanalalamika na wanaisema vibaya serikali yao, hatutaki serikali yetu isemwe. Serikali hii ya Mapinduzi kwa mujibu wa Katiba ipo kwa ajili ya wananchi. Ukisoma katiba kifungu cha 17(a)(b)(c) kinasema hakuna mtu atakayenyang'anywa mali yake. Lakini pia kifungu cha 88 kinatupa sisi mamlaka ya kuisimamia serikali. Wananchi tuisimamie. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumalizia kwa kusema kwamba suala hili la mchanga tusipoliangalia tukaliona dogo, basi litatuumiza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kama juzi na jana nilisikia kwenye redio, baadhi ya wananchi wanaoweka misumari sasa, hiyo ni hatua ya mwanzo, wanaweza kupiga mawe gari, wanaweza kufanya nini, hatutaki tufikie huko. Hetu tukaeni pamoja serikali na wananchi, tena sio waitwe wale wenye mashamba halafu mtu aambiwe anapewa milioni 50 ukapumzike. Wenyewe wametumia wengine milioni 500 kuyaendeleza mashamba yao. Sasa wewe ufikirie kama serikali kwa mwezi mmoja wa Machi Aprili imeweza kukusanya milioni 600, hizo maana yake ni milioni 584, maana yake hao wananchi walikuwa wamewekeza pesa nyingi kwa sababu hiyo biashara inalipa.

Mhe. Mwenyekiti, leo unapowaambia wasipate kitu au uje uwape milioni 20, wengine wana madeni, watoto wao hawaendi skuli wamefukuzwa, wengine bahati nzuri wamekwenda Dahafur nchini Sudan wamepata pesa zao wameziwekeza katika mashamba ya mchanga, leo hii hawana kitu. Mtu jeshi anatembea na bunduki halafu anaona kanyang'anywa mali yake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inakuwaje Mhe. Waziri. Mimi nakuona wewe ni mzoefu, ni mtu mwenye busara na ni mzoefu sana kwenye Bunge umekaa karibu miaka 20, umekuwa Waziri wa Muungano na hapa sasa umekuwa Waziri. Hatutaki Uwaziri wako ukutoke lakini lazima tuwe pamoja tushirikiane na lazima tujue suala la mchanga linamalizika vipi. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani watu wa eneo moja wajione kama sio sehemu ya nchi hii wanyang'anywe chanzo chao cha mapato, wafilisiwe waione serikali ina bughudha, haiwezekani. *(Makofi)*

Mimi naomba kumalizia lakini nasema kwamba lazima Baraza liunde Kamati kufuatilia hili suala. Kwa sababu mimi kama mwenyekiti nilizungumza mpaka na Wakuu wa Mkoa, wao wenyewe wanalalamika kwamba suala hili hawakushirikishwa na linawaumiza. Mhe. Mwenyekiti, sasa kama Wakuu wa Mkoa wanalalamika kwa kamati, maana yake ni nini, maana yake ni kwamba haki haikutendeka. Ni lazima tufanye haki ionekane badala ya kufikiria kwamba ipo haki.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said kwa mchango wako. Ninatumai michango yote mliyoitoa Mhe. Waziri ataifanyia kazi.

Lakini kabla ya kuahirisha kikao tumefikiwa tena na wageni hivi punde wa Mhe. Waziri kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, naomba tuwatambuwe uwepo wao.

Wageni hao ni;

1. Mr. Ali Haji Ramadhani mwakilishi wa *FAO* Zanzibar;
2. *Professor* Mussa Mapusa mshauri katika masuala ya uvuvi. Karibuni sana.(*Makofi*).

Lakini kuna tangazo jengine kutoka kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anawaalika Waheshimiwa Wawakilishi wote katika ufungaji wa tamasha la michezo ya Vyuo Vikuu (*ZARIFA CUP)* leo katika Uwanja wa Amani. Mgeni rasmi katika ufungaji huo ni Mhe. Januari Yussuf Makamba Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Rais Masuala ya Muungano na Mazingira.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa utulivu wenu. Pia nimshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, nawapongeza sana.

Waheshimiwa Wajumbe naomba niahirishe kikao hadi saa 11:00 jioni. Waheshimiwa Wajumbe nawakumbusha saa 11:00 jioni tufike kwa wakati ili tuendelee na michango yetu. Ahsanteni *(Makofi)*

(Saa 6:00 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018
Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana nimesimama kwa kanuni 61 kuhusu utaratibu lakini nakazia kanuni 45 naomba niisome.

"Mjumbe yoyote anaweza kwa kibali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatia mpangilio wa shughuli ambao umewekwa na kanuni ya 27".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika hicho nimesimama kwa kanuni hii kutaka kuweka sawa *Hansard* ndio kusema Mweyekiti uniruhusu kwa sababu hapa nina Hansard yangu ambayo nilichangia 24 wakati wa Wizara ya Elimu sikufahamika *vizuri* na kwa masikitiko kabisa nikajibiwa kama alivyosema mwenzangu kwamba mipasho, lakini naomba ninukuu kipande ambacho Mhe. Waziri alikijibu kwa muono wake.

Mhe. Waziri nitakuomba sana katika hili unisaidie majibu ya kutosha juu ya kadhia, hili suala zima la huu ukarabati wa skuli hususan skuli mpya hizi ambazo zimejengwa hata miaka minne bado au miaka mitano bado, leo hii unatwambia zinakwenda kukarabatiwa ina maana inaonesha wazi kwamba hamkuwa makini katika kuzijenga hata ma-*contract* sikusema kwamba Serikali

sio Makini. *Hansard* yangu hii hapa naomba iende ikachukuliwe irekebishwe, sikusomeka vizuri na tokea jana sina raha katika jambo lile kwa sababu nimezushiwa mambo ambayo sikufanyiwa haki, watu wa mbele walifurahi sana katika hilo naomba kukanusha hilo suala na *Hansard* yangu hii hapa ipo iende ikasomwe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nina *Hansard* ya Mhe. Waziri haina haja kupoteza muda kusoma lakini nimeamua niseme hili ili kujiweka sawa ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naona tumekuelewa na Mawaziri wamekuelewa na *Hansard* itakaa sawa, sasa majadiliano yanaendelea na sasa nimuite Mhe. Shehe Hamad Mattar akifuatiwa na Mhe. Sarahan Said.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami kwa kunipa fursa hii kuwa ni mchangiaji wa mwanzo katika mhula huu wa pili kwa siku ya leo, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na salama na tukaweza kufika hapa na mimi nikiwa mzima nashukuru *Alhamdullillah*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nimpongeze Mhe. Waziri wa Kilimo waziri mahiri ambaye anapenda kujituma sana na kuona kwamba Wizara yake inafanya malengo yaliyokusudiwa, nampongeza sana yeye pamoja na watendaji wake. Aidha niwaombe watendaji wote kwa kusema kuwa kupanga mipango ni sehemu moja. Katika hotuba yake hii nimeona mipango mizuri sana iliyopangwa ambayo kuwa anategemea kuitekeleza lakini tuseme kwamba kupanga ni sehemu moja na kutekeleza ni sehemu nyengine. Ni kusema kwamba nia inashinda matokeo kwa hivyo nia ni sawa sawa na ule mpango lakini matokeo yakawa mabaya lakini ni imani yangu kwamba matokeo nayo yatakuwa mazuri. Hivyo basi watendaji wajitahidi katika kusimamia mipango yote ambayo kuwa imepangwa katika Wizara hii ili tufikie lengo la kujitosheleza kwa chakula na kuongeza mapato ya nchi yeu na kunyanyua uchumi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kwa mfanikio yaliyopatikana kulingana na hotuba ya Mhe. Waziri ya mwaka 2016/2017 walioyatekeleza kwa kweli ni mengi pamoja na changamoto zilizoko lakini ni mengi sana. Mafanikio ambayo yamepatikana hasa pale wanapozungumza kwamba kushirikiana na Taasisi binafsi kwa sababu suala la kilimo linamgusa kila mtu. Niwapongeze sana ile Wizara au taasisi za watu binafsi kama ile ya Kampuni ya *ZAIDI* na *TAHA* ambayo kuwa imeshirikiana na Wizara ya Kilimo kuona kwamba wakulima

wanawajali na wanawasaidia kwa kila hali kwa kueneza na kuhamasisha wataalam wametumia katika taasisi hizi za watu binafsi, vifaa wameweza kutoa na mimi ni shahidi kama hii taasisi ya *TAHA* ambayo kuwa imekuwa ikiwasaidia wakulima jinsi walivyowafaidisha pamoja na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 10 wa hotuba ya Waziri kuhusu ufungaji wa mitambo ya kukamulia alizeti, nimefarijika sana kuona kwamba Mhe. Waziri tayari na sisi wametujali wakulima wa nchi hii kuona kwamba zao la alizetu wamelileta nchini na kulihamasisha liweze kulimwa, karibuni huko nyuma walikuwa wanahamasishwa wakulima lakini walikuwa wanajaribu kulima hawajui ni wapi wakaweza kupeleka mazao haya kwa ajili ya kupata matokeo ya mbegu hizo za alizeti, lakini leo hii nafarijika kuona kwamba wameweza kufunga mitambo hii Unguja na Pemba. Sasa ni jukumu la Waziri kuona kwamba hichi kilimo kinalimwa kwa sababu ndani yake kilimo cha alizeti tunapata faida nyingi, mafuta yake mazuri hayana *cholesterol* lakini kwa upande wa mifugo pia vile vile tunapata mifugo ambaya tunazalisha katika mifugo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika upande wa huduma za mifugo nitakwenda haraka haraka sana. Huduma za mifugo na kinga za tiba ya mifugo, katika sekta hii tumekuwa tukiona mara nyingi sana wafugaji wanavyopoteza mifugo yao kwa msimu ukitokezea hasa mifugo ya kuku, pamoja na jitihada zote zinazopatikana lakini bado wakulima wanapoteza asilimia kubwa sana ya mifugo hii ya kuku. Kwa kweli wafugaji wanapata hasara ikifika msimu kiasi kwamba wanakata tamaa mpaka hata mabanda yenyewe huweza kuona kwamba hakuna haja ya kufanya mradi huu. Kwa hivyo tatizo hili ni kubwa sana kwa wananchi naomba sana watafiti na wataalam waendelee kutafuta ni jambo gani ukifika msimu kama huu linaathiri wananchi na wananchi hatimae wafaidike katika suala la ufugaji.

Lakini vile vile katika suala hilo hilo la ufugaji Mhe. Waziri kuna matatizo ambayo kuwa yanajitokeza ya wadudu wale wa mazao haya na matunda, mara nyingi sana tumekuwa tukiona matunda yetu yanazaliwa kwa wingi lakini hutokezea wadudu hawa wanaharibu matunda haya, wakati mwengine hutokezea msimu ikawa dawa inapatikana wakati mwengine haipatikani kwa kweli inarudisha nyuma juhudi za wananchi. Ni imani yangu kwamba na naomba sana Mhe. Waziri jambo hili la suala la dawa ya matibabu ya matunda kama haya utakuta maembe, papai, machungwa yote yanaharibika unaweza ukawa na miti imejaza matunda lakini hufaidiki nayo ni hasara. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri katika mipango yake suala la utibabu wa matunda kama haya nayo yapatikane.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa pale aliposema kwamba tayari ameweza kununua matrekta mpango wa ahadi kununua matrekta 20 yenye thamani ya Dola 540,827,000 za Kimarekani kwa kampuni ya Mahendra, hichi kilikuwa ni kilio cha wananchi kuona kwamba matrekta Zanzibar bado ni kidogo haiwezekani kwamba Wilaya nzima kuwe na trekta moja. Ni imani yangu kwamba kuwepo kwa matrekta haya na hasa kwa vile sasa kuna wakala, umeanzishwa wakala huu wa matrekta kwamba suala la kilimo kutumia matrekta huenda likapungua japo kuwa halitatosheleza lakini tutaweza kuanzia hapo kulingana na uchumi wetu. Nashauri sana Mhe. Mwenyekiti, afanye juhudi kubwa sana Mhe. Waziri kutoa elimu ya kilimo hichi cha mpunga ambachokuwa kinatumia maji kidogo na mbegu kidogo lakini uzalishaji mkubwa ukulima huu kwa vile matrekta tumeshakuwa nayo hayo sasa tuone tutafanya vipi tuweze kupiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri sana ili tufikie lengo letu tulilojipangia kwenye upande wa Kilimo ni vyema kuanzisha taasisi ya kilimo, hapa si kuanzisha lakini kuipa nguvu hii taasisi ya kilimo, taasisi ya kilimo ipo na ilianzishwa tokea mwaka 2011 lakini la kusikitisha taasisi hii haikupewa ruzuku katika hotuba hii nayo ni ngumu ndio chimbuko. Sasa nawashauri sana tena ina hata sheria yake lakini haina zuruku. Nashauri sana Taasisi hii imegewe fedha kutoka taasisi ya mifugo kwenye milioni mia tano na nusu yake milioni mia mbili na hamsini angalau zipelekwe kwenye taasisi hii ya kilimo nashauri sana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la kilimo ninakuomba sana Mhe. Waziri, uiwezeshe taasisi hii ya kilimo ya Kizimbani pamoja na mipango uliyopanga hii lakini hii taasisi ya kilimo Kizimbani ni muhimu sana kwa suala la utafiti, uiwezeshe kwa kuipatia maabara na vitendea kazi vya maabara ambavyo kuwa tutaweza kufanya utafiti wa udongo ni aina gani tuweze kuutumia kwa mazao gani. Kwani sisa hivi tunakuwa tunabahatisha wenzetu Kenya hapo hawawezi kulima hata kile kitunguu kama hawajajua udongo unahitaji nini na umezidi kitu gani. Kwa hivyo ni vyema sana Mhe. Waziri Kizimbani napo ni roho yetu ile pale uipe nguvu kwa kuipa vitendea kazi.

Sasa niende katika suala zima la mapato, mapato ndio msingi wa hii bajeti yote hii na kila Wizara imepangiwa iweze kutoa mapato katika kuchangia mfuko mkuu wa Serikali, nimeona hapa Wizara imepangiwa bilioni 4.9 hii ni kutoka kwenye vianzio vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka 2017/2018. Nashauri sana ili hili lengo lifikiwe na tuweze kutekeleza bajeti yetu hii tunayoitumia basi kwa kusimamia vyanzo vya mapato, kwa sababu nasema

hivyo imekuwa ikisemekana na kuonekana kwamba baadhi ya sehemu za mapato zinakuwa haziko vizuri kwa mfano eneo la Jozani pale pana sehemu ya kituo cha mapato ya misitu, lakini leo hii unweza kufika saa moja mhusika wa pale hajafika hili ni kero wakati mazao ya misitu inatakiwa saa 12 watu waweze kufanya usafirishaji mpaka 12 jioni. Lakini leo utakuta kwamba saa moja hajafika.

Lakini jambo jengine baadhi yao wanawekwa pale hata kuandika yale mahesabu hawaelewi Mhe. Waziri jambo hili lisimamie vizuri sana na kupelekea kuchelewa kwa hawa makarani wanaoshughulika na mapato zile gari za mashamba zinazotoka pale zinafikia kulundikana kwa wingi, matokeo yake madereva wale waliopanda gari zile zenye mzigo wanatoka wanaingia katika gari nyengine. Sasa wakipata huduma matokeo yake sasa wanaanza kufukuzana kiasi ambacho wanahatarisha amani ya raia wetu. Kwa hivyo nashauri sana maeneo kama haya kuweka watu makini ambao kuwa wanaweza kujua wakati wa kufanya kazi na kuondoka kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala jengine la mapato ambalo kuwa nakushauri sana tunaweza kufaidika kwa suala la mapato na maendeleo ya uvuvi na hifadhi ya bahari, Mhe. Mwenyekiti, namshauri sana eneo la Matumbilini kule Pemba kuna sememu inaitwa kwa Jundo ni eneo linalohitaji kufanyiwa utafiti kwa uzalishaji wa samaki na rasilimali nyengine za bahari, hili ni kianzio cha mapato, ni eneo la ndani lenye ufukwe wa utalii pia kwa ufugaji wa pweza na mambo mengine ambayo yanaambatana na bahari. Ni sehemu ambayo ina mto mrefu mzuri kwa kuhifadhi. Kwa hivyo namshauri sana Mhe. Waziri aende katika maeneo hayo kama hajawahi kufika na yeye aende akaone kwamba ni vipi tutaweza kupata mapato pale na kuweza kutunza bahari yetu kufaidika nayo.

Pia kwenye suala la mapato niende kwenye Kisiwa cha Misali, Mhe. Waziri naomba utakapokuja utueleze Baraza hili kwamba ni vipi tunafaidika na sehemu ile pale, siku zote inapigiwa kelele ni sehemu yenye samaki wengi ina mambo mengi lakini tunafaidika vipi sisi kwa sababu kuna tetezi sana, kuna watu eneo hili wanalitumia kwa kujinufaisha wenyewe wanakwenda pale wavuvi wanazungumza mazungumzo yao wanaruhusiwa na baadae wanavua samaki wale kwa faida yao ile hifadhi inapatikana. Lakini kama hiyo haitoshi tujiulize kule chini tumefanya utafiti gani, hebu tujiulize kwa nini wenzetu watalii kila siku wanakuja wanataka kwenda kule chini tunajua wanaondoka na kitu gani. Kwa hivyo ni vyema na sisi wenyewe tujiridhishe kuna rasimali gani ambayo itaweza kutusaidia katika nchi yetu Mhe. Waziri hilo ni jambo nalo nakuomba sana kujua kwamba tafiti hii ya eneo la Misali inashughulikiwa

vizuri ipasavyo. Kwa sababu tusiseme kwamba hatuna mapato lakini mapato tunayo lakini wenyewe hatuyaungi mkono katika kuyatafuta.

Mwisho kwa ufupi sana Mhe. Waziri katika kitabu hichi cha hotuba yako nimeona jambo moja ambalo nalishauri sana sijaliona katika upande wa mifugo, ufugaji wa sungura ni ufugaji rahisi sana lakini bado hatujaupa nguvu hichi ni kitoweleo kizuri kwa watalii wetu kwanza ni nyama laini ambayo kuwa hata wale madaktari katika nyama ambazo wanatushauri tule ni miongoni mwa kama hizi tuache kula nyama nyekundu. Kwa hivyo hapa tukiwa tunafuga sungura tunaweza kutengeneza ajira kwa vijana wetu, kuna sungura aina mbali mbali ambazo nimeziona mimi katika tafiti zangu nashauri sana na wewe uzifuatilie utaziona umuhimu wake.

Kuna sungura wa kisasa hawa wanaitwa East Africa hawa ukiweza kufuga sungura ishirini tu kwa maeneo ya fupi utakuta unazalisha kwa wingi sana, kwa hivyo vijana wanaweza kuanza kwa sungura 20 na wataalam tunaweza kuwapata hapo Tanzania bara kwa eneo dogo na tukaweza kuzalisha na wananchi wakajitengenezea ajira, kuna aina ya sungura kama California White, American White, Island White na Dachi. Hawa ni aina ya sungura ambao kuwa uzalishaji wake ni mzuri tena wa fedha nyingi sana, kwa hivyo nashauri sana Mhe. Waziri hili jambo ulichukue na ulione kwamba lina umuhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi sina mengi mengi yameshazungumzwa sitaki niyarudie ili naunga mkono hoja hii mia kwa mia na nawaomba Waheshimiwa wenzangu tuiunge mkono hotuba hii kwa nguvu zetu zote iliaweze kutekeleza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamad Mattar kwa mchango wako sasa namuita Mhe. Omar Seif Abeid, baada yake atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa, na Mhe. Makame Said Juma wa Kojani ajitayarishe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maliasili. Awali ya yote hayo mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kutujaalia tukakutana hapa jioni hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefarajika sana na hotuba hii ya Mhe. Waziri, aliyoiwasilisha hapa nikiwa na imani kubwa kwamba yale yaliomo katika Hotuba hii ndio yatakayotekelezwa, kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kawaida huwa nasoma hivi vitabu vyote, lakini hichi sitaki kusoma kwa sababu sitaki kusoma nimeona yale yaliyomo, humu kwenye hichi kitabu ni mambo ambayo nakubaliana nayo, lakini baada ya hayo kuna mambo ambayo mimi nataka niyazungumze ambayo nimeyaona na moja kwa moja mimi nitajikita, katika nitaaza kuichambuka ile Hotuba ya Bajeti ya Mwaka jana ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Amina Salum Ali, katika ukurasa wake wa 48 ibara ya 117 alipoizungumzia kwa kina zao la karafuu. Mhe. Mwenyekiti ukweli usiopingika kwamba zao la karafuu katika nchi yetu ni uti wa mgongo sote tunafahamu hivyo, na hakuna miongoni mwetu yoyote atakayeweza kubisha juu ya jambo hili.

Juhudi kubwa imechukuliwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na shukurani za pekee zimuendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kutoa asilimia 80% ya bei ya karafuu katika soko la Dunia kuirejesha kwa wananchi ni faraja kubwa, ni jambo la kupigiwa mfano. Mwenyezi Mungu ampe hekma, busara na nguvu aweze kuendelea kutuongoza kwa ajili ya manufaa ya watu wetu. Lakini pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo. Waziri wa Kilimo mpango kazi wake, mimi nakubaliana nao sana kwa sababu katika uchangiaji wangu mie mwingi, nilikuwa nazungumzia zao la karafuu, nilikuwa nikizungumzia baadhi ya matatizo, lakini chakufurahisha ni kwamba kuna siku nilimchukua mimi mwenyewe kama Shekh Mussa aliposema alimchukua Waziri wa Elimu akenda naye, lakini na mie nimemchukua Waziri wa Kilimo nikaenda naye mpaka shambani nikenda nikamuonesha nikamwambia Mhe. Waziri tunakuchangia katika Baraza kuhusu zao la karafuu njoo uone tofauti iliyopo.*(Makofi)*

Mhe. Waziri akanikubalia akenda shamba akenda akaona na akajionea yeye mwenyewe jinsi ya mikarafuu ilivyo, lakini pamoja na mambo mazuri na changamoto zipo nyingi, changamoto kubwa inayoikabili zao hili ni pale ambapo mashamba mengi ya Serikali ya mikarafuu ya Serikali yanapobakia Serikalini. Mimi naiomba Wizara naiomba Serikali ichukuwe hatua za makusudi kwa yale mashamba ambayo hivi sasa yapo chini ya Wizara ya Kilimo, yafanye bidii ya kuyarejesha kwa wananchi, nakuomba sana Mhe. Waziri kwenye msimu huu wa kukondisha mashamba ya karafuu kwamba muwakodishe watu mashamba ya mikarafuu kwa mkataba maalum sio kwa ajili ya kuchuma tu bali ya kuyafyekeya, kuyasafisha sisi huyu ndio ng'ombe wetu wa maziwa siku zote nazungumza kiswahili hichi na lugha hii.

Lakini leo tuna tabia ya kumkama tu, bila ya kumuhudumia mwisho tutamtoa damu na hatima yake ng'ombe atakufa. Ni wajibu wetu sasa kwa pamoja

tukamchunga tukampa matunzo mazuri, matunzo mazuri ya shamba hizi ni kuzirejesha pia kuwakabidhi wananchi wakapanda. Leo tumeshuhudia msimu wa 2015/16 na 2016/17 tuliweka lengo la tani 4,200 tukafika mpaka tani 5,700 za karafuu, mimi ningependa nijue katika miaka minne au mitatu hii, kabla ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein mmejipangaje Wizara ya Kilimo naomba jibu kwamba itakapofika 2020 muna uwezo angalau wa kufikisha tani 10,000 za karafuu. Uwezo huo upo ikiwa tutakubaliana na mpango kazi ambao Mhe. Waziri umeuelekeza kwenye Bajeti yako, kwenye Kitabu hichi.

Mhe. Kuhusu mashamba ya Serikali ya Wizara ya Kilimo, hasa yale ya Makuwe hasa Kinyasini, Mtamwe na Daya, yale ni mashamba yalikuwa nitegemezi. Leo haiwezekani kwamba mashamba yale pamoja na fedha nyingi inayochangia yakawa yapo bado ndani ya pori, hebu tujiulize kwa sababu gani mashamba yale yako ndani ya pori mpaka leo wakati yanakodishwa kwa pesa nyingi au Waziri utakapokuja uniambie mashamba yale ni sababu gani ikawa mpaka leo, yameshindwa kupandwa mikarafuu mengine kwa hivyo tukafanya *replacement* ya ile mikarafuu ambayo imekufa, wakati sisi wenyewe nyinyi Wizara ya Kilimo mnatoa miche, mnawapa wakulima lakini nyinyi mmeshindwa kupanda mikarafuu mengine mipya. Ushauri wangu ni kwamba mbakishe mashamba kidogo muweze kuyahudumia na yale yaliyosalia, yale yalikuwa ya eka tatu muwape wananchi kwa masharti, kwa lengo kwamba ndani ya miaka miwili au miaka mitatu mnawasimamia.

Sipendi kuwalaumu napenda kuwapongeza sana lakini mimi najua tatizo linalosababisha moja ni uchache wa wafanyakazi mashamba ni mengi ya Serikali lakini wafanyakazi ni kidogo, haiwezekani kwamba wafanyakazi ishirini au thalathini waweze kumudu kuhudumia mashamba elfu tatu au elfu nne, naomba munieleze mmejipangaje juu ya suala hili, la kupata wafanyakazi ambao wataweza kuyahudumia mashamba yale. Lakini pia Mheshimiwa narudia tena kwamba miche ya mikarafuu ambayo inazalishwa katika vitalu vyenu, haijafikia ubora wa kupanda Mwenyezi Mungu katujaalia mwaka huu tumepata mvua nyingi, ambayo ni nzuri kwa kupandia mikarafuu, naomba sana suala la kuwashajihisha wakulima au nyinyi wizara kutumia miche ya mibotea ambayo imo mashambani inangolewa na wakulima, muyape kipa umbele kulikoni miche ambayo mnaifanya nyie kuizalisha, katika vitalu nyenu. Au hata kama mtazalisha katika vitalu muhakikishe kwamba miche munayoilewa katika vitalu vyenu ni miche ile tu ambayo mnaingowa kutoka mashambani na baadae munaiweka katika vitalu.

Lakini kwa wenzetu kule Tanzania Bara wana Benki maalum ya kuwasaidia wakulima, zamani ile CRDB ilikuwa ikitwa Benki ya Ushirika na Maendeleo

Vijijini, naomba Mhe. Waziri hebu nieleze hii karafuu sisi ndio zao letu kubwa, iwapo tutajipanga vizuri tunaweza kufikisha hata tani elfu kumi na mbili, nyinyi mna mpango gani wa kuvishajihisha taasisi za fedha kuweza kuwekeza fedha zao kwa wakulima wa karafuu huku Visiwani, nakuomba suala hili kama unalo ulifanyie bidii na kama hunalo nakuomba wewe ni mbunifu wa mambo buni kuzishajihisha taasisi za kifedha, zikaweza kutoa mikopo kwa wakulima wa zao la karafuu. Jambo hili litatusaidia sana sisi katika kuendeleza na kukuza kilimo cha karafuu ambapo, Serikali yetu itapata mafao mengi.

Jambo jengine, Mhe. nataka nitoke hapa nishaeleza kidogo kabla sijapigiwa kengele nilikuwa nachangia kuhusu mpango mzima wa Wizara yako, juu ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki, mpango huu Mhe. Waziri ni mpango mzuri iwapo utakuwa pia na usimamizi madhubuti, nataka nijue, kuhusu mpango huu wataalamu wako wamejipangaje kuweza kuwasaidia wakulima wetu, au wavuvi wetu ambao watafuga samaki hawa. Mwenzangu Mhe. Rashid amesema hapendi kuita vifaranga alipenda kusema kama samaki wadogo. Anasema vifaranga ni vya kuku samaki wanakuwa wadogo nakubaliana na yeye ni mwalimu hili litasaidia kuongeza pato kubwa kwa wananchi wetu. Kama tunavyojua sisi Zanzibar, Unguja na Pemba ni Visiwa ambavyo vimezungukwa na baharí na asilimia kubwa ya watu wetu ni wavuvi. Serikali ina mpango umeeleza hapa kwamba mna mpango wa kununua Meli ya uvuvi, Kampuni ya Uvuvi ipo lakini hii itakuwa ni nzuri zaidi, mimi nakwambia kama tutafanikiwa kuliko hata hizo meli. Maeneo ya kufuga kwa Unguja na Pemba tunayo mengi tukiwaeka watu wetu wakiwawezesha wanaweza wakafanya vitu vizuri, vikaleta tija Serikali ikafaidika, na wananchi wenyewe wakapata maendeleo makubwa. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nina jambo moja ambalo pia nataka kulichangia kuhusiana na Idara ya Misitu, Mheshimiwa ni jambo la kusikitisha na naiomba Serikali liliangalie sana, sisi tunapiga marufuku matumizi ya msumeno wa moto, tunakubaliana sote kwamba misumeno ya moto inaharibu kabisa mazingira, lakini kwa nini misumeno hii ya moto tunairuhusu kuingia nchini, na badala yake watu wakianza kuitumia tunaichukua wananchi tunawazuia tunawanyanganya misumeno kwa nini tusiizue misumeno hii wakati wa kuingia, ilikuwa ni busara ni busara zaidi lau kama tungezuia na tukapiga maarufu kuingiza misumeno ya moto hapa nchini kulikoni kuwanyanganya wananchi wakati wameshainunua, wameshatoa pesa zao kununua wameshatoa pesa zao kununua misumeno hiyo. Utakapokuja Mhe. Waziri, naomba uniambie toka zoezi la ukamataji wa misumeno kwa Unguja na Pemba tumekamata misumeno mingapi kwa Unguja na misumeno mingapi kwa

Pemba na mingapi tumeichoma, mingapi imeteketezwa ningeomba nijue na mengine iko wapi.

Ni jambo la kusikitisha kwamba tunachoma, tunakamata misumeno mingi lakini kuna tetezi kwamba misumeno hii inapotea mengine wanarudishiwa watu vile vile, inaendelea na kadhia inaendelea. Naomba nijue ni idadi gani ya misumeno ambayo imekamatwa mingapi, imechomwa Unguja, mingapi imechomwa Pemba na mingapi ipo na iko wapi? Ni busara, wito wangu kwamba tusijiingize kwenye mambo ambayo hayatatuletea tija kwa wananchi wetu, tumeamua hatutaki kutumia misumeno ya moto hapa, vizuri tuipige maarufu isiingie kabisa nchini, hii itakuwa ni suluhisho peke yake la kudumu.

Mhe. nikija sasa kadhia nzima ya mchanga, ambayo imezungumzwa na wenzangu mimi nakubaliana na wazo zuri la Serikali la kudhibiti mchanga sisi kama visiwa kila kitu kinataka utaratibu, hata kula chakula chako wewe mwenyewe unakipika lakini ukikosea utaratibu wa kula kinakudhuru. Kwa hiyo ni vizuri kuwa na utaratibu wa matumizi ya mchanga lakini kuna tatizo moja limezungumzwa na mimi nataka kulichangia kwamba kwa nini Serikali haikuongeza bei ya mchanga, lakini wenye kufanya biashara ya mchanga wanawauzia bei kubwa zaidi wananchi kulikoni kwa nini?

Naiomba Serikali sana kwa hili Mheshimiwa, isilifumbie macho jambo hili litaleta matatizo kwa wananchi wetu, wanyonge wanategemea kujenga uwezo wao mdogo leo gari iliyokuwa ikinunuwa elfu sabiini kama kuuzwa laki moja na nusu, kama Mhe. Machano alivyosema, lakini suala la ardhi mimi nasema Serikali ndio yeye mamlaka ya ardhi. Serikali ina mamlaka peke yake ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi kwamba Serikali ndio yenye mamlaka ya kuchukua ardhi pale inapoona iko haja ya kufanya hivyo, lakini utaratibu ukiwa kuna miti au kuna nini watu wanalipwa fidia hilo mimi naomba kama kuna wananchi, ambao hawakulipwa fidia kwenye maeneo yao, wende Serikali ifanye bidii iwalipe, kwa sababu ile ni haki yako. Kwa nini wawekezaji wanapoekeza wanalipa fidia, kwa wananchi na sisi kama Serikali wakati Wizara inapata mapato ilipe fidia si tatizo. Lakini sikusema kwamba ardhi zile zilikuwa na wenyewe, ardhi yote ni mali ya Serikali mimi nakubaliana na hayo. *(Makofi)*

Natoa wito kwa wizara na pia natowa wito kwa jamii kujua kwamba matumizi ya mchanga kwa utaratibu uliowekwa, ni utaratibu mzuri ambao Serikali mimi siamini kama ina nia mbaya imani yangu kwamba Serikali ina nia nzuri ya kuiweka nchi yetu katika mazingira mazuri, lakini ni wajibu wetu kwa pamoja kukubaliana utaratibu gani tuutumie kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Mhe.

Waziri mimi nitakapokuja nitarudi tena kwenye karafuu, nataka unambie Makadirio yako mwaka huu, kwenye karafuu unategemea kuchuma tani ngapi za karafuu, kwa sababu nasikia msimu wa kukodisha tayari umefika ili hii tukiijua itatupa mwangaza tunakokwenda, kwamba vipi tudhibiti mali yetu tuliyonayo. Tani ngapi za karafuu unategemea kuzichuma,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe Omar Seif Abeid malizia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Dakika mbili au tatu niongeze Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. nakuomba umalizie.

Mhe. Omar Seif Abeid: Uniambie makisio yako uliyoyafanya na nini matengemeo ya kuwasaidia wale wananchi kama nilivyokuuliza mwanzo juu ya suala hili la karafuu. Mhe. kwa heshima na taadhima natamka kwamba nimeunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100%. Ahsante sana Mhe.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako, sasa naomba nimwite nimemtaja Mhe. Asha, sasa naomba nimwite Mhe. Makame Said Juma akifuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti na mimi pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi kuchangia japo kidogo katika Wizara hii ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa ujasiri wake na uhodari wake, ambao kuwa anautumia katika kazi yake hii ya Uwaziri. Mhe. Mwenyekiti kwanza simsifu tu kwa sababu kama Waziri, namsifu kwa utendaji ambao kuwa anao, kwa sababu nimemuona katika njia zake anazokwenda, anakwenda kama vile si mpinzani, anakwenda kama yeye ni mtekelezaji mkuu wa Sera za Chama cha Mapinduzi. Nimpongeze sana hilo, kwa sababu anatumia ujasiri mkubwa, tena anafuatilia kazi zake vizuri sana, kwa hivyo lazima nimpongeze Mhe. Rais hapa aliona hakukosea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mchango wangu ambao utakuwa mdogo nitaanza kwenye upungufu wa samaki. Mhe. Waziri wameligusia sana jambo hili ambalo kuwa nchi yetu imekubwa sana na upungufu wa samaki. Kitu kikubwa hapa alichoona yeye kama ni mazingira ambayo kuwa sasa hivi yamebadilika. Mimi kwa muono wangu naona Mhe. Waziri ajue tu kama samaki ni sawa sawa kama mazao ya kilimo yaliyo juu ya ardhi, yanaendana na

miongo, yanaendana na msimu nayo pia yanaendana na mvua. Kwa sababu hata jua likiwa kali samaki pia huwa wanaadimika. Hata jua hilo au kama atakuwa na wasiwasi huo niangalie mwaka huu. Mwaka huu tunatamaa samaki watakuwa wengi sana, kuliko miaka mengine miwili mitatu iliyopita. Kwa sababu tayari samaki wanaanza kuonekana madagaa na dalili ya mwanzo ni kuwa watoto, wakishakuwa wale watoto badala yake kunakuwa na watu wazima. Kwa hivyo tayari dalili tunayo.

Mhe. Mwenyekiti, asifikirie sana kama samaki hawa wana upungufu kwa sababu wanakamatwa sana, bali hata ni mandhari yalivyo, hali ilivyo, na hali ya mazingira ya bahari kwa mwenendo unavyokwenda katika mwaka. Utakuta safari hii wamepungua samaki fulani kwa mazingira fulani, lakini pia watakuja samaki wengine kwa mazingira mengine ambayo kuwa yanafahamika katika masuala ya kibahari.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tetesi sana ambazo zinatusumbua wavuvi nao ni uchafuzi za mazingira. Sisi wavuvi tunajiuliza tunachafua vipi kwa sababu tukivua maji madogo ni uchafuzi wa mazingira, lakini tunasema hatuwezi kumsomesha mtoto bila ya kuingia kwenye maji madogo. Hatuwezi kumfundisha mtu uvuvi bila ya kuanza padogo, hatuwezi kumfundisha mtu kuogelea kwa bahari kuu. Hili ni lazima tuwe nalo, tuanze chini tuelekee juu kama vile tunavyoaanza elimu. Elimu tunaanzia chini tunakwenda juu na uvuvi tunakwenda hivyo hivyo, tunaanza na udogo mpaka tunafikia pakubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niishukuru tena serikali kwa kuona uboreshaji huu wa wavuvi kwa kuleta meli zetu za uvuvi au meli zitakazokuja za uvuvi. Lakini nina wasi wasi kidogo, nakumbuka mwaka 1995 vilikuja vyombo vya uvuvi wakapewa watu, maboti yale yalikuwa na majina tofauti, changu, chewa na mengineyo. Nimekumbukia boti vile zilikufa bila ya shahada, hazikutambulikana faida, hazikutambulikana hasara bali tumefikia hatua boti zile zimepotea kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, na mara hii ndiyo hiyo tena imekuja meli na meli hii namuomba Mhe. Waziri anijibu vizuri kwani nina wasiwasi kama meli hii itakuwa ni uchumi wa watu, wale wavuvi hawatofaidika kwa dalili ninayoiona. Nimeona dalili kuwa meli hii itakuja na wageni, maana itakuja na waalam. Sijui wataalamu hawa watatoka China au watatoka Korea, lakini naona ni wataalamu ambao sifikiria kama watatusaidia katika nchi yetu. Mara nyingi sana wataalamu wanatizama taaluma zao, hawatizami taaluma za mazingira.

Sasa ningeomba tu Mhe. Waziri na yeye kasema hapa kama kwamba lazima kutakuwa na wavuvi fulani lakini nina wasiwasi kutakuwa na watu fulani hakutakuwa na wavuvi fulani. Kwa sababu mara nyingi sana panapo mambo haya ya usomi wanachaguliwa wasomi na msomi sio mtu anayevua, mvuvi ni mtu aliyekuwa anajua kuvua tu sio msomi. Kwa sababu msomi sifikirii kama yeye atavua lakini watachaguliwa wasomi. Nakumbukia hapa kama hata meli zetu hizi za Tanzania au za Afrika mara nyingi sana wanachaguliwa ambao ni wasomi sio wapiga mbizi wala sio wazamiaji wala sio waokozi, lakini wanachaguliwa watu wa elimu zao hata ikifika wakati wa matatizo hawajui tufanye nini, hawajui tuwaokoe vipi wala tufanye nini. Wao wanajua wakati mimi nimepewa jezi ina nanga hapa atajua kama mimi tayari ni mtaalamu wa bahari, lakini hata ukimuuliza katika mle katika vyombo. Maana tunajaribu kuwauliza wewe fani ya bahari umeipata wapi, atasema kwamba mimi fani ya uvuvi nimeipata kwa kujua jua tu nimejifundisha hivi hivi, kwa hivyo najua kuogelea, lakini ziwezi kujua vyengine.

Nina wasiwasi kama meli yetu hii au meli zetu hizi za uvuvi itafika wakati zitakufa nazo bila ya shahada. Kwa sababu sifikirii kama watapewa wavuvi ambao wanaweza kufanya kazi zile au watapelekwa watu ambao watachukuwa mafunzo wataweza kuwaelimisha wenzao. Bali watabakia pale, wataalamu wale wataondoka meli zile zishakufa na watu hawakupata faida ya aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nimuomba Mhe. Waziri mara nyingi sana ukichagua wavuvi tafuta eneo lililokuwa lina wavuvi usichague eneo ambalo lina wasomi wa uvuvi. Kwa sababu kuna wasomi wa uvuvi hata ukiwaangusha kwenye maji ni msomi tu, lakini hana elimu ya kuwa mimi nakwenda kuvua. Hana elimu ya kuwa samaki yule nakwenda kumshika vipi, kwa sababu kila samaki ana mazingira yake ya kumkamata siyo samaki ni samaki tu kama huyu ni chewa ni chewa tu. Lakini kila samaki ana ujanja wake namna gani vya kumshika na namna gani ya kumvua na sehemu gani yupo. Kama hujui hivyo unaweza ukapata tabu katika bahari unakenda kila siku lakini hujui samaki yupo sehemu gani na hujui sehemu gani anakaa samaki fulani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alizungumzia hapa katika kitabu chake katika kuboresha uvuvi katika nchi yetu akazungumzia uuzaji wa samaki katika nchi za nje kutoka nchini kwetu. Nikitaka kujua tu ni samaki gani bora ambaye katika nchi yetu ana sifa ya kupelekwa nchi nyengine ili na sisi tujipange. Tunapojua kama samaki fulani ndiye anayependwa basi tujue pa kuelekea maana tunakuwa tunajua kama samaki fulani yupo sehemu fulani. Ukiona hivyo katika mizunguko ya bahari basi utamkuta sakamaki aliyekuwepo upande wa magharibi ni tofauti na aliyekuwepo upande wa Mashariki katika

bahari ya Hindi. Tofauti hata ladha yake ya kula, kama hujui hivyo wewe utasema kama kolekole ni kolekole tu au changu ni changu tu. Lakini hata dalili kila mmoja anaishi katika mazingira yake kama vile mwanadamu walivyokuwa katika mazingira yao wanavyoishi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa alizungumzia sana masuala ya kilimo, ufugaji na mambo mengineyo. Mimi nawapa pole sana wafugaji katika ukanda wa Mashariki Pemba, wamepata matatizo sana ya kufiwa na wanyama wao hasa ng'ombe. Ukanda wa Mashariki Pemba katika ukanda wenye ukame nasema ni ukanda unaoongoza. Mwaka huu wamepata hasara kubwa sana sijui Mhe. Waziri atakwenda kuwaona ili na wao angalau wajione kama sisi wafugaji tunaonekana au laa atabaki na kumbukumbu zake tu kwamba na miye najua kama ukame umetokea. Nakumbuka aliyekuwa na ng'ombe 10 wamebaki wawili, hususan walianza kuangamia tokewa wakati kuna jua mpaka iliponyesha mvua wakazidi kupotea. Ng'ombe utamuona ameishi katika wakati wa jua hata akipata mvua tu basi tayari anaathirika baridi inamzidi na anakufa. Kipindi hichi cha mwanzo wa mvua waliathirika sana ng'ombe hawa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ipo haja Mhe. Waziri na yeye kuchukua hatua kwenda kuwaona wafugaji wale hususan katika maeneo ya mashariki hususan Kojani ndipo anapopajua zaidi. Kwa sababu nakumbuka kama hata mfugaji mmoja alikuja akanililia akanambia nifanye nini miradi yangu imeshakufa sijui vya kufanya. Lakini nikamwambia Mungu ndiye atakayetoa. Lakini Mungu hatoi na wewe ujitangaze kama namuomba Mungu. Sasa tunawaombea wafugaji hao na wao waonekane kama vile wanavyoonekana wafugaji wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika suala moja ambalo limezungumziwa na Mhe. Waziri upungufu wa mazao ya kilimo kwa mwaka huu hususan kwa kwetu Pemba, kesho kutwa tuna mtihani au tunaanza kufunga Ramadhani na mwaka huu mvua zilivyokuwa zinanyesha zimeleta ukame sana au uharibifu wa chakula cha muhogo, umeoza vibaya sana na sijui kama haitofika hatua ya uagizia nje futari hii kwa mwaka huu. Kwa sababu mazao hayo yameharibika sana, ipo haja Mhe. Waziri achukue hatua nayo pia ende akawaone wakulima wetu wa mihogo. Sasa hivi ni tatizo sana ambacho ni chakula chetu muhimu katika mwezi wa Ramadhani katika futari kwa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata taarifa moja hapa juu ya ukulima wa mwani. Ukulima wa mwani nao pia kwa miaka mitatu hii liyopita imekuwa ni changamoto sana. Wenzetu wakulima wa mwani wanapata mitihani kila mwani unaopanda unatokewa na mazingira magumu na unakufa. Si sababu nyengine

bali ukame wa jua, ulikuwa mkubwa hata katika bahari unaingia yale mashamba yote yameharibika kwa jua.

Ninawaomba wenzangu wakulima wa mwani wasivunjike moyo mwaka huu mvua zimenyesha. Wasubiri tu maji baridi yakimaliza katika maeneo yao basi kama serikali ina mbegu iwatafutie ili iwape wajiimarishe tena, tuna tamaa mwaka huu itakuwa ni mfano. Waombe bei tu ipande ili na wao wafaidike kwa miaka mengine itakayokuja.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika upandaji wa mikoko, nayo safari hii ukame umezidi sana, miti yetu ya mikoko mwaka huu ina upungufu mkubwa sana. na sababu ya upungufu ni lilie jua. Usione kama ipo baharini ukafikiri kama nayo inapona kwa sababu ya maji ya bahari yanaingia kila wakati. Hii nayo ni lazima ipate maji ya mvua, ikikosa maji ya mvua basi nayo inaathirika vibaya sana. Aliyekuwa hajui hivyo anasema kama ile miti wakati ipo kwenye bahari inapata maji yake ya kawaida tu. Lakini kama ataiangalia basi ikifika wakati wa kiangazi inapata tabu sana mpaka majani yake yanabadilika. Kama kipindi hichi akenda utaiona basi ataona kweli imenawirika na sasa hivi iko vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita serikali ilihamasisha sana upandaji wa mikoko au mikandaa lakini iliathirika kiasi. Pia ni kusema tu Mhe. Waziri asivunjike moyo kuwahamasisha wale watu ili waendelee na wakati, mwaka huu mvua zimekuwa nzuri inaweza ikatusaidia tunaweza tukabahatika mazao yetu yale yakawa tukafaidika baada ya miaka mitano itakayokuja. Mti wa mkoko ni mti ambao unakuwa haraka zaidi kuliko miti mengine iliyokuwepo juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu natumaini ni mdogo tu lakini pamoja na hayo nimpongeze tena Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ili aendeleze juhudi yake nzuri, na nimuombe tu Mhe. Waziri kuna kipindi kimoja aliwafuata wavuvi ili kupata ushauri ili kutoa maelekezo kwa wavuvi wale. Mhe. Waziri alipata msuko suko mkubwa sana siku hiyo kwa wavuvi wangu, pamoja na mapana yake aliyokwenda nayo kujipanua, kujidai kwamba leo nakwenda kukutana na wavuvi matokeo yake alipata changamoto.

Mhe. Waziri, lakini usihofu wale ni watoto wako aliowafundisha kipindi kile wakati wapo chama kimoja, sasa malezi yale bado wanayo na nimeshazungumza nao na waliniomba kama iko siku tunakuomba tena ukamuombe ingawa nikasema sendi kwa sababu namuogopa kuja kwenda tena mkarudia tena. Lakini Mhe. Waziri nasaha walizotoa wanakuomba radhi,

uwasamehe na Ishallanlla ukenda tena watakupokea vizuri na watataka ushauri wako.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namuunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Makame Saidi Juma wa Jimbo la Kojani kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi wa Jang'ombe akifuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abduliwakil na Mhe. Shaib Said Ali ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti kunipa nafasi hii kuchangia. Nakwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu kwa sababu shukurani pongezi kutokana na Kanuni ya 155 na 154 haitaki.

Mhe. Mwenyeiti, katika ibara ya 10 kwa takwimu za uzalishaji wa chakula pamoja na mapungufu juu ya kadhia nzima ya suala la mpunga. Mwaka 2015/16 walivuna zaidi ya tani 29 elfu lakini mpaka 2016/17 tani 4300 ni ndogo sana na changamoto kazieleza. Lakini ikumbukwe tu Mhe. Waziri katika barabara hili alitwambia kwamba ndani ya miaka mitatu tutaona kwamba Zanzibar anaitosha kwa chakula, alivyochukua tokea mwanzo ukakuta tani 29,000, mwaka mmoja baadaye anapata tani 4,000. Naona bado na sina neno la kuzungumza ili lisiwakere Waheshimiwa. Kwa sababu nikisema sio makini nakosea naona sijui niseme neno gani ambalo hapa litaingia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo yake kwa sababu uzalishaji wa mpunga bado haujafikia kwenye malengo. Sijui kwa njia hii atatulisha vipi chakula, alisema apewe maeneo, apewe na misaada na nafikiri serikali imempatia. Maeneo yapo na ndio kwanza mengine ananyang'anya maeneo mengine lakini bado hayajakidhi haja.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda mbele katika kitabu hichi ukurasa wa 13. Mheshimiwa wizara iliweza kushajihisha, kuwaunganisha wakulima wa nje na ndani kufungua duka la bidhaa za kilimo. Niipongeze sana serikali na ina niya nzuri, lakini napata wasiwasi juu ya kadhia ya vikundi alivyosema kwamba kuna vikundi 127 vya vijana kutoka Wilaya zote za Unguja. Katika hili Mhe. Waziri sio vijana peke yao wanaolima. Je, hili kundi jengine la wazee vipi nalo au wazee ndiyo basi tena wameshaachwa kulima. Kwa mujibu wa kitabu chako ulichoandika kwamba umeunganisha vikundi vya vijana 127 na utawafanyia mambo mbali mbali kuwapatia mikopo katika Mabenki ya Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunayo Benki ya Wananchi wa Zanzibar vipi, hakuna njia ya kuweza kupata mikopo kupitia Benki ya Wananchi wa Zanzibar mpaka tutumie benki ya Tanzania Bara kupatia mikopo kupitia Benki ya Wananchi wa Zanzibar mpaka tutumie benki ya Tanzania Bara kupatia mikopo, naona hapa tunajidharaulisha kwamba kila kitu tuelelekee Bara wakati Benki ya Watu wa Zanzibar ipo pale na nafikiri kuna *proposal* nzuri tunaweza tukafanikiwa tukapatiya watu wetu bila ya kuwategemea upande wa pili.

Vile vile nikiendelea mbele na mchango wangu nitarudia wakati niko katika Kamati ya PAC tulikuta pale kuhusu kadhia nzima ya gari ya SMZ 6927 hii gari ilikuwa ya Wizara ya Kilimo na imo kwenye *ledger* zenu lakini Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Ndugu Islamu mlikuwa naye nyie kilimo akaondoka kenda kule kwa Makamu na ile gari kahama nayo na nyie *still* mmesema gari hamna jee hatima yake hii gari iko vipi. Nitaomba sana utakapokuja unipe jibu la hii gari jee bado imepotea katika sijui tu au bado iko kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais au iko pahali gani nitaiomba hiyo ili nipate kujiridhisha na maelezo yangu.

Mheshimiwa nikiendelea mbele nende katika hii suala zima la kadhia ambayo tumekabiliana nayo ambao wachangiaji wangu waliopita wamezungumza hayo hayo lakini kila mmoja ana muono wake katika kuchangia na mimi nitagusia kidogo tu katika hiyo halafu baadaye kwa ruhusa yako Mhe. Spika kutokana na kanuni ya 111 ya Baraza la Wawakilishi nitaomba tuunde Kamati teule kwa ajili ya kadhia hii nzima ya mchanga hapa Zanzibar.

Imekuwa tatizo na wananchi wanapiga zogo sana hawajui ukweli uko wapi wamedhulumika watu mashamba yao wamepoteza zaidi ya mabilioni ya mapesa katika hili naona sasa hivi Serikali imendelea na kufanya biashara zamani Serikali ilikuwa inafanya biashara ikaacha sasa hivi serikali imeendelea tena na biashara, basi nitaomba ninatanguliza kabisa ili nisije nikasahau ikae kwenye *Hansard* kwamba niombe Baraza lako kutokana na kanuni ya 111 tuunde kamati teule kuhusu kadhia hii ya mchanga.

Nikiendelea hapo hapo katika suala la mchanga bado kuna changamoto ambazo wananchi wetu wanazipata mbali ya kupanda bei tu hata wale wenye magari yao wanaendea kuchukuwa mchanga shimoni bahati mbaya siku ile hajauza siku ya pili akiupakia mchanga ule na cheti chake anapata shida, kuna vikosi vya SMZ, kuna Polisi, kuna Maliasili wanawakamata wanatonzwa faini huku ha kule imekuwa kama kichochoro cha wajanja kujipatia pesa ili waachiwe utalipa laki tatu lakini unaachiwa. Sasa tuangalie mtu cheti anacho cha jana mchanga wake kashindwa kuuza leo kaumwaga chini ili gari isiumie anapakia

siku ya pili anakwenda kwenye *site* hana risiti ya siku ile anakamatwa na kutozwa faini namna hiyo, nitakuomba sana Mhe. Waziri hili jambo ulikemee najua lipo kwa sababu uhakika ninao na ulikemee na uunatafuta njia mbadala.

Lakini sio hilo tu hata katika bei elekezi ambayo imetangaza Wizara yako hazifuatwi wananchi wale wanasikitika wenye magari yao wakipata bei zenu elekezi gharama zinakuwa kubwa. Pale mwanzo walikuwa wanapakia kwa elfu nafikiri elfu 40,000 sasa hivi wanapakia kwa elfu 40,000 kwa kijiko kule wakati mwanzo walikuwa wanapakia kwa Shs. 25,000 na 30,000 kwa hiyo gharama zimeongezeka na hata juzi tu nilisikia kwamba kumekatwa miti na kuwekwa misumari ya chuma na misumari ili itobowe magari pana tatizo, na yote hii mchanga wa huku asiende na wala wa kule wasiende. Mheshimiwa ulikuja na rai nzuri sana lakini rai hiyo imezaa dhahama kwa wananchi wetu wamekuwa wanalalamika kuhusu kadhia nzima hii ya mchanga.

Si hiyo tuu hata kuna watu ambao waliboresha yale maeneo yao Serikali imewanyanganya au niseme Wizara yako imewanyanganya sijui kulikoni kuna watu wameboresha yale maeneo, wametumia gharama za nyingi sana. Kuna wengine wametumia mpaka 1.2 bilioni ni pesa nyingi ananunua shamba anapanda miti namna gani unakwenda unakata miti hakuna taarifa ardhi ni mali ya Serikali hatukatai lakini kuna *approach* nzuri kwa wale wenye mali, waambiwe ili mkubaliane waweze kufanikisha kwenye lengo lenu lakini kwa utaratibu huu ulofanyika kwa kweli hauvumiliki ni utaratibu mzito sana, umewatia watu hasara kubwa sana, leo hii mtu shamba yake mwenyewe hana uhuru nayo kuna vikosi vya KVZ vinalinda.

Kuna vikosi vya KVZ kwa kweli hatutendi haki katika watu wetu tunajua watu wetu wanyonge wamejiekeza pesa zao nyingi tuu kuna wengine maskari pale wamefika kwenda *Darfur* huko wameenda kilinda amani wamepata pesa kuja kuwekeza pale leo hii unamnyang'anya shamba kwa kweli Mheshimiwa hilo kidogo linaleta ukakasi.

Nikiendelea mbele vile vile nakuta suala zima kwa mujibu wa maelezo yako umesema kwamba ili Zanzibar tujitosheleze unakuja na wazo la kuleta vifaranga vya samaki duu mimi napata shida katika hilo. Kwa sababu Zanzibar hatujafikia mpaka tutoe vifaranga vya samaki tufuge samaki, kwasababu eneo letu la bahari linajitosheleza samaki walioko bahari kuu hatuwavui sisi kuna samaki wengi sana kule. Wavuvi wetu hawana uhakika kwenda baharini hawana hata uhakika wa kupata samaki aina gani kwa sababu hakuna vyombo, hakuna elimu, namna gani. Sasa leo kutwambia kwamba unatuletea rai ya kufuga vifaranga vya samaki au kufuga samaki tena Zanzibar kisiwa, kwa mimi

kidogo akili yangu naona bado hatujafikia huko isipokuwa ningekuomba tu wale wavuvi uliokuwa nao uwawezesha uwapatie vifaa vya kisasa kama boti za kisasa kama hizo ulizosema kama ZAFICO, unakuja nazo na wale wavuvi wetu wende katika bahari kuu kuvua samaki. Lakini siyo suala la kutuletea vifaranga vya samaki mimi hapa kidogo napata shida.

Nakufahamu sana Mhe. Waziri katika hilo pengine mzee ndio uko kwenye biashara na wewe unaingia kule maana mchanga mmechukua pengine na hii vile vile utakuja kunambia Serikali inataka kuleta vifaranga vya samaki iwe biashara yao. Ningekuomba sana Mheshimiwa katika hilo kidogo tuliangalie vizuri.

Vile vile Mheshimiwa nikiendelea mbele nende katika suala zima la ufugaji wa mazao ya mifugo nazungumzia kuhusu kuku sasa hivi kumekuwa kuna kadhia kubwa ya gharama ya ufugaji kwa wafugaji wetu, wafugaji wetu wengi sana wanashindwa kufuga kutokana na gharama ya kupanda chakula, chakula kimetoka kwenye elfu 43,000 mpaka dakika hii unanunua elfu 61,000 nini njia mbadala ya kuweza kuwawezesha wale watu na sasa hivi tunakokwenda kuna *shortage* ya mayai au tutakuwa na *shortage* ya mayai kutokana kwamba wafugaji wengi wa kuku waliuza baada ya gharama za chakula kupanda. Chakula kimepanda sana, hatuwezi kuingia katika ushindani wa soko la ufugaji katika gharama hizi ambazo zimepanda sasa hivi. Yai itakuwa tatizo Zanzibar hao makuku peduu tusiyoyataka yataendelea kuja tu kwa sababu ya gharama za ufugaji haziendani na soko lilivyo tunakuomba sana Mhe. Waziri uliangalie hili suala kwa kweli wafugaji wetu wanasikitika kila ikikaa unahimiza kilimo, ufugaji lakini kwa upande wa wafugaji bado hatujakuwa tayari. Basi ningeomba ulete rai tuanzishe kiwanda cha chakula la mifungo, ingekuwa vizuri sio kutuletea rai kuanzisha vifaranga vya samaki, ungeleta rai ya kuanzisha viwanda vya mifugo kwa ajili ya mifugo ingetusaidia sana tungeinua wafugaji wengi sana na wangekuwa na hamu ya kufunga kwa hivyo ingekuwa angalau mfuko wa chakula unaweza kununua kwa elfu 40,000 na 50,000. Lakini leo hii mfuko wa chakula elfu 61,000 ni pesa nyingi sana ukiangalia na soko lenyewe toka unanunua kifaranga mpaka unamkuza mpaka unamuuza haendani katika soko hili. Ningekuomba sana Mheshimiwa katika hicho utusaidie sana tena zaidi ya sana kuhusu kadhia hiyo kwa sababu hiyo ni kadhia kubwa sana kwa wananchi wetu.

Lakini vile vile wakati napitia hiki kitabu nitaomba Mheshimiwa unisaidie ndio lile neno lengine nililolitumia jana nikagombwa sana hapa sio kulitumia lakini sijui ndio lugha gani katika kiambatanisho namba moja tofauti ya uzalizaji wa mazao ya chakula, mimi nilipokuwa nasomeshwa skuli karafuu niliambiwa zao

la biashara lakini kwenye kiambatanisho chako hiki umeandika tofauti ya uzalishaji wa mazao ya chakula moja karafuu sasa hujapitia au *typing error* au vipi nitaomba sana katika hicho ndio yale nilosema hamjakuwa tayari sijui niseme kwamba hamjawa waangalifu. Samahani kwa kuzungumza lugha hiyo naogopa kugombwa kila *time* lakini hamjawza waangalifu ulipokee na usikarike nalo kwa sababu ndio maana karafuu ikawemo katika mazao ya chakula, kiaangalie kiambatanaisho chako.

Vile vile tu nikienda mbele tena nakuta kwenye kiambatanisho namba 2 tofauti ya uzalishaji wa mazao ya mifugo hapa kuna maziwa, mayai na nyama ya ng'ombe lakini kwenye nyama iangalie vizuri hapa nazungumzia *peaces*, nazungumzia *liters*, nazungumzia *kilo* ni kweli itakaa kwenye *paragraph* moja kama hivi naomba unisaidie ili nisionekane tobwe zaidi katika hicho. Nilitaka kusema hivyo ili tuendane vizuri na hivi vitabu vyetu tunavyoviangalia jee tunavipitia ipasavyo mpaka tunavileta hapa tunavisoma na baadae unakuta makosa kama haya madogo madogo ambayo yanaweza kutatulika.

Vile vile nikiendelea mbele nakwenda kwenye suala zima la mikarafuu kwanza niipongeze wazo zuri sana, Serikali inatoa mikarafuu, inatumia pesa nyingi sana na kupata fedha za kigeni miche inachukuwa mikarafuu mengi sana lakini jee ningeomba basi Wizara yako ya Kilimo na Shirika la ZSTC, muunde kitu kimoja ili miche ya mikarafuu mnayotoa mnawapa wakulima wetu muijuwe mikarafuu mingapi tuliyoitoa na mingapi imekufa na mingapi iliyokuwa. Kwa sababu angalau ionekana kuna *follow up* tunatoa mikarafuu mingi sana miche mingi sana tunatoa *thousands* ya mikarafuu lakini ukuaji mikarafuu inakuwa kidogo zaidi sasa kila siku tutakuwa tuna *shortage* ya mikafuu. Hii ningeomba labda katika hicho labda ungefanya utaratibu wa kufuatilia safari hii tumetoa mikarafuu laki moja, jee mikarafuu yetu laki moja mikarafuu yetu laki moja imekuwa yote laki moja au tumepata mikarafuu elfu thamanini, kwa hivyo utajua mwakani tufanye vipi ili tunaendelea kungalia kwamba tunafika katika malengo yetu.

Chengine nende katika suala zima la Utoaji wa Ruzuku wa Pembejeo kwa Kilimo kuendelea kutoa ruzuku huku pembejeo za kilimo, mpunga na taratibu za ununuzi bado haujafanikiwa vyema imekuwa kuna matatizo mengi kama kuchelewa, ubora wa pembejeo. Juzi tu hapa lilikuja swali kuna dawa zaidi ya tani mia nane nafikiri zimeharibika ambao dawa imeingizwa kwenye soko kwa wakulima wetu, sasa na hili nitakuomba sana Mhe. Waziri uliangalie kwa sababu dawa ile tayari imeingiza hasara zaidi ya shilingi milioni mia tano imezungumzwa hapa, wakati wa maswali na majibu lakini ikawa hatujapata jibu siku ile likaletwa jibu likasomwa hasara karibuni milioni mia tano ya dawa

ile iliyokuwepo ndio changamoto kama hizo, ziko changamoto nyingi sana katika hii pembejeo kwa wakulima wetu bado wanasikitika kwamba hawapati ndani ya muda na mazonge mazonge mengine, najua una nia ya kweli kabisa kuisaidia nchi hii nakushukuru sana katika uongozi wako lakini bado inahitajika ufuatiliaji wa ziada ili kuona tunafika kule kwenye malengo yetu tunayohitaji kwamba kuona kwamba baada ya muda si mkubwa Zanzibar tuweze kulisha chakula chetu wenyewe bila kutegemea chakula cha nje.

Vile vile nikiendelea mbele Mheshimiwa umetuambia hapa kwamba kampuni ya ZAFICO hatimaye imerudi tena nikupongeze sana kwa dhati kabisa kweli unayo nia kwa sababu nakumbuka zamani alisema tulikuwa tunanunua samaki wa ratili hapa. Kuna vituo mbali mbali vibandani tunakwenda kununua samaki wa ratili, lakini baada ya muda ule utaratibu umekufa. Kwa hivyo hata hilo naliomba utapokuja kuanzisha utaposimama basi uweko ufuatiaji wa makini ili lisitokee kama makosa yaliyotokea nyuma, ikapelekea Shirika lile likafa na hatimaye sasa hivi tunaanza tena upya kuanza ni kupoteza gharama nyingi sana kwasababu umetuambia kuna karibuni bilioni 7,000,000,000 katika kulianzisha Shirika lile japo ni pesa zetu si zile za ndani sawa, lakini lisimame wenyewe lijitosheleze. Sio leo tunakusanya pesa nyingi tunawaambia matatizo yetu ya ndani yanatupatia pesa baada ya miaka kumi tukiulizwa tena au mitano hakuna ZAFICO wala boti, wala wafanyakazi itakuwa hamtendei haki wananchi wa Zanzibar.

Nilitaka niseme hayo machache tu Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa muda wako huu lakini nakazia, vile vile naliomba Baraza lako tukufu kabla ya kupitisha bajeti hii basi tutowe ruhusa tupige kura kutaka kuunda kamati teule kwa ajili ya kadhia ya mchanga.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Diwani sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya akifuatiwa na Mhe. Sarahani na namuona Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa naye ajitayarishe.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kuniona jioni hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Mimi nitajikita kwenye ukurasa namba 63 Mheshimiwa ambapo kuna pana programu mbili hapa mimi nitazungumzia maendeleo ya uvuvi na uhifadhi *protection* ya bahari.

Mhe. Waziri, awali ya yote napenda kupongeza sana hotuba hii kwa wataalamu wa nambari imehifadhiwa kwa misingi hasa ya nambari bilioni imeainisha kama ni bilioni na milioni imeainisha kama ni milioni hongera sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kwa heshima kubwa naomba kukuuliza kwa muda huu sote tunaelewa kuwa bahari inaliwa na inaliwa kwa kiwango kikubwa na maji tukiangalia ukanda huu kuanzia Chukwani.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ahmada Yahya samahani kidogo kabla ya kumpisha Mwenyekiti aendelee na mjadala huu nilikuwa naomba nitowe taarifa kidogo suala zima la Mhe. Abdalla Diwani pamoja na Mhe. Machano Othman Said asubuhi juu ya kuundwa kwa kamati teule lakini kama kanuni inavyosema ni haki yenu, lakini kwanza tulikuwa tunaomba mpaka Waziri atakapokuja kutoa majumuisho tukiwa tumeridhika basi naona itakuwa haina haja kama hatujaridhika kama ulivyosema tunaweza tukapiga kura na hiyo kamati ikaundwa, lakini kwanza tuwache mpaka atakapokuja Mhe. Waziri katika majumuisho yake. Sasa naomba nimpishe Mwenyekiti ili aendelee na majadala.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naendelea Mheshimiwa kwa heshima kubwa naomba kukuuliza kwamba sote tunaelewa kuwa bahari inaliwa na inaliwa kwa kiwango kikubwa hususan kuanzia ukanda wa jeshini Chukwani mpaka Kizingo hali ni mbaya na inatisha na kwa kisayansi ukanda huu ardhi yake ni ya kifusi sehemu ndogo sana ni *coral stone* kwa hiyo jee wizara ina mpango gani, pengine kwa kushirikiana Wizara ya Ardhi, Maji, Ujenzi na Nishati kuweka mawe makubwa ambayo ni *big stone* ili kuzuia mawimbi ya bahari pindi yanapokuja makubwa.

Teknologia hii kwa hakika Mheshimiwa nina hakika unaifahamu ni teknolojia ya kutumia gharama nafuu, nyezo nafuu hata utaalamu nafuu, nchi yetu kila mmoja anaelewa kati yetu kama ina utajiri wa mawe na pindi tukitumia mawe makubwa *coral stone* na tukihifadhi nadhani tutahifdhi hii bahari yenyewe kwanza, hofu yangu mnapofanya *visit* kwenye bahari kila siku utaona inaliwa na mawimbi ya bahari kila siku. Nakushauri Mheshimiwa uandae mpango mahsusi japo ni *pilot* kidogo kidogo wa kuweza kuhifadhi bahari, nina hofu wajukuu zetu wasije wakarithi kwamba bahari imesogea mbele na wakakoa fursa hii ya keki ya nchi yetu. Huu ni mpango rahisi wala hauhitaji gharama

kubwa kwa hivyo Mheshimiwa nakushauri kidogo kidogo na namini kwamba tutazuia bahari yetu isiliwe.

Jengine nilikuwa nasoma kitabu hiki kwa jumla programu zote nazifu tena Mhe. Waziri kimeandaliwa kitaalamu sana, lakini sijaona programu ya kunguru ambayo sasa imeanza tena kuchafua mazingira na taswira ya mji wetu, sasa kunguru imekuwa ni *disaster* hali imebadilika na wamerejea upya kwa hivyo Mheshimiwa nakushauri sana kitengo hiki ukitilie mkazo, kama dawa zinunuliwe na wawe wanafanya katika yale magenge kuna magenge maalum na hasa hawa wanakaa katika miti mikubwa kwa mfano Chukwani pana mbuyu hapo wanakaa wengi, kwa mfano pale Skuli ya Biashara kuna Mkuyu wanakaa wengi.

Kwa mfano skuli ya Mwanakwerekwe kuna muembe wanakaa wengi. Sasa ukiangalia *angle* tatu tu hizi hapa inakuwa *disaster*. Tukiimarishe kitengo hiki Mheshimiwa ili kusudi tuweze kuishi na tuweze kulala kwa amani. Kwa hayo machache mheshimiwa mimi sina hofu wizara hii naifahamu, watendaji wake ni mahiri na mabingwa nadhani una *PhD* nyingi sana hapo na *masters* nyingi sana kwenye wizara yako, ni wasikivu na wanafanyakazi vizuri. Mimi nakupongeza mheshimiwa na timu yako.

Kwa hayo, machache mia chini ya mia naunga mkono hoja yako. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ahmada anayefuata ni Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae atafutia Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii kuchangia Wizara yetu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambayo ni uti wa mgongo wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake, kwa maelezo yake na kwa kweli ameonesha nafasi zote za uendelezaji katika mafanikio na maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo sasa bila ya kilimo hakuna maisha, maana yake kama hakuna chakula ndio ukame na ndio maisha. Mimi nimsifu Mhe. Waziri kwa juhudi zake alizoibadilisha Zanzibar katika kipindi kifupi sana, kwa sababu kwa kweli katika sekta ya matunda sasa hivi tikiti linaweza likanunuliwa mpaka 1500/- na watu wamehamasika kula matikiti, watu wamehamasika kula *fruit* ilikuwa si desturi yetu kula *fruit* tulikuwa tukionekana kula *fruit* ni kama madude, chakula kilikuwa wali tu au muhogo na ndizi. Lakini sasa hivi *fruit* kuna watu humu

wanalalia *fruit* tu hawataki chakula chengine, hiyo ni hatua moja ya mabadiliko ya mfumo wa kiafya.

Kwa hivyo, mheshimiwa kwa hili nikupe pongezi kwa sababu upatikanaji wake wa haya matunda ni rahisi sasa hivi kukwambia kweli ingawa juhudi za lazima zinahitaji ziendelezwe kwa sababu kuna matunda mengi ambayo bado hatujayafanyia utafiti wa kina wa kuyaendeleza. Kwa hiyo, mheshimiwa nikupongeze sana kwa hilo, kwa sababu kwa kweli Zanzibar imebadilika katika suala la *fruit* imebadilika sana. Kwa hivyo, nakuomba tuendelee tena kwa juhudi zako hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitilie mkazo kwa sababu kwa kweli pahali panapoonekana na juhudi hatuna ulazima wa kupingana, kwamba lazima mimi wewe nikupinge kitu. Hapana mimi nahitaji kuona kama kuna kasoro na mimi nitoe mchango wangu ili kuiendeleza nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wewe ni Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini nataka nikwambie kwamba unaweza kuwa unaungana na wizara nyingi sana zinagusana ama unaonekana humo humo ama unaonekana si huko lakini hutoki. Kama sisemi vibaya Mheshimiwa wewe una dhamana kubwa sana, moja ya kuupamba mji wetu, uupambe mji wetu Mheshimiwa kwa miti. Ukiupamba mji huu utabadilika mandhari yake sio kujenga mabanda ya chipsi tu, na miti iwepo ambayo kama tulivyokuwa tunachangia baadhi ya maeneo kwamba barabara zetu zitapendeza, kwenye maeneo ya vivuli yatapendeza, maeneo ambayo tunasema ni maeneo ya kupumzika. Kuna maeneo haya ya Uwanja wa Mnazi Mmoja ambao wakati mwengine ndio tunafanyia sherehe zetu bado waangalie wazee walivyopanda miti. Lakini hakuna mti mdogo mdogo ambao tunapanda tena. Sasa pale tunahitaji kupanda miti tena ile mengine inaanza kung'oka, kupasuka au kuanguka. Kwa hivyo, Mheshimiwa ningekuomba sana mji wetu ukaubadilisha na wewe una uwezo wa kuubadilisha, hivyo nakuomba hili ulitizame kwa jicho la huruma sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie katika bonde la Tibirinzi, bonde hili liliwekwa mahsusi hasa kuwa bonde la mpunga na ndio likatiwa mlango wa kuzuia maji ya bahari yasiende na mengine yazuie kwa bonde la mpunga. Lakini bonde lile sijui kwa tabia nchi ambayo mazingira yamebadilika, lile bonde kwa mpunga halikubali tena kwa muda huu, sijui kama litaweza kukubali tena. Mhe. Mwenyekiti, lakini lile ni eneo la *asset* la kuweza kutengeneza mimi natoa kama wazo la kutengeneza bwawa la samaki katika maeneo yale ambalo kama limejijenga, kwa sababu maji yanaingia wenyewe unaweza ukayazuia, unaweza ukayafunga. Ningekuomba sana ukalitizama lile

bonde tusipoteze ile nafasi kwa sababu kilimo cha mpunga kimekataa pale mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakuomba wewe pamoja na wataalamu wako lirudishe lile bonde ili litizamike watu wanaanza kulijenga sasa, wanaingia mule mule juzi tumewavua kwenye bahari, lile si bonde la kujenga lakini kutokana na linavyoachwa litajengwa hivyo hivyo watu watakaa. Kwa hivyo, mheshimiwa nikuombe lile bonde la Tibirizi hebu watafute wataalamu walitizame tutalifanyaje tusiliache vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema Mhe. Waziri na mimi nikusifu sana. Mhe. Mwenyekiti, samaki wa kufuga wana mipangilio, samaki wa kufuga unavua unachokitaka, sio mtu kwenda baharini akasema leo upepo mkali, leo sikupati. Ukitaka kuvuna unavuna kwa ustaarabu, ukitaka kuuza umejipangilia. Kwa hivyo, nakuomba kama ulivyokuwa umejipangilia hii sekta ya samaki ya kufuga iendelezwe kweli kweli, iendelezwe kwa sababu ina upeo mzuri tu wakuweza tukapata mazao zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na bonde la Chamanangwe au ule uwanda wa Chamanangwe. Mhe. Mwenyekiti, naukumbuka ukanda ule palikuwa na ng'ombe wa kutosha lakini pia palikuwa na majani ya kulishia ng'ombe yakutosha. Leo watu wameshagawana mapande wamevuta kamba maana yake pale hapajapimwa watu wanavuta kamba tu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikuombe nafasi yako ile utakuja taka tayari kwamba wewe una uwezo wa kifedha kwa biashara ile ya ng'ombe lakini nafasi huna tena. Kwa hiyo, ningekuomba ukatafuta nafasi ya kupima lile eneo lisiguswe ukaliendeleza katika kilimo kama hiki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye zao la nazi. Mhe. Mwenyekiti, watu walikuwa wakitafuna mbata, walikuwa wakisema labda wana njaa lakini imeonekana ukitafuna mbata mpaka maradhi ya sukari yanatoka. Mafuta ya nazi ukiyatia kwenye nywele za mwanamke zinang'ara vizuri sana, enzi hizo wazee wetu walikuwa wakijipaka mafuta ya nazi anang'ara hamna habari ya makopo kopo anajua Waziri Amina Salum Ali pale ameshatutolea maelekezo sana. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, nazi haipo na hata ukitaka mafuta ya nazi huyapati.

Sasa hivi kuna daktari moja niliwahi kuona *message* moja yuko America alikuwa anahojiwa kuhusu habari ya maradhi ya sukari. Anasema maradhi ya sukari sumu yake ni mafuta ya nazi, kama mtu atakuwa anaweza kunywa vijiko kama viwili asubuhi na usiku basi sukari itashuka. Lakini mafuta ya nazi yaliyo

pure sio yale ya viwanda ya nazi ambayo tunapika kwenye masufuria na kuyagida vizuri. Zamani tunakula mpaka ule ukoko wake wa chicha watoto wanang'ara kweli kweli. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nazi ilikuwa na hoja nzuri sana, hivyo naishauri wizara upandaji wa minazi kwa ajili ya kurudisha minazi mheshimiwa nakuomba sana kama ulivyo na *speed* ya mikarafuu basi na minazi uweze kuirudisha.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije kwenye suala zima la mazingira. Mhe. Mwenyekiti, tunapanda mti mmoja tunakata kumi, sasa hatufiki mtu sasa hivi mimi nataka niseme tu kwamba serikali nayo imeacha upeo mkubwa kwa wananchi kila kitu mtu ni chake. Serikali haina lake, mnazi unaupanda wewe lakini wakati wa kuukata si wako tena ukaombe kibali mnazi ndio uukate, mkarafuu ndio uukate akikwambia mkarafuu wangu naukata. Mheshimiwa hilo ni zao la taifa unakwenda kukata mkarafuu halafu sheria hakuna kuchukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tutakuwa tunakwenda mbele tukirudi nyuma, tutakuwa hatwendi kwa sababu mkarafuu unakatwa. Mkarafuu kuota mpaka ukaja ukazaa ni miaka sita, ingawa kuishi kwake ni miaka mia mbili unaishi, lakini wazee wetu wametuachia urithi wa mikarafuu kati kati tumeikata yote. Leo tunauhitaji mkarafuu haupo tunapiga *speed* mpya ya mkarafuu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningeomba adhabu za kukata mti zirudi, heshima ya kukata mti irudi kama kuna kibali kutoka kwa sheha lakini mtu asikate mti wake tu inakuwa hatufanyi vizuri, maana yake huku tunapiga kelele kupanda, huku tunakata. Kwa hivyo, ningekushauri hayo niliyoyasema.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasema kwamba katika sekta za kilimo kwenye zana za kilimo, kwenye utafiti, kwenye mambo ya matrekta na kila kitu. Mhe. Mwenyekiti, kama wizara ina mafungu mengi, ina mambo mengi basi haya mafungu ya pesa ambayo yana tafiti, ambayo yana zana za kilimo ambayo yana mambo mengi, haya mheshimiwa fungu lake lisingekuwa linaingizwa kwenye wizara, unaliingiza fungu lake kwenye tafiti. Watafiti watakaa watajua wana kiasi gani cha pesa zao na wafanye nini katika tafiti hizo, ukisubiri fungu la wizara haitokubali wizara kama kuna kasoro fulani aje ampe mtafiti. Tunaona kwamba mtafiti hana maana yoyote ingawa ana maana kubwa sana, lakini serikali ilishamtengea fungu ila pesa zimeingia kwenye wizara.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu kwenye kitabu cha Mhe. Waziri umeshafanya mazungumzo na Mahindra katika zana za kilimo unataka kununua matrekta 20. Sikushawishi sana lakini naweza kusema Mheshimiwa

matrekta niliyozoea ambayo yanatumia nguvu sana na yana uwezo wa kukaa muda mrefu *ford* nilikuwa naikumbuka. Wenzetu hawa watengenezaji wa matrekta lakini udongo wetu tuukumbuke ardhi yetu ni ngumu unaweza ukatia trekta ikanyuka mbele haikati. Sasa wasije wakatupa trekta ndogo ndogo ikawa mabonde mengine hayendi ikabaki tunatizamana. Kwa hivyo, ningeshauri kabla hatujanunua matrekta ukafanye utafiti tena mheshimiwa wewe mwenyewe kwanza ni ushahidi kwa sababu nyumbani kwako ni Wawi, kwenu ni Wawi na palikuwa na Kiwanda cha Matrekta Wawi.

Mhe. Mwenyekiti, tena mimi nataka nikuulize utakifufua lini kiwanda kile kwa sababu pale trekta zilikuwa zinasubiri kilimo, sio kama kilimo kinasubiri trekta. Matrekta yalikuwa yamepangana yanasubiri siku za mvua, leo trekta hapana lakini mheshimiwa kile kiwanda kifufue kitasaidia kweli kweli. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ana-*speed* ya kufufua kilimo, sasa namuomba Kiwanda cha Matrekta kifufue. Lakini na hii habari ya pesa Mheshimiwa haya mafungu yafungulie *account* iwe pesa zao zinaingia kwenye vitengo, wawe wanajijua mtafiti sisi tunamkamata mtafiti pesa yake ipo lakini tunapitisha fungu hapa kesho linaingia kwenye wizara unakula vyengine. Hivyo Mheshimiwa itakuwa haiendi, hilo jengine.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nikwambie kitu kimoja kwa utaalamu wa zamani wenzetu Wazungu kuja katika *system* ya kilimo walitumia mapikipiki zaidi katika kufanikisha mambo haya. Leo Mheshimiwa mnanunua magari tu ma-*Prado* gari moja la *Prado* linanunua pikipiki kumi, hebu yanunue mapikipiki uyasambaze mheshimiwa hawa watu wafike vijijini. Mtafiti na mtu ambaye ana sekta ya kilimo hana shida ya gari yeye pikipiki lake linamtosha kwenda kufanya shughuli zake, kwa sababu huyu haingii barabara anapita njia za chochoro kwenda kwenye ng'ombe, kwenda kwenye mabonde ya mpunga watafutie mapikipiki wala sio vespa mapikipiki ya nguvu yakuweza kuingia mabondeni. Kwa hiyo, nikushauri Mhe. Waziri gari moja ya pesa zake unaweza kununua pikipiki kumi kata msingi wa magari kidogo wanunulie mapikipiki uangalie kazi itakavyokwenda. Mheshimiwa hilo nilikuwa niliendeleze.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka kusema uvunaji wa maji niliona humu kuna uvunaji wa maji ya mvua, hebu mheshimiwa utakapokuja njoo utuelezee kidogo huu uvunaji wa maji maana yake Mwanakwerekwe maji hayana pakwenda, Kibonde Mzungu maji hayana pakwenda. Sasa wewe unataka kuvuna maji hebu njoo useme maji unayotaka ni yepi? Maana yake mvua zilizokuja hizi kama Mheshimiwa maji haya utayamiliki kwa kuya-*store* ukayavuna mwaka mmoja sisi hatuna shida ya maji mimi ninakuhakikishia. Sasa njoo unipe utaalamu wa lile shimo la Mwanakwerekwe utalifanyaje, njoo

unipe utaalamu wa maji ya Kibonde Mzungu yanayoua kila siku maji yale tuyavune vipi au unataka msaada gani tukupitishie uya-*store* maji haya. Sisi tunayafungulia milango yaende baharini lakini keshokutwa tunaandika vitabu jua na kali maji hatuna. Hapa mheshimiwa na wewe tumia utaalamu wako uje utufahamishe kidogo unataka msaada gani ili uvune maji maana yake hayo ndio mambo ambayo yapo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hebu tujitizame tulipo na utaalamu ulipo miaka ya nyuma *fisheries* walikuwa na boti za nguvu za kuweza kwenda bahari kuu, lakini leo ndio tumekuwa watu wakubwa na utaalamu mkubwa hata viongozi wetu lazima niwaambie mkitoa misaada msitoe boti ndogo ndogo, hebu agizieni boti ya uhakika hizi boti ndogo ndogo wanaziuza hawa. Mheshimiwa ukiwapa boti za mbao baada ya mwezi wanagawana mbao kila mmoja anachukua chake, lakini nina uhakika watu hawa zikanunuliwa boti kwa sababu wana utaalamu mkawapeleka *fisheries* wakakaa chini ya serikali basi watavua samaki kwa uhakika na nakuhakikishieni kwamba tutakula samaki na tutauza nje. Kwa hivyo, ningeomba serikali ifanye jitihada za kununua boti za uhakika za kuweza kwenda bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunaibiwa bahari kuu hatwendi na kitoweleo chetu ni cha shida, mtu mpaka aende akavue nguru mmoja arudi huyo huyo akija akimgawa na mtu wenyewe ana wake wanne anategemea nguru huyo huyo basi humnunui. Kwa hivyo, lazima Mhe. Waziri ujikaze kweli kweli kutafuta boti za uhakika halafu watu hao hao utawaajiri wewe, lakini ukiwanunulia boti za mbao wataziuza zote na wanakaa pale pale barazani. Kwa hivyo, hilo nilikuwa nikwambie tena.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimwambie Mhe. Waziri kitu kimoja kwamba wewe una dhamana kubwa hata hivi sasa Ramadhani inakuja tunakutizama wewe, soko likichafuka pale tunakutizama wewe, lakini Mheshimiwa kitoweo ni ghali, nyama ya ng'ombe kilo ni 10,000/- atakula nani? Wewe una uhuru una uwezo wa kwenda Bara ukaleta ng'ombe hapa angalau huu mwezi wa Ramadhani watu wakala kitoweleo kwa 5000/-. Tukiwafuata wafanyabiashara mheshimiwa kila siku watatuzidishia bei kilo itafika 15,000/-. Sasa wizara yako ina utaalamu, wizara yako ina mawasiliano na Bara tutafute ng'ombe na wenzetu hawa hawatumii dola tunatumia pesa zetu hizi hizi za Tanzania tukaleta ng'ombe tukawakusanya tukawa tunatumia. Pia mimi ningekushauri fungua shamba jengine Bara ambalo litaweza kuwa linashughulika na ng'ombe na mbuzi ambao watakuwa walaji ni wa Zanzibar na watakuwa wameangaliwa kiafya, lakini usafiri wao moja kwa moja utakuja huku.

Mheshimiwa tukiliachilia suala hili kwamba tuliache tu hivi hivi basi wafanyabiashara watakuwa wanawaumiza walaji siku zote, na wewe mimi nakuhakikishia kwamba utaweza kutuweka vizuri katika masuala haya ya kitoweo kuanzia samaki. Mheshimiwa kimerudi kidogo nikupe pongezi huku nakulaumu laumu lakini huku nakupongeza. Kwa kweli nakwambia matunda, kitoweo cha samaki na ng'ombe wameongezeka katika ulaji vizuri wa watu lakini bado jitihada za makusudi zinahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kama watu watakula nyama ya ng'ombe vizuri sana na samaki basi hospitali hawendi. Mhe. Mahamoud Thabit Kombo tutampunguzia kuagiza dawa kwa sababu chakula ni uzima. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri nguvu hizi kwa sababu sasa hivi hayo matunda tu watu wanang'ara kweli kweli, sasa hivi Wazanzibari wanang'ara kwa matunda. Kwa hivyo, ningeomba sana suala hilo nalo ukalitilia maanani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika kitu ambacho nimeona ni mtu mmoja ambaye nimekuona leo ni mstaarabu wewe umenitilia changamoto, kwa sababu vitabu vyote hivi anataka pesa tu lakini changamoto zake hazisemi, na ukimsemea mwengine akasirika. Lakini nimekuona humu umeweka changamoto na umezitaja na nimefurahi kwamba ukisaidiwa hizi moja ambalo limo humu ni ushirikiano wa watu na wananchi ambao hukwambia kweli wao ndio nguvu kazi kubwa. Kama tunawaongoza basi wakikubali kuongozeka kila mmoja atajua wajibu wake na tutafanya kwa kweli, kwa hivyo, nimsifu kwamba na kasoro alizonazo kule kwenye wizara yake ni hizi, kwa hivyo Mwenyezi Mungu atamjaalia hizo kasoro zitaondoka ili tuweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa jengine ambalo nataka nikuombe kuna mashamba mengi ya serikali nataka ayalime iwe mfano kwa watu, sekta ambayo amejitahidi sana ni sekta ya kusaidia vikundi, amewasaidia na watu mmoja mmoja. Watu wana tabia, wana tabia mwengine ana ng'ombe wake wa maziwa mke wake akiwa na mimba anakwenda kujifungulia kwao anaondoka yeye na mkewe wakenda wakajifungulia huko ng'ombe wakamuacha akafa. Sasa wewe ukiwa una ng'ombe wako wa uhakika ambao wana wataalamu ng'ombe hawafi, mimi najua sana Mhe. Waziri anapata hasara sana kwenye maeneo, watu unapofika wakati wa kijamii anasahau ile biashara yake, wewe kwani ukimpeleka mkeo ukarudi unasema hapana mpaka azae ndio nirudi ng'ombe atakufa. Sasa tukisema tunawategemea sana hawa watu wa kawaida watatupeleka pabaya ndio kama hivyo unavyoona, viongozi wetu hao wanatoa maboti yawasaidie kuvua wanaliuza wanarudi pale pale wanakutizama machoni tena, wewe umeshategemea kwa hilo.

Sasa mimi ningemuomba sana aongeze nguvu zake yeye mwenyewe za wizara pahala pa ng'ombe aweke ng'ombe kweli kweli, pahala pa kilimo aweke kilimo kweli kweli. Mimi nina uhakika ule msemo wake aliosema kwamba ana uhakika mpaka mwaka 2020 mchele Zanzibar tutakuwanao wa kutumia wenyewe, mabonde yetu haya kila anapoona kwenye kilimo apeleke trekta, apeleke mtaalamu, apeleke mbegu, atizame Mheshimiwa namhakikishia kwa utaalamu wa kumwagilia maji ninavyoona na Mwenyezi Mungu akimjaalia akaweza kuvuna maji mwakani, mara hii hakuweza mvua zilikuwa nyingi zilimzidi, mwakani yasimzidi maji. Mwakani kabla ya kujipanga ajipange kabisa maji atayadhibiti vipi ili maji haya yaweze kutuendeleza sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nataka nimsifu sana kwa kweli ni waziri mahiri kwa upande wa kilimo, mifugo na maliasili. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa kwamba asichekee mali yoyote ambayo inahusika na serikali ambayo ina maendeleo ya serikali akayafumbia macho. Kuna mambo mengi yanayohusu wizara, yanayohusu serikali kwa jamii, kwa umma, kama tutayafumbia macho hatwendi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said bado dakika moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hee! Mheshimiwa nilifikiri utasema tano lakini haya tuendelee. Sawa ahsante Mhe. Mwenyekiti. Sasa Mheshimiwa katika jambo ambalo litatusogeza mbele ni kwamba asifumbie macho sheria ambayo ipo na kama anaona haitoshi ailete tuje tumbadilishie. Kwa sababu Mheshimiwa unajua nataka niseme vizuri kwamba serikali yetu, neno 'serikali yetu' tunalitafsiri vibaya, kila jambo ni letu ndio ni letu, lakini wakati wa letu ni kuvuruga si wa kuongoza. Sasa tukisema ni letu kwamba ni letu ni tofauti, sisi tulifikiria kama litakuwa letu ndio tulibebe tulisogeze mbele, lakini kumbe ni letu wanalivuta wanaliangusha haliendi. Kwa hivyo, ningemuomba Mheshimiwa asicheke na maeneo, asicheke na mtu anayekata miti, asicheke na mtu anayevuruga maliasili, yeye asimame mstari aangalie kitu gani kwa utafiti aliyonao. Kwa sababu hatumii kauli ya maneno anatumia tafiti. Nimemuona humu Mheshimiwa kama alivyosifu mwenzangu hapa mimi naona yeye na Mhe. John Pombe Magufuli wako sawa sawa, ana takwimu mpaka za wapi, takwimu za uhakika Mheshimiwa hao watu wawili nashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mheshimiwa nawasifu sana Mhe. Rais John Pombe Magufuli kwa takwimu na Mhe. Waziri wa Kilimo,

Maliasili, Mifugo na Uvuvi kitabu kizima chote hiki ni takwimu. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa anayefuata Mhe. Asha Abdalla Mussa na baadaye atafuatia Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuzungumza machache na kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nami niungane na wenzangu ambao wamechangia na wameweza kuhoji mambo mbali mbali ambayo yanaikabili Wizara hii ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wetu wa Kilimo pamoja na watendaji wake wote na tunaona kwamba Mhe. Waziri anachukua juhudi kubwa sana na kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wananufaika kwa suala zima la kilimo, uvuvi na mifugo pamoja na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wajumbe wenzangu wamezungumzia baadhiya mambo mengi mimi nitachukua kama dakika tatu tu nizungumzie haya yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa upande wa kilimo. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kusimamia wizara yake na kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanalima mazao ambayo yanaweza kututosheleza kwa ajili ya chakula pamoja na biashara. Lakini niseme kwamba wapo baadhi ya watu ambao wasiowatakia nchi yetu maendeleo wanakuwa waharibifu wa mazao hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitolea mfano mwaka jana wananchi wa maeneo ya Pemba walijitahidi sana kuimarisha zao la karafuu kwa ajili ya biashara, cha kusikitisha baadhi ya watu walikwenda wakaikata mikarafuu ile. Nilitaka nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze wale watu ambao wamehusika na suala la ukataji wa mikarafuu wamefikia wapi. Je, wamepatikana? Kama wamepatikana wamechukuliwa hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, nijue kusema kwamba asilimia 90 wananchi wa Zanzibar wanajishughulisha na kilimo na hapa Zanzibar tunafahamu kwamba chakula kikuu ni wali, ambapo zao hili la mpunga tunatakiwa tujitahidi sana tuhakikishe

kwamba mpaka ifikapo mwaka 2020 basi tunaweza kujitosheleza wenyewe tusiweze kuagizishia mchele kutoka maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha kwamba tunawavunja moyo wananchi wetu kutokana na zana za kilimo ikiwemo matrekta pamoja na pembejeo nyengine. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanajibanabana wanakusanya pesa zao kidogo kidogo mpaka unapofika wakati wanapeleka katika vituo vyao kwa ajili ya kupata matrekta mapema, cha kusikitisha ni kwamba muda unafika wa kilimo lakini inafika muda matrekta hayapo. Mheshimiwa namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze Zanzibar nzima katika vituo vyake ambavyo vipo vya kilimo kuna matrekta mangapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mafanikio yaliyopatikana kupitia kilimo. Mimi nitakuja moja kwa moja kwenye ukurasa wa 10(b). Mhe. Waziri katika hotuba yake ameelezea suala zima la ununuaji wa mitambo ya kukamulia mafuta ya alizeti, kwa upande wa Pemba Ole, Dodeani pamoja na Bambi. Nataka nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba, amefanya utafiti gani kabla ya kufunga mashine zile kuhakikisha kwamba eneo walipokwenda kufunga hizi mashine linaweza kuzalisha tani 4.5 kwa siku. Mpaka sasa kwa upande wa Pemba ni tani ngapi ambazo zimekamuliwa mafuta mpaka kufikia mwezi Machi, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la uhakiki wa vyombo, majengo pamoja na mashamba. Wamesema katika kitabu chao wamefanya uhakiki katika maeneo mawili, katika eneo la Kilombero pamoja na Kibokwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika kituo cha kilimo Kilombero hali inasikitisha sana majengo ni mabovu lakini pia ile hali yenyewe iliyomo mule ndani huwezi ukaamini kwamba kuna ofisi. Kituo kile ni cha miaka mingi lakini kwa kweli bado hakijapewa kipaumbele. Namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe kwamba vituo hivi ambavyo vinashugulikia masuala mazima ya kilimo basi avipe kipaumbele kwa ajili ya kuimarisha vituo vile. Lakini pia kuna matrekta mengi sana ambayo hayafanyi kazi na mwisho wake sasa kuna baadhi ya watu inafika pahala vile vyombo ambavyo vimekaa kwa muda mrefu basi vinachukuliwa au vinaibiwa. Mhe. Waziri nimuombe kwamba avifanyie uhakiki katika vituo vyote vyombo vilivyopo ambavyo havifanyi kazi na baadae waone kama wizara wanavifanyia matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, nije suala la mwisho kuna mashamba haya ya mifugo. Kuna shamba moja ambalo lipo Pangeni, hili shamba ni la siku nyingi kulikuwa na mifugo mingi, lakini namuomba sana au namtaka sana Mhe. Waziri

atakapokuja hapa atueleze katika shamba lile la mifugo Pangeni kuna ng'ombe wangapi wa serikali lakini pia kuna ng'ombe wa watu binafsi. Basi atakapofika hapa atueleze ni sababu gani ambazo zimesababisha ng'ombe wale mule ndani wachanganyike wa serikali pamoja na watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 99, asilimia moja mpaka atakapokuja kunijibu masuala yangu haya ili na mimi niunge mkono kabisa kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha Abdalla anayefuata ni Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadae Mhe. Mussa Foum Mussa ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na kutoa hotuba ya wizara hii adhimu ya kilimo. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri, ni kwamba yuko *serious* kweli kweli kukiendeleza kilimo kwa hivyo, anastahiki sana pongezi.

Pia niwapongeze wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo kwa juhudi kubwa sana wanazozichukua kukiendeleza kilimo, kuendeleza kilimo si kazi rahisi ni kazi ya kuvunja moyo wakati mwengine, ni kazi ambayo kwa kweli ya kuchosha lakini wako wanaendelea kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwanza kidogo kwa historia baadae nitaeleza kuhusu takwimu na muda ukiruhusu nitaeleza kuhusu utafiti wa kilimo. Kihistoria tunasema kwanza kilimo ni maisha yetu sisi sote tunategemea kilimo, sisi wenyewe ni kilimo kwa sababu umekuja kutoka udongo utarudi kwenye udongo na tunategemeana. Mimea inawategemea binadamu kwa maisha yao na sisi tunaitegemea mimea (miti) kwa maisha yetu. Unapotokea uharibifu wa mazingira basi wanadamu ndio wanaopaswa kuzuia uharibifu huo ili maisha yaendelee.

Sasa kihistoria kilimo kilianza huko wenzetu wanasema Uingereza na kwengineko huko, kilimo kilianza kwa kulima kwa vijiti kikaendelea wakatumia mitaimbo, wakaendelea wakatumia farasi, tukaendelea tukapata matrekta hayo leo. Sasa kumekuwa na maprogramu mbali mbali za kilimo lengo ni kuzalisha mazao ya kutosha ili binadamu apate chakula kwa maisha yake. Tunaelewa hakuna kiwanda kinachoweza kuzalisha tunda lolote liwe fenesi, shelisheli au zao lolote iwe mpunga, mbaazi, lazima ulime upate hilo zao. Wataalamu wengine wamejaribu kuchanganya changanya pengine mbaazi

ukachanganya na mpunga utapata kitu gani kwenye kiwanda lakini hakijalika vizuri kuliko vile kinavyopatikana kutoka ardhini.

Sasa hapa kwetu Tanzania tulianza kusema kwamba kulikuwa na programu ya Kilimo Kwanza, tukawa tunasema siku zote kilimo ni uti wa mgongo wa maisha yetu, kukawa na programu ya Kilimo ni Uhai nimesema, kukawa na programu hapa kwetu Kilimo cha Mtakula, nadhani mnakumbuka, Mtakula kwa maana ya mpango wa kujitosheleza kwa chakula, mpango maalum wa kujitosheleza kwa chakula. Kama *decade* tatu zilizopita *decade* kwa maana ya miaka kumi kumi, *decade* tatu ni miaka 30 miaka ya 80 huko hapa tulikuwa na programu maalum ya kuzalisha mazao kwa wingi inaitwa *fertilizer program.* *Fertilizer program* ile ilikwenda kule shambani kumfanyia maonesho mkulima ajue unatakiwa ufanye nini li uweze kuzalisha na nadhani programu ile ilipiga hatua baadhi ya mazao yaliongezeka tija. Walikuwa wanaoneshwa namna gani ukitumia mbolea utaweza kufanikiwa, namna gani usipotumia mbolea hutafanikiwa, ukipalilia inakuwaje. Kwa sababu kilimo au uzalishaji wa mazao lazima yafanyike kwa wakati, kupalilia kwa wakati, kuweka mbolea kwa wakati na viwango vinavyohitajiwa hata kuvuna basi uvune kwa wakati; usipofanya hivyo lazima hutapata mazao ya kutosha.

Katika kukiendeleza kilimo hiki nadhani wizara yetu hii adhimu najua inafanya hivyo, inafanya kuta elimu ya ugani**,** yaani *extension*, inafanya tafiti mbali mbali lakini bado kuna haja ya kuweka mkazo katika kufanya huu utafiti ili mazao mengi yaweze kupatikana. Kwa sababu nikiangalia hizi takwimu sasa ndio nakwenda huko kwenye takwimu, nikiangalia hizi takwimu kwa kweli ni takwimu za kweli zimechukuliwa huko mashambani zikaletwa ni kweli kabisa wala si kosa la mtu, lakini ukiziangalia hizi takwimu kwa kweli zinatisha.

Mwaka 2016 ukurasa wa saba na wa nane, 2015 natoa mfano wa zao moja tu hapa. Mwaka 2015 mpunga umezalisha tani 20,082; mwaka uliofuata tani 4,000. Mahindi tani 2,800; mwaka uliofuata tani 800. Angalia punguzo lenyewe hilo sasa ukitizama kwa *average* punguzo kwenye mahindi natoa mfano, ilikuwa mwaka 2015 ilikuwa ni tani 0.4 yaani *kilogram* 400 kwa eka. Sasa hizi ukizifanya *average* kuna wale wanaopata mwingi kuna wale wanaopata kidogo, kwa hivyo utaona wale wanaopata kidogo wamepeta kidogo sana hii average ya *0.4 per* eka ni ndogo sana.

Lakini isitoshe mwaka 2016 ilishuka ikafika nusu 0.2 ukipiga mahesabu hapa utazipata hizo 0.2 takwim hii inatisha. *Trend* hii ikiendelea namna hii hicho chakula utakipata wapi. Tunapaswa tufanye tafiti kama wanavyofanya wenzetu. Wenzetu wanazalisha tani mpaka 20 kwa hekta moja ya mpunga na zaidi

wengine wameshafika 40. Sisi ndio kwanza tuko kwenye 0.4 *tones* au pengine tumekwenda mbali sana tani 6, tani 7. Hii bado haituridhishi.

Sasa Mhe. Waziri alitoa ahadi kwa nia yake safi kabisa, alitoa ahadi kwamba ifikapo mwaka 2020 tutajitosheleza kwa chakula kwa *trend* hii hatuwezi kujitosheleza. Lakini leo mimi namsifu sana Mhe. Waziri leo kasema ukweli wake. Mimi nilikusudia niulize Mhe. Waziri ulituahidi utafanya hivi mbona hatujapa lolote unafanya nini ili uweze kufikia lile lengo. Lakini leo kasema mwenyewe. Kasema kwamba kama atapata zile nyenzo zinazohitajika basi bado ana uhakika ataweza kufikia lengo lake. Nadhani hiyo ndio *statement* nzuri kabisa ambayo ndio inayofaa katika suala hili. Kama hakuna nyenzo na kwa *trend* hii tunayokwenda punguziko hili linalotokea kila mara nina hakika hatutaweza kufika hata robo.

Nikiingia sasa kwenye mfugo hapa kuna ongezeko la mayai halafu kuna takwimu zinaonesha kuku waliochinjwa mwaka 2015-2016. 2015 kuna kuku waliochinjwa ni milioni moja, lakini 2016 ni laki saba, huku mbele tunaambiwa mayai yaliongezeka ukifanya takwimu ukipiga mahesabu mayai yaliongezeka kwa kiasi cha mayai milioni mbili. Lakini sasa nikijiuliza hili punguziko la kuku la kutoka milioni moja kuchinja hadi laki saba, hili lilitokana na nini? Bila shaka labda hao Peduu inawezeka labda hao Pedeuu lakini pia inawezekana *production* nayo imeshuka. Sasa ndio nikasema hizi takwimu zetu hizi zinatisha sana, sisi tunataka tuzalishe chakula.

Siku zote tukiwa tegemezi tunaagiza tu kutoka nje hatuwezi kuzalisha chetu sisi, sasa hiyo itakuwa sijui tunafanya nini, ardhi yetu ni nzuri, mfano Malaysia, Malaysia kuna mafenesi kuna madoriani kuna kila kitu tunachozalisha hapa. Lakini ukilikuta doriani la Malaysia, ukilikuta pera la Malaysia utashangaa sana mapera yetu haya vipera vidogo, lakini kule Pera linakuwa kubwa linakuwa zuri, Fenesi linakuwa zuri hata yale mashabuka ya mle ndani inakuwa hamna unalikuta fenesi safi, doriani hili unalisarifu mpaka unasonga halua ya doriani. Sasa sisi hapa kwetu midoriani ile ile ya miaka ile ndio hiyo hiyo tunaigemea na madoriani yale hayatoshi, hiyo midoriani ya zamani pia inakatwa wamebaini watu mbao za doriani labda zinafaa basi wanaikata.

Kwa kweli, hali hairidhishi bado tunahitaji kuongeza kasi kama zile ambazo zilikuwa zinafanywa siku za nyumba ambapo *FAO* walituletea *fertilizer* programu hapa tukafanya *fertilizer* program na mazao yaliweza kuongezeka na kumbuka ilifanywa *fertilizer program demonstration plot* mpaka huko nzi wengi kule Gando ilifanywa *fertilizer program* na wakati ule nadhani Mhe. Assa Othman Hamad ndie aliyekuwa anashughulikia *fertilizer program* kule

Pemba basi mazao yalikuwa yanaongezeka kidogo kidogo. Lakini ulipoka ule mradi basi hakuna tena chengine.

Sasa nadhani tufanyeni wenyewe *technology* ipo ingawa *technology* ya leo kesho inawezekana ikawa si *technology* tena imeshapitwa na wakati, kwa sababu ya uvumbuzi unaokuja kila siku. Lakini zipo *technology* tuzifateni *technology* nadhani tunaweza tukafika pahala tukaweza kuzalisha mazao ya mifugo na ya kilimo kwa wingi sana.

Nasema wakulima wetu kwa kweli wanakufa, mtu analima kama hivyo eka nzima anapata kilogramu 200 jasho lote lililopotea. Nadhani hailipi pengine ana pesa kidogo kasaidiwa na ndugu yake ili alime lakini anachokipata hakilipi na sisi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tupo, lakini sasa tunashindwa nyezo pengine hatuna. Sasa tujitahidi sana Mhe. Waziri na bidii yako kubwa hii hebu tuingieni kimataifa sasa tupate misaada ya kimataifa ya kitaalamu na ya kinyenzo ili tukiendeleze kilimo, hakuna kishichowezekana.

Kwa upande wa miti sasa imeelezwa kwamba kuni zimeongezeka *cubic meter* nadhani elfu moja imeongezea kutoka 2015-2016 yaani kuongezeka kwa *cubic meter* za kuni matumizi maana yake umekata miti mingi. Sasa kama miti inakatwa namna hiyo hatutakuja kupata jangwa.

Mimi nasema historia ukisoma historia za ndani kabisa kule Arabuni kwenye jangwa inasemekana kulikuwa na misitu mingi sana wakaikata wakauza huko Ulaya wakawa wakawa wanakata wanauza sasa hivi jangwa. Kumekuwa ni tabu sana kupata ardhi ya kulima mpaka wafanye kitu kinaitwa *inoculation* wachukuwe udongo huko walete pale ndio waanze kuzalisha au kupanda miti wanayoitaka. Kwa hivyo, ni hasara na sisi tusifike huko tunaweza tukajikuta tunakwenda vibaya sana.

Jengine nigusie mchanga kidogo, lengo la serikali kwa kweli ni safi kabisa, ni kuondosha uharibifu wa mazingira ambao unatokea sasa hivi, mashimo ya mchanga yalikuwa yameshakuwa tishio mtu anachimba mchanga mpaka maji yanatoka chini na hayo maeneo yaliyokuwa yanatumiwa kwa kilimo ndio yanayochimbwa mchanga hatuwezi kwenda bila ya ku-*control*.

Sasa kama kuna sababu kuna tatizo limejitokeza kwa wananchi tukaeni pamoja tulitatue tuwaelimishe watu wetu wajue kwamba kuna tatizo hii ardhi tunaitegemea sisi tunaweza tukenda sisi hakuna matatizo lakini tunayazalisha matatzo kwa vizazi vyetu vinavyokuja. Sisi tumezungukwa na bahari huko chini yetu kuna maji ya chumvi yanapita, kuna maji baridi yanapita, huko

kwenye maji bahari pia huko kuna milizamu ya maji baridi. Sasa milizamu ya baridi ile tunaweza tukachimba tunaona maji haya ni maji baridi kumbe ni maji baridi yenye mlizamu uliokwenda pwani.

Tukiendelea kuchimba hivi ukija mlizamu ule kwa sababu pengine tutakuwa *below sea level* maji yale yanakuja zake huku tunaanza ku-*create* chem chem ambazo kwa kweli zinaweza zikaleta maafa makubwa makubwa. Natoa mfano Bwawa hilo hapo la Mwanakwerekwe pale pamechimbwa pasingekuwa vile pale wala pasingefurika hata siku moja pamechimbwa mchanga. Sasa tujifunzeni kutokana na matatizo kama yale na matatizo kama yale si hapo tu yapo mwahala mwingi, tumesababisha maji kukaa mahala ambapo tungepatumia kwa chakula.

Sasa mimi nasema mpango huu wa kuzuia uchimbaji holela kwa lengo la kuhifadhi ardhi yetu ili isipotee. Hakuna sababu kwa nini tusiunge mkono, hakuna sababu kabisa tusiunge mkono, tuelimishane hadi tufikie pahala watu wetu waelewe lengo wasione kama wanaonewa la kuhifadhi ardhi hii.

Baada ya kusema hayo nadhani nimeyagusia kama nilivyosema mwanzo kwamba nitazungumzia historia kidogo, nitazungumzia takwimu ambayo nimezisema hapa takwimu zilivyo na nathubutu kusema kwamba takwimu ni vielelezo vinatosha kabisa. Ukipewa takwimu utaweza kujifunza mambo mengi kwenye takwimu. Takwimu zinaonya, takwim zinafundisha, takwimu zina kila kitu. Hapa kitabu hichi karibu asilimia hamsini ni takwimu.

Humu mna takwimu zimeorodheshwa kwa njia ya *table* kuna takwimu zimeorodheshwa kwa njia ya *pie chart* ni hii hapa, kuna takwimu humu zinaonesha kwa njia ya *histogram* yale ma-*block graph* na takwimu zimeonesha kwa njia ya *linear graph* yote haya ni kutuelemisha namna gani wenzetu hawa jinsi wanavyofanya kazi kwa ustadi.

Na kweli niseme kwamba kitabu hiki kimeandikika kitaalamu kama kuna matatizo madogo madogo ya makosa madogo madogo haya ni makosa ya kimaumbile...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Dr. Makame Ali Ussi: Dakika mbili enh! Ahsante sana kwa kunibatanabahisha. Nilitaka kukwambia mwanzo kwamba ukiona *time* yako naichukua unambie na nitakuwa tayari kuambiwa. Na mimi niko tayari kukuachia muda wako ili nisikupotezee muda wako.

Lakini sasa mimi nathubutu kusema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, mia kwa mia na Mwenyezi Mungu awasaidie wafanikishe tupate chakula. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Anaefuata ni Mhe. Mussa Foum Mussa na baadae atafuatia Mhe. Masoud Abrahaman na kama muda utatosha atafuata Mhe. Said Omar kwa dakika tano.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sema utaratibu kanuni ya ngapi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Taja kanuni unayosimamia.

Mhe. Jaku hashim Ayoub: 63 Mhe. Mwenyekiti, sijui kama unayo hapo hiyo mimi naijua kichwani hiyo.

Note yangu nilileta toka asubuhi nataka muongozo wa kiti chako haijaonekana au bahati mbaya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae. Umo katika orodha kwa hiyo subiri orodha ikifika utaitwa. Mhe. Mussa Foum Mussa endelea.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri pamoja na watendaji wake wote kwa jitihada zao walizozifanya katika kipindi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kusema kwamba nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ya visiwa ndogo. Mhe. Mwenyekiti, inataka uangalifu mkubwa kuhusu suala la kuishi kwetu, kwa sababu nchi hii tunategemea tulime humu humu na tuishi humu humu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kidogo tunajenga sehemu ambazo kwa za rutuba kwa ajili ya kilimo tunaziacha sehemu za mawe ambazo kuwa hazina rutuba nzuri, baada kunatokea matokeo ya uharibifu. Nitoe mfano

na mfano mzuri tunao Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Kijichi, Mwera, Fuoni hizi ni sehemu za rutuba nazo zilikuwa zina minazi mingi lakini leo ndio sehemu zilizojengwa ukiangalia Zanzibar tulikuwa tunajisheleza kwa nazi, nazi hapa zilikuwa zinafanywa mbata zinasafirishwa. Leo sisi wenyewe nazi sasa ikiwa huna 1500 huipati nazi haipo.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kama alivyoliangalia suala la mchanga katika masuala ya nchi yetu ilivyo, kwa hivyo na suala la kujenga na kulima aliangalie vizuri, tunaishauri serikali iangalie vizuri kwa sababu nchi yetu ni visiwa watu wanaongezeka ardhi ndio ile ile hapo pa kulima hivi sasa tunawaniana hapo hapo huwezi ukapata sehemu ya kulima hata ekari tano huwezi ukapata kulingana na sehemu hiyo hiyo unayoitaka wewe na mwenzako ni hiyo hiyo. Sasa namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie vizuri aangalie namna ya utaratibu wa kujenga watu wasiachiwe kujenga kwenye mabonde ambayo mabonde hayo hayo tunategemea tulime mpunga na baadae zinatokea athari watu siku za mvua watu wanapata hasara kubwa.

Mhe. Mwenyekiti ,baada ya hapo vile vile niendelee kusema kwamba nije katika suala la wakulima. Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu la Kiwani wananchi wengi wa kule wanategemea kulimo na nataka niseme kwamba na mara hii walikuwa wamejitayarisha vizuri kwa kilimo. Lakini kama tulivyoona kwamba kipindi chetu hichi cha mvua zilikuwa nyingi hususan Pemba wakulima wengi vipando vyao vimeharibika. Kwa mfano jua lilikuwa kali baada ya mvua wakulima wamejitahidi kutafuta mbegu za muhogo, mahindi, kunde lakini hizi zote baada ya kuota tu mvua imetokea na vipando vyote vimeharibika. Hivi sasa hawa mbegu ya muhogo kupanda tena, mahindi hawana, kunde hakuna.

Sasa namuomba Mhe. Waziri hili suala kwanza alijue baadae afuatilie kwa wakulima wetu alau na yeye kwenda kuwapa moyo alau wa kuwategemeza alau watapata mbegu wapi tena. Sasa hili suala namuomba Mhe. Waziri ajtahidi aende na yeye au watendaji wake wote wale wanaohusiana na mambo haya basi waende wakaangalie je, vipi sasa wakulima tutawasaidia ili na wao hali si nzuri hivi sasa maana yake watu huwa wanategemea katika vipando vile vile alau wapate mboga ziwasaidie kimaisha. Lakini hali si nzuri mvua Mwenyezi Mungu kafanye rehema zake na la Mungu halina makosa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende katika kitabu kidogo kuna muelekeo wa wizara. Muelekeo wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika mwaka 2017-2018. Mimi hapa kidogo nataka nisome ukurasa wa 47 sehemu c naomba ninukuu:

(c) Kuendeleza uzalishaji wa mazoa ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo vanila na pilipili hoho;

Sasa hapa mimi nataka niizungumzie hii pilipili hoho. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafahamu kwamba kwetu sisi hususan Muambe hichi kilimo cha pilipili hoho kilikuwa ni maarifu na kinalimwa sana.

Sasa Mheshimiwa alipoileta hii kwa sababu kipindi kikubwa pilipili hoho imepotea hailimwi alipoileta hii kwanza nimpongeze kwa muelekeo wake huu wa kufanya matayairisho ya kukirejesha tena kilimo hichi cha pilipili hoho. Lakini nataka nimwambie basi namuomba ikianza hii shughuli basi ianzie hata kule kwenye jimbo langu kwa sababu nathubutu kusema kwamba ndiko asili yake kubwa kwa kule Pemba. Nataka nimwambie kwamba ajitahidi aende akaelimishe wananchi kwa sababu viko vikundi vingi tu hususan vya wanawake, hili suala wanaweza wakalipokea vizuri na wakapata maendeleo ya kuwasaidia katika maisha. Lakini nataka nimuulize Mhe. Waziri, je hivi sasa hii pilipili hoho katika soko la ulimwengu ni bei gani, ili wananchi wetu washajiike ikiwa bei itakuwa nzuri. Kwa mfano, kama karafuu hivi sasa watu wameshajiika sana kuchuma karafuu kwa sababu ya bei. Sasa je, hii pilipili hoho nayo bei yake ni nzuri kwa sababu na huu uchumaji wake unamtihani. Kwa hivyo, kifupi namuomba Mhe. Waziri hili suala alichangamkie vizuri.

Baada ya hapo vile vile niende kwenye programu ndogo ya maendeleo ya uvuvi. Hii iko katika ukurasa wa 64, lakini mimi nataka niisome alama (d) hii iko katika ukurasa wa 65 inaelezea hivi:

Kifungu cha 94(d)

"Kuwaendeleza wavuvi vijana Unguja 10 na Pemba 10, kuvua katika kina kirefu cha maji".

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi bado sijafahamu vizuri, kwa sababu inaeleza kuwaendeleza wavuvi vijana 10 Unguja na 10 Pemba katika kina kirefu cha maji. Je, kuwaendeleza vipi, kwa kutumia chombo gani na je, mbona hii idadi ndogo. Hawa anawaendeleza kwamba waende wakasome baadae waje wawafundishe wenzao au wanawaendeleza vipi. Sasa namuomba Mhe. Waziri kwanza hii idadi naiona ya vijana 10 Unguja na vijana 10 Pemba kuvua katika kina cha maji marefu.

Sasa aje atueleze je, vijana hao wataendelezwa kwa njia gani ya kuvua, watatumia nini au wao wataendelezwa baadae waende wakasomeshwe baadae waje wawasomeshe wenzao au vipi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hapa atakapokuja hili suala atufafanulie vizuri ili na sisi tufahamu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika barabara ambazo zilifadhiliwa kwa ile miradi ya *MIVARF* ni barabara yetu ya Mtangani, kutoka Ukutini mpaka Mtangani Pwani. Lakini kama walivyosema wenzangu kwamba barabara zile zimewekwa kifusi na mvua hizi sehemu nyengine zitakuwa ngumu kupitika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ikiwa barabara hizi bado hazijakabidhiwa kwa serikali, basi aende akazikaguwe, mule ambamo mumeharibika basi mfanyiwe matengenezo kwa sababu nia ya barabara hizi ni kuwasaidia watu walioko vijijini, bado ile nia ni nzuri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hizi barabara ziangaliwe kwa jicho la huruma ili ile azma iliokuwepo basi iendelee kutumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa sababu wenzangu wamechangia mengi. Niliyoyauliza kidogo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho anipe maelezo na mimi nifahamu, kwa sababu na mimi nataka kwenda kuwashajiisha wananchi ili haya mambo mengine kama ya kilimo basi wananchi washajiike.

Baada ya maelezo hayo mimi mwenyewe pamoja na wananchi wa Jimbo la Kiwani, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe.Mussa Foum Mussa. Naomba nimwite Mhe. Masoud Abrahman, kama muda utakuwepo atatumia dakika tano Mhe Said Omar Said.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana jioni hii kwenye kikao hiki adhimu. Lakini ni kushukuru pia na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kwenye kilimo cha kutegemea mvua. Mhe. Mwenyekiti, kilimo hiki sasa hivi kwa Zanzibar kinaonekana kinafeli. Kwa nini niseme kinaonekana kinafeli, kwa jinsi ya hali ya hewa inavyokwenda. Jua likitoka kali sana basi ikianza mvua inaanza moja kwa moja. Kwa hivyo, wakati wa jua kali matrekta hayawezi kulima katika maeneo.

Lakini na inaponyesha mvua matrekta hayawezi kuingia bondeni yakaweza kufanyakazi.

Kwa hivyo, niiombe tu wizara iandae utaratibu mbadala ili tuhakikishe konde zetu hizi zinaweza kulimika kwa ule wakati muafaka, kwa sababu sasa hivi mabadiliko ya hali ya hewa yanasababisha kilimo cha kutegemea mvua kinatuletea tabu. Kwa mfano, mara hii wizara imejikubalisha kuweka mashamba ya mfano heka 50 kila wilaya, lakini heka hizi wanapewa pembejeo za aina zote na baadae wataweza kurejesha, lakini kwa bahati mbaya sana kilimo hiki hakikwenda vizuri. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake waweze kuandaa angalau utaratibu mzuri wa kuweza kukiandaa kilimo hiki cha kutegemea mvua.

Mhe. Mwenyekiti, kilimo hiki kinategemea matrekta lakini inaonekana kuna upungufu mkubwa serikalini wa matrekta. Mhe. Waziri alisema kuwa tayari kishaagizia matreka, lakini naomba matrekta hayo yaliyoagizwa basi waende wataalamu wazuri kuyaangalia ili matrekta hayo yawe na viwango, kwa hali ya ardhi sasa hivi Zanzibar wakati wa jua kali inakuwa ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili ili tulime vizuri ni lazima tupate mbegu bora. Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa mara hii mbegu haikuwa nzuri sana. Mbegu unaletewa ndani ya kipolo muna mipunga zaidi ya aina tatu, lakini pia kuna mchele. Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua mimi unapotafuta mbegu bora ni lazima uanze pale wakati wa kuiatika. Unatafuta mbegu bora lakini mpaka mpunga unaupandikiza vizuri, mpunga ule unaupalilia vizuri, mpunga ule wakati wa kuchanua unakwenda kuchagua mbegu zilizokuwa sio mbegu bora. Lakini sasa hivi inaonekana watu wanafanya biashara kwenye huu mpunga ambao unafanywe ni mbegu bora, hatima yake ndio tunajikuta unaletewa mpunga kwenye kipolo, humo humo mna *Super DC*, humo humo mna *Super Bikeni* na humo humo mna mchele. Sasa kwa kweli mbegu bora hatutoweza kuipata. Kwa hivyo, niwaombe watu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wajitahidi wanapowaandaa watu wa kuandaa mbegu bora, basi wawe wanatumia utaalamu na wawafutilie kwa ukaribu. Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, iwe ile mbegu hawaendi kuipiga kwa magongo wakati wa kupiga ule mpunga, ili tusiletewe mchele ikawa tunaambiwa ndio mbegu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo suala hilo hilo niende kwenye suala la mbolea. Niwaombe sana Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, serikali inapoteza pesa nyingi sana kununua mbolea lakini pia inafidia kwa wakulima. Mbolea ile ile ukienda kuiuliza Mlandege utaambiwa bolo shilingi 60,000/- au 50,000/-, lakini serikali inafidia mpaka shilingi 50,000/-. Kwa

bahati mbaya sana unamkuta mkulima mbolea inatoka serikalini lakini anauziwa kwa bei ya juu. Kwa hivyo, niwaombe wafuatilie kwa ukaribu, ili azma ya serikali, azma ya Rais wakulima wetu wapate mbegu kwa bei nafuu iweze kubakia.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze mara hii Wizara ya Kilimo wamejitahidi sana kututafutia dawa iliyo bora, kweli nawapongeza katika kipindi hiki. Ukitoka tu na dawa yako ukienda kondeni ukipuliza magugu yanakufa kama inavyotakiwa. Kwa hivyo, hilo nasema niwapongeza.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Waziri kachukua ahadi hapa na katuomba bajeti yake ipitishwe, ili akitimiza miaka miwili mitatu lengo lile la umwagiliaji wa kuagiza mchele mwingi nje ya nchi liweze kuondoka. Mimi nimpongeze kwa hilo na uwezekano huo upo. Haidhuru kuna tatizo kwa Zanzibar, kwa sababu wenzetu Tanzania Bara wanafanikiwa kupata mpunga mwingi kwenye eneo dogo wakitumia utaalamu kwa sababu maji yao hawayatoi chini ya ardhi. Sasa hivi kumekuwa na uzito mkubwa kwa watu wa kilimo cha umwagiliaji maji kwa Zanzibar, kwa sababu wenzetu wa Shirika la Umeme wamekabwa na watu wa Tanzania Bara kwa ajili ya umeme wao. Kwa hivyo, ule umeme ambao tulikuwa tukiupata zamani tunaenda kwenye kilimo cha umwagiliaji unatumia tu yale maji, sasa hivi haupo. Ni lazima mkulima atowe shilingi 30,000/- kulipia *plot* moja ili aweze kulima kwa msimu.

Kwa hivyo, niiombe serikali Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kasema kwa mara hii anategemea kuandaa maeneo ambayo watayatega maji. Lakini maeneo yote aliyoyataja ni maeneo madogo tu ya umwagiliaji, kuna maeneo makubwa ya umwagiliaji kayawacha. Kwa hivyo, nimuombe sana yale maeneo makubwa ambayo yanaumwagiliaji na maji mengi yanapita wakati wa mvua za masika, waandae utaratibu serikali waweze kuyatega haya maji ili wananchi wetu ikifika wakati waweze kulima vizuri bila ya kutegemea maji yanayotoka chini ya ardhi. Bado nasema maji yanayotoka chini ya ardhi ni gharama kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa hili analolipigia debe mbegu ya shadidi, ni kweli mbegu ya shadidi unalima eneo dogo lakini pato lake linakuwa kubwa. Lakini mbegu hii bado niseme lile suala la taaluma ni lazima aongeze fedha kwenye eneo lile, kwa sababu mbegu hii huwezi kuipanda kama sio mtu uliopata mafunzo. Kwa sababu mbegu unatakiwa uipande katika muda mfupi tu baada ya kwisha kuiatika ikishatoa miche tu iweze kukua vizuri.

Lakini niombe sana Mhe. Mwenyekiti, zamani ulipokuwa umwagiliaji upo kwa nguvu kubwa na unafanyakazi vizuri sana, kulikuwa na vigari vya kupalilia mpunga, vigari vile ndio vinaweza kupalilia kwenye hiyo mbegu ya shadidi. Lakini sasa hivi tunaletewa tu vigari lakini uwezo wa kupalilia mpunga kwenye maji ni mdogo sana. Kwa hivyo, niombe vile vigari sina uhakika kama vilikuwa vinatoka Korea, au vinatoka China au vinatoka wapi, wavitafute *sample* ile ile, ili waletewe wananchi wetu haidhuru watanunua kwa fedha zilizokuwa sio bei kubwa, ili tuweze kulima kilimo hicho cha shadidi na tuupalilie. Kwa sababu mpunga kama utaupandikiza hukuupalilia vizuri haukupata mbolea hauwezi kuwa mzuri. Kwa hivyo, niombe sana suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri na timu yake. Jana nilimtembelea katika maeneo maeneo, akaniahadi, akaniambia na akanithibitishia kwamba lile eneo ambalo lilitakiwa lilipwe fedha kwa ajili ya kuunga umeme kwenda kwenye bonde la Kizimbani ambalo linaitwa Bonde la Kwajusa, lakini Bumbwisudi pia eneo la Kirundunda tayari wameshawasilisha fedha na wakati wowote kazi inaweza ikafanyika. Kwa hivyo, niwapongeze kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe. Nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na timu yake alituahidi kuwa ng'ombe 368 watatolewa kwa Zanzibar nzima Unguja na Pemba, lakini pia na mbuzi 760 watatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili mimi sina tatizo nalo, lakini naomba sana hili suala la Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe kuna tatizo ambalo huwa linajitokeza, na tatizo lenyewe zaidi inakuwa ni wale madaktari ambao wanatakiwa wawe kwenye wale ng'ombe kwa ukaribu. Nimeshashuhudia kuna eneo ng'ombe anaumwa anaweza akakaa siku mbili bila ya kwenda kutibiwa. Kwa hivyo, kama ng'ombe anaumwa hajatibiwa muda wa siku mbili, basi atawaambukiza wenzake ambao wako pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, na mfumo wa sasa hivi niwapongeze ni mfumo mzuri, maana yake kila lile eneo ambalo wanatakiwa wapewa ng'ombe, wanaambiwa ng'ombe 20 wawekwe pahali pamoja, ili madaktari wakitoka huko wanakotoka waweze kwenda kuwatibu. Kwa hivyo, niombe tu kwenye eneo hili madaktari wawe karibu sana, ili wakulima wetu waweze kufanikiwa au kufikia lengo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi mara hii wamejitahidi kulima sana, lakini kwa bahati nzuri, hatuwezi kusema bahati mbaya kwa sababu ni mambo ya Mwenyezi Mungu, watu wameathirika sana na vilimo. Mihogo imeoza kwa maji, mipunga imezama pia na mazao mengine yamezama.

Kwa hivyo, niiombe serikali iwaangalie kwa jicho la huruma, kwa sababu ile mihogo ambayo tuliitegemea tutapata futari mara hii yote imeshazama, naamini kwa hali hii inavyokwenda sasa hivi huwenda kilo moja ya maharangwe sijui itafika shilingi elfu ngapi. Kwa hivyo, kwa wananchi itakuwa ni mzito mkubwa na hasa watu wetu wa vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapa kwenye ukarabati wa barabara. Nilimsikia Mhe. Waziri kuwa atasaidia kukarabati barabara ya Kizimbani. Barabara ile Mhe. Mwenyekiti, ndio inayoingiza watalii kwenye eneo la Kizimbani. Lakini sasa hivi kama Mhe. Waziri atatoka aambiwe aende Kizimbani basi gari yake anaweza akaiweka Mndo.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwanza bajeti ikishapita hili suala usiliweke mwisho wa bajeti, uliweke mwanzo wa bajeti kwa sababu eneo la Kizimbani ni eneo ambalo tunategemea kuingia watalii, watalii wakienda njia wakizikuta ni mbovu hawawezi kuingia katika eneo lile. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, watakapopata hiyo ruzuku basi waliangalie kwa jicho la huruma eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Kizimbani ni eneo la utalii, lakini pale kuna vijana wetu wengi wamejiajiri kwa kupitia utalii. Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo linajitokeza mara kwa mara. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imeweka watu wao Mndo wa kukusanya fedha kwa kila gari inayoingia katika eneo lile. Wananchi au vijana wetu wa eneo lile wanaambiwa kila mtalii kuna dola ambayo amepangiwa atowe. Lakini pia akifika kwenye shamba kuna dola ambazo anatakiwa atowe, pia akifika kwenye eneo la *spice* ambapo kuna vifaa vinavyouzwa, yule *guide* ambaye kamleta yule mtaa na yeye anataka apate chochote kutoka pale, serikali inahimiza vijana wetu wajiajiri, lakini kwa kweli suala hili sasa hivi imekuwa ni tatizo, vijana wa Kizimbani, Dole na Mbuzini wameniita tumezungumza nao. Wanaomba sana Mhe. Waziri au Katibu Mkuu au muhusika yeyote twende tukazungumze nao ili tuwape moyo vijana hawa, na tuwaambie pale kuwa eneo hili ili mtalii aingie ana hitaji kutoa dola fulani na sio vyenginevyo. Kwa sababu inaonekana sasa hivi serikali kama inafanya biashara iliyokuwa haina msimamo. Kwa hivyo, zile fedha wananchi wanataka na wao wazipate.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala hili Kizimbani nako kuna Shehia na kuna matatizo mbali mbali, wenzetu maeneo mengine ya Kusini na Kaskazini kuna mahoteli, mahoteli yale wanapoingia wageni au wale matajiri wenye mahoteli wanasaidia zile Shehia kwa matatizo mbali mbali, ya kielimu, afya na mambo

mengine. Lakini sisi tunategemea Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kupitia watalii na sisi watusaidie japo asilimia kidogo kwenye Shehia ya Kizimbani, kwa sababu tuna matatizo mengi na wananchi wanahitaji kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna neno mara nyingi huwa nalizungumza hapa la wakulima ambao hawajapata hati katika maeneo ya Dole pamoja na Mbuzini. Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Balozi Seif Ali Iddi, lakini pia watu wa Idara ya Ardhi walitusaidia kusimamia mpaka suala hili likakaa sawa, na baadhi ya wakulima wetu wakapatiwa hati miliki. Lakini kuna kundi mpaka leo halijapata hati miliki, na hati zile sio kuwa mtu aweke majumba yake na nini, ni hati za muda ambazo mwananchi atapata kulima afaidike kula yeye na familia yake. Lakini sasa hivi inaonekana ni muda mrefu, na kila siku tukikaa nao kwenye vikao mbali mbali wanatuuliza. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe tu kwa kushirikiana na waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi, suala hili mulizungumze ili ikifika kesho kutwa basi muweze kutupa jibu angalau la kuweza kuwajibu wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ukataji minazi ovyo pamoja na miembe na miti mingine. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wenzangu wameligusia sana. Lakini mimi nataka niseme suala hili itafika wakati Zanzibar minazi na sisi itakuwa ni historia. Kwa sababu sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, ukipita kwenye barabara zote. Ukenda barabara ya Melisita, ukija barabara ya Dole, ukienda barabara ya Kitope kwenye barabara kuna maduka ya miti na vitu vyengine. Katika miti sasa hivi unayoikuta barabarani inauzwa zaidi ya asilimia 70 ni minazi. Madawa ya kulevya huyakuti kuuzwa kama vile serikali inakemea. Kama ingekuwa hao wanaokata minazi huko mabondeni wanakokata hawaonekani lakini ile miti iliyokwisha kuwekwa barabarani haionekani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri pamoja na watendaji wako suala hili likisimamiwa vizuri basi minazi itakuwa haikatwi Zanzibar. Kama kuna sheria itasimama sheria, kama hakuna sheria basi itengenezwe sheria ili minazi iendelee kubaki vizazi na vizazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea naomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri aniambie. Kwa bahati nzuri mimi natembelea sana kwenye lile shamba la kilimo la Kizimbani. Wananchi wetu sasa hivi unapofika msimu wa tungule na embe basi yule ambaye sio mlaji wa embe itabidi ale embe kwa sababu unazikuta embe 10 dodo zinauzwa kwa shilingi 1,000. Lakini sasa hivi ukienda kuiuliza embe moja ya dodo inaweza ikafika ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Masoud Abrahman, naomba umalizie dakika moja iliyobaki.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Embe hiyo unaweza kwenda kuinunua moja shilingi 2,000, sababu ya kukuambia hili Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka tulikwenda kuweka jiwe la msingi Kizimbani kwenye Kiwanda cha Kusagia Matunda. Kwa hivyo, utakapokuja utuambie jengo lile mpaka leo limefikia hatua gani na ni lini tunaweza kupata taarifa nzuri ambayo itakuja kutuelimisha na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho nizungumzie barabara hizi za *MIVARF*. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, barabara hizi sasa hivi zimekuwa kama ni tatizo. Kuna maeneo leo asubuhi nilikwenda kukagua mipunga yangu basi na mimi nimekwama na gari yangu. Kila eneo ambalo halikutiwa kalbi zile za kupitisha maji chini zimechimbuka na hazipitiki. Serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini pia kwa kupitia Idara ya Barabara, naomba kuandaliwe kamati ili zipitie hizi barabara, kwa sababu hiki kilio kimekuwa kikubwa, ili tuweze kuondoa hili tatizo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi niseme tu naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa asilimia 98 na asilimia 2 mpaka atakaponipa majibu yangu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu hoja iliyokuwa mbele yetu wachangiaji iwe ni mwisho huyu ambaye amechangia muda huu kwa leo na Jumatatu tunatarajia kuweza kufanya majumuisho. Naomba sana wachangiaji nitakaowataja hapa waweze kuchangia kwa maandishi, ambao ni Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwanza), Mhe. Shamata Shaame Khamis, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Shaib Said Ali, Mhe. Said Omar Said, Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei).

Waheshimiwa Wajumbe hao wote niliowataja watalazimika kuchangia kwa maandishi na ni vyema wachangie Jumatatu ili tuweze kuendelea na hatua iliyobakia ya majumuisho. Baada ya hapo niwashukuru sana kwa utulivu wenu, na michango yenu kwa wizara hii na hadi hapa ndio mwisho wa kikao chetu cha leo. Naomba niahirishe mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi tukijaaliwa.

(Saa 1:39 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 29/05/2017 saa 3:00 za asubuhi)